**21 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 21 Juni, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, namuita Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, aweze kuuliza swali lake.

Na. 681

**Hitaji la nyumba kwa watumishi wa umma waliopo vijijini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza: -

Je, ni nyumba ngapi zinahitajika kwa Watumishi wa Umma waliopo Vijijini?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimwa Mwenyekiti, ni kweli kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za watumishi waliopo vijijini hususan watumishi wa kada ya elimu na afya. Hadi Mei, 2023, idadi ya nyumba za walimu zilizopo vijijini ni 55,097 wakati upungufu ni nyumba 255,097. Aidha, kwa upande wa watumishi wa afya, nyumba za watumishi zilizopo ni 7,818 na upungufu ni nyumba 15,272.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kupitia Mradi wa *SEQUIP,* Serikali imekamilisha mchakato wa kujenga nyumba 212. Serikali itaendelea na jitihada za kukabiliana na upungufu wa nyumba za watumishi wa kada za elimu na afya hususan waliopo vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa ukosefu wa nyumba unasababisha walimu na hao wafanyakazi wa Serikali kuchelewa, lakini katika vijiji vingine kuna nyumba za wananchi ambazo hawaishi huwa wanakuja tu wakati wa sikukuu ikiwemo *Christmas*. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuziagiza Halmashauri ziingie mkataba na hawa watu wenye ma–*bungalow* huko vijijini ili waweze kupatia wafanyakazi nyumba za kuishi?

Swali la pili, upungufu ulioandikwa ni mkubwa sana, hata tungejenga kwa miaka 10 bado hatutatosheleza. Serikali inasema nini sasa kuongeza hela zaidi katika mfuko huo wa ujenzi ili hii kazi iende kwa uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kuhusu Serikali ina mpango gani kuingia mkataba. Hili ni jukumu ambalo linaachiwa Halmashauri wenyewe kuweza kuingia mikataba na wenye nyumba ambazo hazitumiki na naamini hili Mheshimiwa Mbunge amelileta kwa sababu kule Mkoa wa Kilimanjaro wengi wanakuwa wapo katika Mikoa mingine na wanarudi kipindi cha mwisho wa mwaka. Kwa hiyo, tutakaa na kuona ni namna gani tunaweza tukazungumza na Halmashauri ambazo zina mazingira kama ya Mkoa wa Kilimanjaro, kuona ni namna gani wanaweza kuingia mikataba hii kwa ajili ya kuweza kuwaweka watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la hela ya ujenzi. Ni wajibu wa Halmashauri kuanza kuweka fedha, kutenga fedha katika mapato yao ya ndani kwa ajili aya ujenzi wa nyumba za watumishi wa kada ya elimu na afya. Serikali Kuu tayari imeshachukua jukumu kubwa sana, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, amepeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa maboma, madarasa katika Halmashauri hizo na ukamilishaji wa maboma lakini vilevile katika afya ameshapeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Kwa hiyo, ni wajibu wao sasa kuanza kuunga mkono jitihada zile za Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga na kukamilisha maboma yaliyojengwa na wananchi kwa ajili ya nyumba za watumishi wa umma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, namuita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko aweze kuuliza swali lake.

**21 JUNI, 2023**

Na. 682

**Ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Mkoa wa Mara**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata za Mji wa Tarime kwa kuwa kuna Kituo kimoja tu cha Afya Nkende?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati cha Ketare katika Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa kujenga jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* Maabara, Jengo la Wazazi, Jengo la upasuaji na Jengo la Kufulia na ujenzi umekamilika na kituo kimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya katika Kata za kimkakati kote nchini, zikiwemo Kata za Mji wa Tarime.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za pembezoni katika Halmashauri wa Mji wa Tarime ni pamoja ya Kata ya Nyandoto na Kata ya Kenyamanyori. Wananchi wa Kata ya Kenyamanyori walishaanza kujenga kituo cha afya kwa nguvu zao wenyewe na baadhi ya maboma yamekamilika kuanzia mwaka 2019, Serikali iliahidi kwamba itapeleka fedha kuhakikisha kwamba kituo kile kinakamilika maana wako nje ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua *commitment* ya Serikali sasa ni lini watapeleka fedha ili waweze kukamilisha Kituo cha Afya cha Kenyamanyori kupunguza adha ambayo wanaipata kuja kupata huduma kwenye hospitali ya Mji wa Tarime?

Swali langu la pili, katika Kata za Susuni na Mwema katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ni Kata ambazo zipo pembezoni na wanapata huduma sana sana wakienda kituo cha Sirari kule au hospitali ya Nyamwaga lakini wengi wanakuja Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tarime. Ninataka kujua ni lini Serikali itahakikisha kwamba Kata hii ya Susuni na Kata ya Mwema na zenyewe zinapata vituo vya afya ili kuweza kupunguza adha ya wananchi wale kusafiri mwendo mrefu kutafuta huduma ya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Matiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kwanza la lini fedha itakwenda kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kenyamanyori.

Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Kenyamanyori kwa kuweza kuanza kwa jitihada zao wenyewe ujenzi wa kituo chao cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fedha tutatuma timu pale ya Mganga Mkuu wa Mkoa kwa ajiili ya kufanya tathmini ya ujenzi ule ambao umefanyika na kuona kama vinakidhi mahitaji yanayotakiwa ili kusajili kituo cha afya kipya katika Kata ile na baada ya tathmini ile wataiwasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha ya kupeleka kuunga mkono juhudi hizi za wananchi wa Kenyamanyori kumalizia kituo kile cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la Kata ya Susuni na Mwema zilizoko kule Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Tutafanya vivyo hivyo kama ambavyo nimemjibu swali lake la kwanza la kuhakikisha timu ile inapoenda Tarime Mji, wafike vilevile kwenye Halmashauri ya Wilaya Tarime na kufanya tathmini katika Kata hizi mbili ambazo amezitaja Mheshimiwa Matiko na kisha walete taarifa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili tuweke katika mipango yetu ya kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba tunapeleka kwa ajili ya kujenga vituo hivi vya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Wananchi wa Tarafa ya Msitu wa Tembo wamekuwa na changamoto kubwa ya kufuata huduma za afya kwa umbali mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea wananchi hao kituo cha afya?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga vituo hivi vya afya ambavyo ametaja Mheshimiwa Regina Ndege, katika mwaka wa fedha unaofuata tutaangalia kama kuna fedha iliyotengwa kujenga kama hakuna tutatenga katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH A. MRIMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini, sasa Serikali itatusaidia fedha ya nyongeza kwa ajili ya ukamilishaji ujenzi kituo cha afya Machochwe kama tulivyoomba? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Mheshimiwa Mrimi amekuwa akilifuatilia sana kuhusu fedha hizi za Kituo cha Afya Machochwe na tutaendelea

kama ambavyo nimeonana naye ofisini mara kadhaa kumueleza kwamba, tunaangalia namna gani bora tutapata fedha ya kumalizia kituo hiki cha afya na pale ambapo Serikali itapata fedha basi tutapeleka katika kituo hiki cha afya cha Machochwe ili kiweze kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Namuita Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 683

**Uanzishaji wa *SACCOS* katika Mikoa 16 nchini**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, lini *SACCOS* 130 za wanawake na vijana zitaanzishwa katika mikoa 16 ikiwemo Kigoma kama ilivyoainishwa katika Ilani ya 2020/2025?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ninaomba kujibu swali Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa jumla ya *SACCOS* 41 kwenye Mikoa 16 zikiwemo *SACCOS* 03 za Mkoa wa Kigoma. *SACCOS* hizo ni *Kasulu Women SACCOS* yenye wanachama 100 ikiwa na mtaji wa milioni 44, *Vijana Kidahwe SACCOS* yenye wanachama 20 ikiwa na mtaji wa milioni 14, na *Amani Wanawake SACCOS* yenye wanachama 33 ikiwa na mtaji wa milioni 21.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha Mikoa ikiwemo Mkoa wa Kigoma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuanzisha na kuzisimamia *SACCOS* kama

ilivyoainishwa kwenye Ilani ili ziendelee kutoa huduma inayokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Sylvia Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kutokana na majibu ya Serikali utaona kabisa bado tuko kwenye asilimia 31.5 ya utekelezaji, hii inaonesha bado kazi inatakiwa kufanyika. Nataka kujua ni nini mkakati maalum wa Serikali, kuhakikisha wanawake wengi na vijana wengi wanapata uelewa na umuhimu wa masuala haya ya *SACCOS* ili waweze kujiunga wajikwamue kiuchumi?

Swali la pili, kulikuwa na *VICOBA* vingi vya wakinamama na vijana. Je, Serikali iko tayari kuviwezesha vitambulike rasmi ili viingie kunufaika kwenye mikopo ya asilimia 10 katika mfumo huu mpya unaokuja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvia Sigula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza la mkakati maalum wa Serikali kwa ajili ya kutoa elimu kwa wingi zaidi ili kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na Majiji na Halmashauri za Miji, zina utaratibu na watumishi waliokuwa kule Maafisa Biashara, Maafisa Maendelo ya Jamiii pamoja na Maafisa Ushirika. Ni wajibu wao kuhakikisha kwamba wanasajili vikundi vingi zaidi au *SACCOS* nyingi zaidi kwenye maeneo yao na kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa *SACCOS* hizi. Hivyo basi, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaelekeza tena Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya hapa nchini kuhakikisha hawa niliowataja Maafisa Biashara, Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Maafisa Ushirika

wanafanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya kuweza kutoa elimu juu ya umuhimu kuwa na *SACCOS* na kusajili *SACCOS* nyingi ambazo zinakidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la *VICOBA* kutambuliwa zaidi na kupewa mikopo. Hili linategemeana vilevile na wao *VICOBA* kukidhi vigezo vile vya masharti ya mikopo ile ya asilimia 10. Hata katika mapitio yanayofanyika kwa maelekezo yake Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, juu ya utoaji wa mikopo hii bado mikopo hii itakuwa ni ya vijana, wanawake na walemavu. Kinachofanyika ni *review* ya namna ya utoaji wa mikopo ile, siyo ubadilishwaji wa namna mikopo ile inavyotolewa kwa watu. Kwa hiyo, kama vikundi hivi vitakuwa vinakidhi vigezo, *VICOBA* hivi kwamba vina vijana, vina wanawake na walemavu, vinatakiwa pia kunufaika na mikopo ile inayotolewa. Kwa hiyo, tutazingatia hili pia katika timu ile inayofanyia mapitio haya ili waweze kuongeza *SACCOS* nyingi zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Halmashauri hakuna sheria inayoruhusu vikundi vya *SACCOS* kukopeshwa. Je, ni lini Serikali italeta sheria Bungeni ili kufanya marekebisho *SACCOS* ziweze kukopeshwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ile ya Fedha za Serikali za Mitaa ambayo inaelezea namna ya utoaji wa mikopo ya vikundi, tayari kama nilivyokuwa nikimjibu Mheshimiwa Sigula kwamba kama *SACCOS* hizi zinakidhi vile vigezo vilivyotajwa kwenye Sheria ile ya Fedha ya Serikali za Mitaa, ya kuwa ni kuna vijana kwenye *SACCOS* hizo, ama *SACCOS* hizo zinaongozwa na walemavu au wanawake watastahili kupata fedha hizi za vikundi za asilimia 10,

haina haja ya *SACCOS* hizi tena kusajiliwa kama vikundi kwa sababu tayari ni *SACCOS* zilizosajiliwa na kama viongozi wao wale mwenyekiti, katibu na muweka hazina wanakidhi vigezo vya umri kwa vijana na ni wanawake au walemavu basi wanastahili kupata mikopo hii ya asilimia 10. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, anayefuata kuuliza swali ni Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Zahor.

Na. 684

**Mpango wa kuendeleza ekari 1000 za Shirika la Elimu Kibaha**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza eneo la ekari 1000 za Shirika la Elimu Kibaha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEORGRATIUS J. NDEJEMBI)** aliuliza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Elimu Kibaha lina eneo lenye ukubwa wa hekta 1,358 katika Mji wa Kibaha. Eneo lenye ukubwa wa hekta 675.31 limeendelezwa kwa huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika. Aidha, eneo lenye ukubwa wa hekta 220.1 limetengwa kwa ajili ya upanuzi wa huduma za Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lenye ukubwa wa hekta 170.913 limetengwa kwa ajili ya kuanzisha shamba darasa la kilimo cha umwagiliaji *(block farming)*. Aidha, Shirika limetenga eneo lenye ukubwa wa hekta 38.84 kwa ajili ya uwekezaji *(investment hub)* lililopo mkabala na barabara ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lililobaki lenye ukubwa wa hekta 252.837 linatumika kwa ajili ya huduma nyingine za kijamii ikiwemo Makanisa na Misikiti na lina miundombinu ya umeme, maji na limepitiwa na bomba la mafuta (*TAZAMA)*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza. Umeridhika? Haya tunaendelea.

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, namuita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay aweze kuuliza swali lake.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naishukuru Serikali kwa sababu, swali hili ni la mwaka jana 2022. Nina swali dogo tu la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa utekelezaji wa uwekaji wa lami katika barabara ya Mbulu kwenda Garbabi umeanza na unatekelezwa na kampuni ya Kichina: Serikali ina mpango gani wa kwenda kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi wale ambao barabara ile kwa jiografia ya milima inahama kwenda kwenye makazi yao ili wapate fidia pamoja na elimu zaidi kwa ajili ya kutoa ushirikiano kwa mkandarasi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge arudie swali ili niweze kumwelewa vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, rudia swali lako.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hivi sasa kampuni ya Kichina inatekeleza ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mbulu kwenda Garbabi kilometa 25, lakini barabara hiyo kwa jiografia ya milima inahama kwenda nje ya mita 22.5 kutoka katikati ya Barabara: Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kwenda kuwaelimisha wananchi ili tujue

wanaofidiwa na wasiofidiwa ndani ya *corridor* hiyo ya barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyo utaratibu kwamba pale ambapo tunajenga barabara tunatumia sheria za barabara na hasa kwenye kutoa fidia. Kwa wananchi ambao wako ndani ya mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kwa pande zote wanakuwa wako kwenye hifadhi, lakini wale ambao wako mita 7.5 kwa pande zote ambazo zimeongezeka, barabara inakuwa imewafuata, na hao kwa kweli wanatakiwa wafanyiwe tathmini, waainishwe na walipwe fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina hakika kama hivyo ndivyo, Mheshimiwa Mbunge suala hilo litafanyika kwa hao wananchi wa Mbulu hadi Garbabi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naomba kufahamu kwenye mikataba iliyosainiwa, barabara ya Hydom – Mogitu yenye urefu wa kilometa 68, ipo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Haydom – Mogitu ilikuwa ni sehemu ya barabara ya *Serengeti Southern Road* wakati wa *design* ya awali, lakini katika mpango huu wa *EPC + F* barabara hii kwa sasa tunaifanyia usanifu, maana ilikuwa imefanyiwa usanifu wa awali, sasa tumeiingiza tuifanyie usanifu ili

tutakapokamilisha hiyo barabara ambayo ni ya *EPC + F* tuweze kuijenga hiyo pia kwa sababu ndiyo inayounganisha barabara ya Hydom kwenda Sibiti na barabara ya Singida kwenda Babati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Dumila kwenda Kilosa, kutoka Kilosa kwenda Mikumi kupitia Masanze – Zombo – Ulaya na Muhenda mpaka Mikumi ni uti wa mgongo kwa uchumi wa Mkoa wa Morogoro: Nini Kauli ya Serikali kuhusiana na hali ya barabara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dennis Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Londo kwamba, kwa kweli hiyo ni barabara muhimu sana na hasa tutakapokamilisha hii barabara ya kutoka Lumecha – Malinyi – Kidatu hadi Mikumi. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba, kwa sababu ya umuhimu wake, katika bajeti inayokuja tumeitengea fedha ili kuendelea kuijenga kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Kilosa na Mikumi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini barabara ya Chombe – Kaoze – Igonda mpaka Ilemba itajengwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza ni kuifanyia usanifu wa kina hiyo barabara halafu baada ya hapo Serikali itajua gharama halisi ya kuijenga hiyo barabara na ndiyo sasa tutaiingiza kwenye mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Barabara ya Igawa – Kinyanambo – Mafinga huko imefanyiwa upembuzi yakinifu kwa muda mrefu na iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu kwa barabara hiyo inayokwenda mpaka Mafinga.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Igawa – Kinyanambo ipo kwenye ilani na kwa kweli, inatakiwa ijengwe kwa kiwango cha lami hasa tukizingatia umuhimu wa barabara hii inayopita maeneo yanayozalisha sana hasa mpunga. Serikali inaendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mpango uliopo ni kuhakikisha kwamba inafanyiwa ukarabati iweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba Serikali imeendelea kujitahidi sana kuhakikisha barabara hii inafanyiwa matengenezo mara kwa mara na kupitika kwa muda wote wa mwaka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Je, ni lini barabara ya Oldiani – Mang'ola – Matala – Lalago itajengwa kwa kiwango cha lami na kuwa ni barabara inayounganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu? Ni Sera ya Wizara ya Ujenzi kuunganisha Mkoa kwa Mkoa. Ni lini ujenzi wake utaanza?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Awack, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyotaja ni kweli, ni barabara kuu, lakini mpango wa Serikali kwa sasa ni kutafuta fedha kwanza kuijenga kutoka Oldiani mpaka Mang'ola kwenye eneo ambalo wanazalisha sana zao la vitunguu. Kadri tutakavyopata fedha, basi tutaendelea kutoka Mang'ola hadi Sibiti kwa kiwango cha lami, lakini kwa sasa Serikali tunafikiria kuijenga kwa kiwango cha lami *Oldiani Junction* mpaka Mang'ola, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Sasa namwita Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, aweze kuuliza swali lake la msingi.

Swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 686

**Ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru yenye urefu wa kilometa 300. Katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa kilometa mbili katika Mji wa Tunduru. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa sehemu iliyobaki, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Barabara ya kutoka Ipogolo kwenda Kilolo imekuwa ikiendelea kutafutiwa mkandarasi kwa muda mrefu. Napenda kujua ni hatua gani zimefikiwa na ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara ya kutoka Ilula hadi Kilolo ambayo kipindi cha mvua huwa inakuwa imeharibika na Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye majibu yake

aliahidi kwamba itafanyiwa matengenezo, hadi sasa kuna maeneo bado: je, ni lini matengenezo hayo yatafanywa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ipogolo – Kilolo yenye urefu usiopungua kilometa 33 ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa Mradi wa *Rise*. Tunapoongea sasa hivi Mbunge atakuwa na wananchi wa Kilolo wanafahamu kwamba, iko kwenye hatua ya manunuzi kwa ajili ya kuanza kujengwa barabara yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili aliyoitaja ya Ilula – Kilolo ambayo anasema mara nyingi inaharibika, ni kweli, eneo hili lina mvua nyingi, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya kipindi hiki cha mvua kwisha wakandarasi wapo, watakuwa muda wote wanaingia *site* kwa ajili ya kuikarabati hii barabara kwa kiwango ambacho itapitika bila matatizo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara inayotoka Tabora Mjini kupitia *Mwanza Road* ambayo inapita Bwawa la Igome mpaka kwenda Mambari - Nzega, ni muda mrefu haina lami na imekuwa ikisuasua: Lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa lami?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichosema Mheshimiwa Mbunge wa Tabora. Nataka tu nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo kwenye ilani na

tumeitengea fedha kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Namwita Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake. Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa niaba.

Na. 688

**Kutafuta masoko ya mazao ya kilimo**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA K.n.y. MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta masoko ya mazao ya kilimo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi kwa kujenga masoko ya kimkakati mipakani, ujenzi wa vituo vya masoko na kuboresha miundombinu ya maabara za *TPHPA* ili ziweze kupata ithibati itakayowezesha kufanya uchunguzi na kutoa vyeti vya ubora vinavyokubalika Kimataifa, kuongeza tija na kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na nchi mbalimbali na kufungua masoko ya mazao katika nchi hizo. Hadi sasa tumefanikiwa kufungua soko la korosho

nchini Marekani, soko la parachichi China, India na Afrika Kusini na tunaendelea kuhudumia masoko ya nafaka katika nchi mbalimbali za Afrika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Stella Fiyao. Mji wa Tunduma ni mji ambao unavuna sana mahindi, na uko mpakani na nchi ya Zambia: Ni lini Serikali itawekeza pale kuhakikisha wakulima wale hawauzi kwa hasara ndani, wapeleke hata nje kwa sababu wao wako karibu na nchi ya Zambia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Zao la kokoa ni zao ambalo hapa Tanzania ni la pili kwa Afrika kwa ubora; na inasemekana zao hili linanunuliwa sana katika nchi ya uingereza: Ni lini mtamsaidia mkulima wa Kyela aweze kuuza zao la kokoa kwa bei nzuri ambayo yeye kama mkulima atanufaika kuliko madalali wa katikati wanaonufaika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mpaka wa Tunduma ni kati ya mipaka ambayo imekuwa ikitumika sana kusafirisha mazao. Nataka tu nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa tunawekeza nguvu kubwa kuhakikisha tunawasaidia wakulima wetu ili mwisho wa siku waweze kunufaika na mazao yao na hasa katika utaratibu wa kurasimisha biashara ya mazao na urahisi wa usafirishaji mazao ili mkulima aweze kunufaika na mazao yake ikiwemo katika mpaka huu wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu kokoa. Ni kweli katika eneo la kokoa tunafanya vizuri, lakini mkulima pia ana haki

ya kupata bei nzuri kutokana na ushindani wa kimasoko uliopo. Kama Serikali tutahakikisha kwamba tunaweka miundombinu rafiki ili kuwaruhusu wakulima wetu kutafuta masoko makubwa nje ya nchi ambayo yatawasaidia pia kupata bei ya uhakika na hasa katika kilimo hai cha kokoa ambacho bei yake imekuwa ni kubwa sana kimataifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daniel Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Wananchi wa Babati Vijijini wanatumia sana zao la mbaazi kama zao lao la biashara: Ni nini mkakati wa Serikali wa kutafuta soko la zao hili la mbaazi kwa ajili ya manufaa ya kiuchumi ya wananchi wa Babati Vijijini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kutafuta soko la uhakika la mbaazi na hasa kwa kuishirikisha Serikali ya India, ikiwa ni mmoja kati ya wanunuzi wakubwa. Wiki moja iliyopita, tulimtuma Naibu Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Kilimo, kwenda India kwa ajili ya kufuatilia yale makubaliano ya awali yaliyokuwepo ya soko la mbaazi na majadiliano yanakwenda vizuri ili tuweze kuwahakikishia wakulima wetu masoko ya uhakika, hasa ya mbaazi ambapo India wamekuwa wanunuzi wakubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imeweka zuio la kuu za mahindi nje ya nchi. Hali hiyo imesababisha bei ya mahindi kushuka. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Mbozi debe sasa hivi ni shilingi 8,000 na bei inazidi kushuka; nini kauli ya Serikali

ili kuwaokoa hawa wakulima ambao kwa sasa wamevunjika moyo na kuporomoka kwa hii bei?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto kubwa ambayo tunaipata katika biashara ya mazao ni uholela. Serikali ilichokifanya siyo kuzuia moja kwa moja. Imetoa mwongozo na kuweka utaratibu wa namna ya kufanya biashara ya mazao nchini Tanzania ambapo tumeelekeza kwamba, hivi sasa kila mfanyabiashara wa mazao, ahakikishe kwanza kabisa anapata *Business License;* pili, awe ana *TIN;* na tatu, kabla hajaenda mpakani kusafirisha mazao, ahakikishe kwamba ameshapata kibali cha kusafirisha mazao nje ya nchi *(Export Permit)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya hivi ni kuweka takwimu sawa, kwa sababu kumekuwepo na wafanyabiashara ambao wanakwenda mashambani moja kwa moja kwa wakulima kwenda kununua mazao na hivyo Serikali kupoteza mapato mengi sana. Serikali ipo kwa ajili ya kuwalinda wakulima na kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei bora tukishawasimamia, kwa sababu ndiyo azma ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba mkulima ananufaika na kilimo chake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia uuzaji wa mazao ghafi nje ya nchi, badala yake yaongezwe thamani kwa kusindikwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi na ndiyo mkakati wa Serikali. Hivi sasa tunajielekeza katika kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa nchini badala ya kuyapeleka ghafi nje ya nchi. Kwa mfano, katika eneo la zao la korosho hivi sasa tunaweka mkakati mkubwa kuhakikisha kwamba, zaidi ya asilimia 60 ya korosho yetu ifikapo mwaka 2025 iwe inabanguliwa hapa ndani na kuongezewa thamani. Hivi sasa tumeshaandaa eneo la Nanyamba kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha ubanguaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika maeneo mengine ikiwemo parachichi na mazao mengine pia, mkakati ni huo huo wa kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu rafiki kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili tuwe tuna mnyororo mzima wa kuongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo na mwisho wa siku kuliongezea Taifa mapato kupitia mazao haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Liko soko kubwa sana la mazao ya kilimohai, kwa mfano pamba yetu ya Tanzania iko namba tatu: Je, ni lini Serikali itaweka angalau kitengo mahususi cha kushughulikia kilimohai katika Wizara ya Kilimo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, mazao mengi ya kilimohai yana soko kubwa na yana uhakika sana wa masoko nje ya mipaka ya Tanzania. Kama Serikali, tumekuwa ni sehemu ya washiriki katika kuhakikisha kwamba tunafanikisha wakulima wetu kuweza kuyafikia masoko hayo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wizara ya Kilimo pia tunaweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba tunashirikiana

na wadau wakubwa wa kilimohai kwa kuweka kitengo maalum ambacho tutakuwa tunashirikiananao ili mwisho wa siku tufanye kazi kwa pamoja, maana wadau wakubwa wa kilimohai ni taasisi nyingi za binafsi ambazo zimekuwa zina mchango mkubwa. Nasi kama Serikali lazima tuhakikishe pia tunashirikiananao. Kwa hiyo, tunao watu ambao ni *focal person* katika Wizara ya Kilimo. Tutaendelea kuwaimarisha ili wafanye kazi kwa pamoja na sekta binafsi kwenye kilimohai.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kwa majibu ya swali namba 688. Tunamalizia swali la 689, namwita Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 689

**Kufufua zao la kahawa nchini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua zao la kahawa nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kufufua zao la kahawa hususan katika maeneo yenye mibuni iliyozeeka, mashamba yaliyotelekezwa na kuanzisha kilimo cha kahawa katika maeneo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hiyo inajumuisha uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya kahawa; kuimarisha maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa ili kudhibiti magonjwa na kuongeza kasi ya uzalishaji wa miche bora; kuboresha mifumo ya masoko ya kahawa ili kumlinda mkulima; kuwezesha matumizi ya

teknolojia za umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa na kuimarisha utafiti na maendeleo kupitia Kituo cha Utafiti wa Kahawa Tanzania *(TaCRI)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa mwaka 2022/2023 jumla ya miche 8,784,146 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Kati ya kiasi hicho, miche 5,458,123 ni aina ya arabika na miche 3,326,023 ni aina ya robusta. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Serikali imepanga kuanzisha mashamba 40 ya mfano katika wilaya 20, kuratibu uzalishaji na usambazaji wa miche bora 20,000,000 katika wilaya 52 na kufufua mashamba 150 yenye jumla ya hekta 400.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mkakati wa Serikali unaonekana hawajafanya utafiti wa kuweza kujua ni kwa kiasi gani uzalishaji wa mbegu unahitajika nchini: -

Je, Serikali ipo tayari sasa kutengeneza mkakati, angalau wa miaka mitano, wa kuhakikisha kwamba wanafanya utafiti wa kujua ni idadi kiasi gani ya mbegu zinatakiwa ili uzalishaji huo wa miche milioni 20 kwa mwaka angalau upande hadi kufikia miche milioni 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa *TaCRI* na Bodi ya Kahawa peke yao hili zoezi hawaliwezi: -

Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuhakikisha kwamba inaihusisha sekta binafsi katika eneo hili la uzalishaji wa mbegu ili sasa hili zao la kahawa tuweze kulifufua kote nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti kwenye kahawa ndiyo kazi ambayo imekuwa ikifanyika muda wote kupitia *TaCRI* ili kuwezesha kuongeza uzalishaji katika zao letu la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa miche ya kahawa unaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na mahitaji. Kwa hivi sasa tumetoa maelekezo kwa wenzetu wa *TaCRI* pamoja na wakulima pia kuhakikisha ya kwamba tunang'oa ile mibuni yote iliyofikisha zaidi ya miaka 25 ambayo imezeeka na kupanda miche mipya ili kuongeza uzalishaji. Hivyo, itatulazimu kuongeza uzalishaji mkubwa sana wa miche ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sisi kama Serikali peke yetu hatuwezi kufanya, tumewahusisha pia sekta binafsi ili kwa pamoja tuweze kuzalisha miche mingi zaidi, na lengo hapa ni kuwa na miche mingi ya ziada ili wakulima wetu waweze kuipata kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumeongeza mkakati mwingine wa kuhakikisha kwamba tunatumia teknolojia ya chupa *(tissue culture)* kwa ajili ya kuongeza uzalishaji miche mingi zaidi ya kahawa, iwafikie wakulima kwa wakati, na tuweze kuongeza uzalishaji wa zao hili la kahawa hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde.

Tunakwenda Wizara ya Nishati, namwita Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 687

**Kupeleka nishati ya gesi vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kupeleka nishati ya gesi asilia katika vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro ili kupunguza matumizi ya kuni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia inaweza kusafirishwa kwa njia ya mabomba au kwa njia ya mitungi/tanki inayobebwa na malori/treni/meli ambapo gesi asilia inakuwa katika hali ya gesi iliyogandamizwa *(Compressed Natural Gas – CNG)* ama kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*. Hadi sasa, gesi asilia inachimbwa Mtwara na hivyo maeneo yaliyounganishwa na kuweza kutumia nishati ya gesi asilia ni yale yanayopitiwa na miundombinu ya mabomba ya kusafirishia gesi ambayo ni Mikoa wa Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kwenda Mombasa Nchini Kenya kupitia Mkoani Tanga, ni moja ya miradi inayotoa fursa ya kuunganisha Mikoa ya Kaskazini na gesi asilia ikiwemo Kilimanjaro kwa kuweka toleo katika eneo la Segera (Tanga). Mradi huu wa bomba bado unafanyiwa kazi Serikalini, utakapokamilika gesi asilia itaweza kufikishwa Mkoani Kilimanjaro, vikiwemo vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro na katika maeneo mengine mkoani humo na mikoa ya jirani, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niishukuru Serikali kwa majibu ya kutia moyo. Nina maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kaya nyingi kule Uchaggani na maeneo mengi ya Tanzania, kaya zote zina wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza kwenye gesi endelevu kwa mfano tupate nishati ya kupikia na kuwasha taa kutoka kwenye kinyesi cha wanyama ili kuzuia matumizi ya kuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kuhamasisha wananchi watumie majiko bunifu na mikaa ya tofali inayotokana na pumba za mpunga na masalia mengine ya mimea ili kupunguza matumizi ya kukata miti na kuwapatia wananchi nishati?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Prof. Ndakidemi, kwa ufuatiliaji wa eneo hili ambalo ni eneo jipya ambalo Serikali imetilia mkazo kuhakikisha kwamba tunatumia nishati safi, hasa ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali yote mawili kwa pamoja kwa kutoa maelezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka jana Mheshimiwa Rais alizindua mjadala wa Kitaifa wa nishati safi ya kupikia, na ni azma ya Serikali kupitia Wizara ya Nishati, mmeona tukijikimu kuelekea sasa kwenye nishati safi ya kupikia. Na katika eneo hili

tunahamasisha utumiaji wa gesi ya mitungu, lakini gesi asilia, lakini pia maeneo mengine waliyoyasema ya kutumia *biomass,* kwa maana vinyesi vya wanyama, na mikaa hii ambayo ni ya kutengeneza ambayo haitoi moshi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati kupitia *REA* inawezesha na ku-*facilitate* wale wagunduzi na watengenezaji wa majiko banifu na hii mikaa ya asili, kama mlivyotembelea mabanda yetu mliwakuta pale wabunifu wa namna hiyo. Kwenye Serikali itakuwa siyo rahisi sana kutumia nguvu ya Serikali kuzalisha umeme au gesi ya kupikia kwa pesa ya Serikali kutumia vinyesi vya wanyama na maeneo mengine. Kwa hiyo, Serikali inatoa pesa lakini pia tunapata mifuko mingine kama *Green Fund* ambayo ina-*facilitate* wananchi na wawekezaji binafsi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Prof. Ndakidemi kwamba tutaendelea kusimamia eneo hili kuhakikisha kwamba tunawawezesha wananchi na kuwapa fedha za mitaji ili waendelee kupata vitendea kazi vya maeneo hayo kuweza kuzalisha gesi asilia na kuweza kutumika katika kuwasha umeme, lakini pia katika nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gesi asilia ina gharama ndogo sana kuliko ile gesi ya mitungi, na kwa kuwa Serikali imeshawekeza katika Mkoa wa Dar es Salaam, maeneo ya Mikocheni na Msasani: -

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuhakikisha gesi hiyo asilia inapelekwa katika wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo azma ya dhati kabisa, na katika bajeti ya mwaka huu imetenga pesa kwa ajili ya kuendelea kupanua miundombinu ya upelekaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uunganishaji wa gesi asilia kwa mteja mmoja nyumbani kwake kwa miundombinu tuliyokuwa nayo sisi ina-*range* kutoka milioni mbili mpaka sita kwa mteja mmoja. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kutafuta uwezeshaji wa kuweza kutambaza mabomba mengi zaidi katika maeneo yetu na kufikisha miundombinu hii ya gesi ili wananchi walio wengi zaidi waweze kupata nishati hii na kuitumia kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tumefungua milango kwa wawekezaji wengi zaidi ili waje washirikiane pamoja na Serikali kuweza kuendelea kusambaza gesi asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam. Lakini tunao mpango wa kuleta mpaka Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine ambayo wanaendelea kutumia na kuhitaji nishati ya gesi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa tisa iliyokabiliwa na ukame, Mkoa wa Simiyu ni mmoja wapo, je, Serikali ina mpango gani kupeleka gesi asilia?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, gesi asilia inaweza kupelekwa kwa njia ya mabomba au kwa kugandamizwa na kuwekwa kwenye magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tuko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi, lakini mipango iliyopo Serikalini ni kusogea sasa kuja katika Mikoa ya Bara kwa ndani zaidi kwa njia zote hizo, kwa maana ya kuwekeza katika kuleta kwa malori na treni au kuleta kwa bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Simiyu na maeneo ya Mkoa wa Mwanza ambapo kuna watumiaji wengi wanahitaji gesi kwenye viwanda, mipango ya Serikali ni kuendelea kupanua wigo wa upelekaji wa gesi katika maeneo hayo. Mkoa wa Simiyu nao pia utafikiwa pale ambapo uwezeshaji utakuwa umekamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wa vijijini wanatumia kuni na mkaa kwa sababu ndiyo nishati inayopatikana kwa wepesi kwenye maeneo yao: -

Serikali ina mkakati gani wa kupeleka nishati mbadala ambayo ni gesi asilia ili iendane na nguvu tunayotumia kupiga marufuku kutumia kuni na mkaa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba watu wengi wa vijijini wanatumia mkaa na kuni katika hasa nishati ya kupikia. Tunalifahamu hilo na

tumeliona na Serikali imeanza jitihada za kuanza kupunguza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia kwa namna ambayo imeonekana ni rahisi zaidi kuliko nishati ya gesi ya asili, ni kuwezesha wananchi kupata mitungi ya gesi ya viwandani kwa kuanza kupikia, na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha ilitengwa mitungu 70,000, tumetenga kwenye bajeti inayokuja mitungi takribani 200,000 ili angalau tutoe mtaji wa mwananchi kuweza kupata kianzio cha kupata gesi halafu baada ya hapo sasa ataanza kununua na kuelekea kwenye kutumia gesi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaboresha na kuona namna tunavyoweza kupunguza gharama za hii mitungi ya gesi ili wananchi walio wengi waweze kui-*afford* kwenye maeneo yao, Serikali inaweka ruzuku lakini tutaangalia namna nyingine ya kuweza kupunguza gharama hizi ili kila mwananchi aweze kutumia gesi safi ya kupikia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; muuliza swali wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero.

Na. 690

**Kuazisha Tawi la Chuo Kikuu Huria – Halmashauri ya Ifakara**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanzisha Tawi la Chuo Kikuu Huria katika Halmashauri ya Ifakara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina mkakati wa kuanzisha Tawi la Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania katika Halmashauri ya Ifakara. Aidha, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimefungua matawi yake katika Makao Makuu ya Mikoa yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Mkoa wa Morogoro ambapo wananchi wa Halmashauri ya Ifakara wanapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pia kina vituo vya mitihani kwenye ngazi ya wilaya kwa pale ambapo idadi ya wanachuo ni 50 na kuendelea. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na ninaishukuru Serikali kwa majibu hayo, lakini swali la kwanza; kwa kuwa Ifakara ni katikati ya Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, na mahitaji ya kuwepo kwa tawi ama kituo cha mitihani ni makubwa mno: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Tawi dogo la Chuo Kikuu Huria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; endapo halmashauri itatoa eneo kwa sasa: -

Je, Serikali iko tayari kujenga Tawi la Chuo Kikuu Huria ama tawi la chuo kikuu kingine chochote? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kujibu swali hilo, japo linafanana na jibu lako la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha jibu katika majibu ya swali la msingi, lakini Mheshimiwa Asenga anataka kufahamu, japo kuwa pale tuna Kituo cha Chuo Kikuu Huria ambacho wanafanyia mitihani bado ana msisitizo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Asenga; Chuo Kikuu Huria kinao utaratibu wa kuwa na vituo vya mitihani katika ngazi za wilaya pamoja na kata kulingana na uhitaji wa maeneo hayo. Lakini vilevile kina utaratibu wa kuweza kuanzisha matawi au vituo hivyo vya kuratibu mitihani katika makambi yetu ya majeshi pamoja na kambi mbalimbali za wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Asenga naomba tu nikuhakikishe kwamba Serikali itaendelea kufanya tathmini ya kina katika eneo hilo ulilolitaja la Kilombero, Ulanga na kule Malinyi na maeneo mengine nchini, na kuweza kuona kama uhitaji huo upo ili tuweze kuanzisha ama vituo au matawi ya Chuo Kikuu Huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili, kwanza tuishukuru Halmashauri ya Ifakara, lakini tukushukuru wewe binafsi kwa jitihada zako za kutenga eneo kwa ajili ya Chuo Kikuu Huria. Naomba nikuhakikishie kwamba Serikali itaendelea kufanya tathmini, pamoja na uwepo wa maeneo haya, lakini vilevile kuna uhitaji wa rasilimali fedha pamoja na uhitaji wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi vyote vikichanganywa ndipo tunakwenda kuanzisha matawi haya ya chuo kikuu, lakini vilevile uhitaji wa hilo tawi katika eneo hilo. Kwa hiyo, baada ya tathmini hii tutajihakikishia sasa kama upo umuhimu wa kwenda kuanzisha tawi katika eneo la Ifakara au la, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; ninamwita Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Lucy Sabu.

Na. 691

**Kudhibiti watoto chini ya miaka saba kusoma shule za bweni**

**MHE. LUCY J. SABU K.n.y. MHE. JUDITHI S. KAPINGA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti watoto chini ya miaka saba kusoma shule za bweni?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule uliotolewa mwezi Novemba, 2020. Mwongozo huo umeelekeza bayana kuwa kibali cha kutoa huduma ya kulaza wanafunzi wa bweni kitatolewa kuanzia darasa la tano na kuendelea. Aidha, huduma ya bweni itatolewa kwa kibali maalum kwa wanafunzi wanaosoma chini ya darasa la tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutolewa kwa mwongozo huo, pia, Serikali imetoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2023 unaowaelekeza wamiliki wa shule wasiokuwa na kibali maalum cha kutoa huduma ya bweni kwa wanafunzi waliochini ya darasa la tano wasiendelee kutoa huduma hiyo. Aidha, kwa kushirikiana na wadau wa elimu, Wizara inakamilisha kuandaa vigezo vitakavyotumiwa na Kamishna wa Elimu katika kutoa kibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kudhibiti tatizo la watoto chini ya darasa la tano kusoma shule za bweni kwa kuhakikisha kuwa inafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na shule itakayobainika kukiuka maelekezo hayo itachukuliwa hatua za kinidhamu, na kisheria ikiwemo kufutiwa usajili, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; je, ni vigezo vipi vinatumika kwa ajili ya kibali maalum kutolewa kwa shule za bweni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 2023 umetoa maelekezo wamiliki kuwa na kibali kwa ajili ya shule za bweni: -

Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa shule ambazo zimekiuka agizo hili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi, kwamba vipo vigezo ambavyo Kamishna wa Elimu anatumia, lakini hivi sasa tunahuisha vigezo hivyo. Na nimesema kuwa Wizara kwa kushirikiana na wadau inakamilisha kuandaa vigezo vitakavyotumiwa na Kamishna wa Elimu katika kutoa vibali hivi maalum. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea kufanya uhuishaji wa vigezo hivi na mara vitakapokuwa tayari basi Umma utajulishwa juu ya

vigezo hivi ili iweze kufwata wakati wa kuomba vibali hivyo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, anataka kujua hatua zipi zilizochukuliwa; naomba nimhakikihsie Mheshimiwa Mbunge wale wote ambao walikuwa wanaendesha shule hizi kinyume na utaratibu wameweza kupewa *notice*, lakini vilevile wadhibiti ubora wetu wameweza kutembelea maeneo hayo na kuweza kujiridhisha juu ya huduma ambazo zinatolewa hapo, na baada ya kuona hali ilivyo basi tutachukua hatua mara moja, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya utafiti kujua watoto wangapi waliopo Bwenini wanafanyiwa ukatili wa kijinsia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mheshimiwa Mbunge anaomba Serikali iweze kufanya utafiti, nimwondoe hofu Serikali iko tayari kuchukua ushauri wake tuweze kufanya utafiti wa kuweza kujua athari zinazotokea katika unyanyasaji wa watoto wetu katika maeneo aliyoyataja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omar Kipanga, ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango na namwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa Tarime Vijijini aulize swali lake.

Na. 692

**Uhitaji wa Kituo cha Forodha Itiryo – Bikonge – Tarime Vijijini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaweka Kituo kidogo cha Forodha katika Kata ya Itiryo – Bikonge Tarime Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2022/2023 – 2026/2027) wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na ofisi katika maeneo yote yaliyobainishwa kupitia utafiti wa mwaka 2021/2022 kuhusu mahitaji ya ofisi za *TRA* nchini. Mpango huo umejumuisha Mkoa wa Mara na utekelezaji umeanza katika ujenzi wa nyumba mbili za wafanyakazi na usanifu wa ujenzi wa Ofisi ya Forodha mpakani Kilongwe – Rorya. Aidha, usanifu wa ujenzi wa majengo ya nyumba za watumishi mpakani Sirari umekamilika na ujenzi utaanza mapema baada ya kumpata mzabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji katika vituo vingine vya Mkoa wa Mara utaanza kadri ya upatikanaji wa fedha, ikiwa ni pamoja na Kogaja, Borega, Kirumi na Itiryo – Bikonge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba alienda Bikonge na Nyamuhonda; wananchi wa Jimbo zima walienda kwake wakitaka kujua ni lini wataweka pale kituo kwa sababu kitasaidia kuokoa fedha za Serikali na kufanya biashara mpaka watu wa Serengeti watanufaika hapa. Kwa hiyo niliomba nijue ni lini kituo hicho kitajengwa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliahidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninapozungumza hapa Kanda ya Ziwa yote Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Geita, Mara biashara ya mazao imesimama kwa sababu Sirari kuna vurugu kubwa kwa zuio ambalo limetolewa na Mheshimiwa Waziri kwa Niaba ya Serikali. Watu wa Sirari na kanda ya ziwa wangependa kujua ni lini zuio hili litaondolewa kwa sababu wakati wanatoa tamko la kuzuia tayari wafanyabiashara wa mazao walikuwa na mazao kwenye maghala yao, hawafanyi biashara; na ulikuwa ukipeleka mazao Kenya unaleta bidhaa nyingine kutoka Kenya. Kanda imesimama biashara haifanyiki;

Je, ni nini kauli ya Serikali katika jambo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimpongeze sana kwa namna anavyofatilia kituo hiki kidogo cha forodha pale mpakani. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hiki mara tu upatikanaji wa fedha utakapopatikana basi kituo hiki kitajengwa, asiwe na hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili naomba tulipokee kwa sababu limechanganya Wizara tofauti, Wizara ya Kilimo,

Biashara na Fedha. Naomba tulipokee tukakae kama kamati tutakutana na wewe Mheshimiwa Mbunge tuone namna gani tutatatua changomoto.

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe naona amesimama.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa majibu ya ziada katika swali alilouliza Mheshimiwa Waitara. Mimi na yeye tumeshaongea zaidi ya mara moja mara mbili, naomba nirejee na Watanzania wanielewe. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijazuia watu kufanya biashara ya mazao na kuuza mazao nje ya nchi. Serikali ilichokizuia ni watu kufanya biashara bila kufuata utaratibu wa Kisheria. Haiwezekani mtu unanunua mahindi Songea unapakia kwenye malori huna *business license* ya aina yoyote, hata *business name* kusajili ambayo ni huduma inayotolewa. Huna *tin number*, huna *tax clearance*, huna *export permit*, huna *phytosanitary* halafu unataka nchi ikuruhusu kwenda kuuza nje mazao hayo. Malipo hayaonekani katika mfumo rasmi wa fedha, hatuzipati data katika *export statement* zetu za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Rais yako wazi, Mtanzania yeyote anayetaka kufanya biashara ya mazao kwa ajili ya kuuza nje ama kuuza ndani ya nchi akate leseni ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipitie kwenye Bunge lako Tukufu kuwaambia wafanyabiashara wa mazao, nendeni kwenye halmashauri kateni leseni za biashara, nendeni *TRA* chukueni *Tin Certificate* ili muingie kwenye mfumo rasmi na *formalization* ya biashara ya mazao ya kilimo. Hatuwezi kuendelea katika mfumo huu unao endelea. Na nia ya Serikali ni kurasimisha shughuli za kilimo na shughuli za biashara za mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana mtu yupo tayari apigwe *penalty* ya shilingi laki nane au milioni moja kwa sababu hana leseni avuke upande wa pili. Wiki iliyopita tumeruhusu malori Sirari, wiki hii tumeruhusu zaidi ya malori 506 na wote wamelipa faini ya shilingi milioni moja. Hatuwezi kuruhusu mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wafabnyabiashara mazao ya kilimo yatauzwa popote, nendeni mkajirasimishe mwe na *business license*, mwe mna *Tin,* mna *Tax clearance*. *This is how we formalize economy*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha forodha Oloika katika kata ya Ololosokwan Wilayani Ngorongoro ili kupunguza usumbufu kwa wananchi lakini kuongeza mapato ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Serikali kupitia *TRA* walifanya utafiti nchi nzima. Kwa hiyo upatikanaji wa fedha katika nchi yetu basi kituo alichokitaja Mheshimiwa Mbunge kitajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Engineer Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kulikuwa na ujenzi wa vituo vikubwa vitatu vya forodha, kipindi inajengwa Vigaza kulikuwa na cha Manyoni halikadharika kulikuwa na Kituo cha Nyakanazi Biharamulo ambacho kilikuwa kimeshaanza kujengwa na tayari majengo yako pale, lakini kimetelekezwa kile kituo na kiko chini ya Wizara ya Fedha.

Sasa nilitaka kujua ni lini ujenzi wa Kituo cha forodha Nyakanazi Biharamulo ambacho kilishaanza ujenzi utafufuliwa ili uweze kukamilika kwa manufaa ya Biharamulo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezra kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki kilikuwa na mgogoro kati ya Mkandarasi na upande mwingine lakini tumechukua hatua na ninacho mhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hivi karibuni tutapata mwafaka wa jambo hilo na kituo hicho kitaendelea na ujenzi kama kilivyopangwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Schwale swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SCHWALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka 2021 Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alifanya ziara kwenye Jimbo la Momba kumwonesha mahali ambapo tunapendekeza kujenga kituo cha forodha. Mwaka huu mwezi wa pili Mheshimiwa Waziri Mkuu pia tulimshirikisha wazo hilo na akaona ni jema;

Je, Serikali imefikia hatua gani kujenga kituo kipya cha forodha ndani ya Jimbo la Momba ili kunusuru kituo cha forodha kilichopo Tunduma kwa sababu kimezidiwa ili kiweze kutoa huduma kwa ufasaha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRII WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hicho ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha alienda lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda. Tuna mpango wa kujenga kituo hicho. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subra mara tu fedha zitakapopatikana tutajenga kituo hicho.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale aulize swali lake.

Na. 693

**Kufanya mapitio ya Sheria ya Manunuzi ya Umma**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kufanya mapitio sheria ya Manunuzi ya umma kwa kuwa ni kikwazo kwa utekelezaji wa miradi katika Halmashauri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imefanya mapitio ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na kuandaa mapendekezo ya kutunga upya sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo hayo yamekamilika na muswada wa kutunga upya sheria ya ununuzi wa umma unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nishukuru Wizara kwa majibu mazuri yanayotia matumaini. Jambo hili linaenda kutatua tatizo kubwa la ununuzi, na hasa katika taasisi zetu za umma ambazo zinaingia kwenye ushindani ambazo zinashindwa kufanya manunuzi kwa sababu ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa miradi mingi kwenye halmsahuri zetu sasa hivi inatekelezwa kwa *force account* na watu wanaoingia kwenye manunuzi ni watu ambao hawana taalum; Je, Serikali iko tayari kutoa mwongozo mahsusi ili kuongoza kuona namna gani hayo manunuzi yanayokwenda kufanya kusiwe na mgongano ambao sasa hivi nani ambaye anatakiwa kujibu maswali hayo ya ununuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ili kupunguza safari nyingi za maafisa ununuzi kwenda na kurudi kwa ajili ya kwenda kufanya manunuzi, Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza yale masurufi *(imprest)* kutoka milioni tatu ili kufika milioni kumi, kwa sababu sasa hivi hakuna bidhaa inayoweza kununuliwa kwa shilingi milioni tatu? Kwa hiyo matokeo yake wale maafisa manunuzi wanakwenda na kurudi zaidi ya mara tatu kwa bidhaa moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Kuchauka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ridhaa yako nijibu maswali yote mawili kwa pamoja. Taratibu, mwongozo na kanuni zinatolewa mara baada ya kutunga Sheria hiyo katika Bunge lako Tukufu. Hii ndiyo nafasi adhimu baada ya Muswada kuja Bungeni ya Wabunge kutushauri na kutuelekeza. Serikali yao ni sikivu sana tutaendelea kupokea ushauri huo na kuufanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Manunuzi ya Umma inaelekeza asilimia 30 kwenda kwenye makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu lakini Sheria hii inaonekana kuto tekelezeka.

Je, ni lini Serikali itatilia mkazo Sheria hii ili iweze kuleta tija kwa jamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njau kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ipo na inatekelezwa. Tuna toa maelekezo kwa maafisa masuhuli wote ambao hawajatekeleza hili watuletee ripoti na tuwaambie kabisa watekeleze sheria hii kama ilivyowekwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika manunuzi ya Serikali kumekuwepo na utamaduni wa kuongeza bei bidhaa zinazonunuliwa na Serikali ukilinganisha na bei halisi iliyoko sokoni.

Je, Sheria hii mpya inayofanyiwa marekebisho itagusa eneo hili kuhakikisha Serikali inanunua kulingana na bei ya soko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge katika hili. Itakapopita Sheria hiyo basi zitafuatwa taratibu zote za manunuzi katika bei halisi ambayo ipo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa miradi mingi ya Halmashauri inasimamiwa na walimu wakuu, waganga pamoja na walimu wakuu shule za msingi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa semina hao walimu wakuu baada ya sheria hiyo mpya kupitishwa upya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpakate kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali taratibu, kanuni na miongozo itatoka mara tu baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria hii. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subra itakapopita Sheria hii basi hayo yote anayoyatarajia yatapatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa majibu.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Hapa ninayo matangazo machache. Tangazo la kwanza…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Hapa ninayo matangazo mawili; tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu Wabunge anasema naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kufuatia Tangazo la Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kwamba Sikukuu ya *Eid Al-Ad* itafanyika tarehe 29 Juni, 2023 badala ya tarehe 28 Juni kama tulivyotazamiwa. Kamati ya Uongozi ilikutana jana tarehe 20 Juni, 2023 na kuzingatia mabadiliko ya ratiba ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea.

Katika Kikao hicho Kamati ya Uongozi iliridhia mabadiliko ya ratiba ya Mkutano na kwamba Bajeti ya Serikali sasa itapigiwa kura tarehe 26 Juni, 2023 na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge utahitimishwa tarehe 28 Juni, badala ya tarehe 30 Juni. Ratiba ya Mkutano yenye mabadiliko hayo imewekwa kwenye vishkwambi

vya Wabunge na katika tovuti ya Bunge. Hivyo kila Mbunge awepo siku ya Jumatatu tarehe 26 Juni, 2023 hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa tangazo la kwanza angalieni kwenye vishkwambi vyetu mtaikuta ratiba hiyo kila mmoja ataweza kuona.

Tangazo la pili ni la wageni; wageni waliopo kwenye Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika kutoka *ABSA Bank Tanzania Limited* ambao ni kama wafuatao; wa kwanza ni Ndugu Obedi Laiser ambaye ni *Managing Director/CEO,* wa pili ni Ndugu Bernard Tesha ambaye ni *Chief Finance Officer,* mwingine ni Ndugu John Mosha ambaye ni *Chief of Staff,* mwingine ni Ndugu Innocent Wamcha ambaye ni *Dodoma Branch Manager,* Ndugu Nellyana Mmanyi ambaye ni *Head of Corporate Coverage* na Ndugu Ally Zingizi ambaye ni *Media Official,* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni Ndugu Mohamed Kawaida ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Taifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nirudie maana walikuwa hawajasikia vizuri wenzetu wa huku; ni Ndugu Mohamed Kawaida ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa UVCCM Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM. *(Makofi)*

Haya ahsante, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ameambatana na Kada wa CCM Ndugu Daudi Laizer, karibu sana, karibu sana Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Tawala nchini Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni sita wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wakiongozwa na Mwandishi wa Vitabu Ndugu Sandra Lema**.** *(Makofi)*

Sandra Lema yuko wapi, mgeni wa Mheshimiwa, ndio kiongozi wao, nafikiri mmemwona pale, wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Geophrey Pinda ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni watoto wake kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Daniel Sillo kutoka Babati Vijijini, Mkoa wa Manyara, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma, tunashukuru. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Catherine Magige kutoka nchini Marekani, ahsante. *(Makofi)*

Wapo wageni 59 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni viongozi UWT wa Kata, Wilaya na Madiwani kutoka Simanjiro, Mkoa wa Manyara, nafikiri mnamuona, karibuni sana, mnamuona Mheshimiwa Qwaray yupo anachapa kazi hapa ya kuwawakilisha. *(Makofi)*

Lakini pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka Mkoa wa Morogoro karibu sana mgeni wa Mheshimiwa Shangazi. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Manyara, ahsante. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Francis Mtega ambao ni viongozi wa CCM na Madiwani kutoka Mbarali, Mkoa wa Mbeya. Madiwani kutoka Mbarali, Mkoa wa Mbeya, haya karibuni sana Dodoma Waheshimiwa Madiwani wetu kutoka Mbarali. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Taasisi ya Chawa wa Mama kutoka Igunga, Mkoa wa Tabora, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Aysharose Mattembe ambao ni kikundi cha waimbaji wa *TAG Jerusalem Spiritual Centre* kutoka Singida Mjini, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni familia yake na Umoja wa Walimu Wakuu kutoka Tarime Mjini Mkoa wa Mara wakiongozwa na Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Tarime. Siwaoni, pengine wataingia baadaye. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wake Ndugu Lucy Thomas Malongo. Mke wa Mheshimiwa Waitara punga mkono, nafikiri mnamwona pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Juma Usonge Hamad kutoka Taasisi inayojishughulisha na Elimisha Rika kwa Watoto wa Kike na Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi ya Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke kutoka Kasulu, Mkoa wa Kigoma, ahsante. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni viongozi wa Chama cha Wafanyakazi *(TUGHE),* Tawi la Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi *(MUWASA),* ahsante. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Maryam Omar Said ambao ni familia yake na wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo yako makundi mawili; kundi la kwanza ni wanafunzi 138 kutoka Shule ya Msingi *Royal Elite* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana wanafunzi na walimu wao wapunge mikono,. *(Makofi)*

Kundi la pili, ni wanafunzi 42 na wafanyakazi nane kutoka Shule ya *Rahma Pre and Primary School* ya Jijini Dodoma, karibuni

sana wanafunzi, lakini pia na walimu wao wanaowalea sijui wako wapi? Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI.**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2022 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na majadiliano. Watakaoanza kuchangia asubuhi ya leo ni pamoja na Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangoia Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapochangia Bajeti ya Serikali, kwanza kabisa huwa tunafanya mapitio ya Bajeti. Vile vile, ukizingatia mwaka wa fedha uliopita tulipitisha Mradi maarufu sana kama Mradi wa *TACTIC* kwa ajili ya kujenga miradi mbalimbali kwenye miji 12 ambapo Jiji la Arusha ni mji mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana kwamba tutaanza kujenga Stendi ya Kisasa, eneo la *Bondeni City* kuanzia Mwezi wa Saba wa mwaka uliopita. Umepita wa saba tumekwenda mpaka Desemba imepita leo tuko mwezi wa Sita tunakaribia kuumaliza, mpaka leo hata tenda haijatangazwa na bado tunazungumzia

bajeti ya mwaka unaofuata. Kwa hiyo, ningefurahi kuona majibu ya Serikali kuhusiana na mpango wa ujenzi wa Stendi ya Jiji la Arusha, kitu ambacho Wanaarusha wanakitamani sana kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kuishulkuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye mpango wa kujenga viwanja vya michezo vya Kimataifa kwenye Mikoa miwili, Mkoa wa Dodoma lakini pia na Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Arusha ni mahali sahihi kwa sababu hii ni sehemu ya kuunga mkono *Royal tour* lakini pia ni sehemu ya kuchangia kwenye masuala ya *Sports tourism.* Hii pia ni kazi nzuri ambayo imefanywa na wenzetu wa Wizara ya michezo kupitia Waziri wetu Dkt. Pindi Chana pamoja na Naibu Waziri, Katibu wetu Mkuu Ndugu yangu Yakubu ambao wanafanya kazi kwa ubunifu mkubwa na wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumepokea mpango huu katika hali nzuri zaidi na tumekwishatenga ardhi ya kutosha kwenye Kata ya Olmoti, Diwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Kata ya Olmoti wako tayari kabisa kwa ajili ya kuupokea mradi huu kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Arusha tuna hoteli nyingi, tuna mazingira mazuri zaidi, hali ya hewa nzuri na nimeambiwa viwanja hivi vitakwenda kujengwa pia maeneo ya *basketball,* riadha na hasa ukizingatia kwamba Arusha na hasa maeneo ya Karatu ndio wakimbiaji wengi zaidi wanapatikana katika nchi yetu. Kwa hiyo tunaunga mkono jambo hili na ni imani yangu kwamba *consultant* ambaye nimeambiwa kwamba atapatikana wakati wowote kuanzia mwezi wa Saba kwa maana ya mwaka wa fedha unaoanza mwezi wa Saba, basi kazi hiyo itakwenda kuanza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwenye mapitio upande wa madini, tunaishukuru sana Serikali kwa sababu imekubali kurudisha madini ya *tanzanite* kwenye masoko yote. Tumeambiwa

kwamba mpango huo utaanza kuanzia mwaka wa fedha unaokuja mwezi Julai na kuendelea. Vile vile, kuna mawazo hapa ya kuondoa kodi kwenye minada katika maeneo mbalimbali ambayo itafanyika, tunaunga mkono pia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo za awali, napenda nichangie kwenye masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, wakati Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya ziara Mkoa wa Kagera ilikuwa ni tarehe 9/6/2022, alitoa maelekezo kwa *TRA* kuhakikisha kwamba hawarudi tena kufukunyua masuala ya kodi zaidi ya mwaka mmoja. Tunaona hapa Waziri wa Fedha amekuja na mapendekezo kwenye *Finance Bill,* lakini suala hili hajalileta kuliingiza kwenye mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba, ili kumlindia heshima Rais wetu na ili kuendelea kuyatunza maelezo ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa kwenye hadhara, ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha akatuletea hapa kwenye *Finance Bill* maelekezo haya yakaingia kwenye Sheria ili *TRA* wasiingie kwenye mtihani wa kuacha kusimamia sheria. Kama ni vizuri zaidi wakaweka utaratibu mzuri zaidi wa kuhakikisha kwamba wanaingiza kwenye sheria hasa kwenye Muswada wa Fedha wa mwaka huu na Wabunge tutawaunga mkono, kwa sababu ni lazima tumuunge mkono Rais wetu anapoonekana kuwajali wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nimefurahi sana kuona Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba maeneo ya biashara yasifungwe. Nadhani tamko hilo lingeenda mbali zaidi, sio tu maeneo ya wafanyabiashara, lakini pia wanapoacha kufunga biashara wasifunge pia akaunti za wafanyabiashara. Wanapoacha pia kufunga akaunti za wafanyabiashara, waache pia kwenda kuchukua *computer* za watu, kuchukua simu za watu kwa wafanyabiashara wa maeneo mbalimbali. Watafute mbinu za kisasa za kuweza kukadiria kodi, kukusanya kodi lakini sio kwenda kuwavamia wafanyabiashara kuchukua vifaa vyao kwa kutumia kigezo cha *investigation.* Kwa hiyo, nadhani hilo nalo

Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kulipa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tumeona pia hapa yamekuja mapendekezo ya kuongeza shilingi 100 kwenye mafuta ya *petrol* na *diesel.* Hili wazo mimi binafsi sikubaliani nalo, kwa sababu kwanza ukiangalia kwenye mafuta peke yake kuna kodi kama 22. Kuna kodi ya *Wharfage, Railway Development levy 1.5 percent ya CIF, Custom Association Fees, Weight and Measure, TBS, TASAC, EWURA,* wako wengi na ziko kodi 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye hizo kodi 22 bado kuna kodi kiasi cha shilingi 413 tunaita *fuel levy.* Hii 413 tayari kodi ya barabara imo humu ndani. Ukiangalia kuna 186 kwa ajili ya *TANROADS,* kuna shilingi 177 kwa ajili ya *TARURA,* kuna shilingi 50 kwa ajili ya maji. Kwa hiyo, unaona kabisa barabara zimezingatiwa *TANROADS, TARURA* wamo humu na maji pia yamo. Kuongeza shilingi 100 nyingine ni kuongeza mzigo kwa mwananchi na kumwongezea mzigo Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi, unapoongeza shilingi 100 mfanyabiashara hana shida, yeye anaongeza ule mzigo, halafu anampelekea mwananchi. Daladala zitataka kupanda bei, mabasi yatapandisha bei na gharama nyingine zitaongezeka kwa sababu itakuwa inagusa pia uzalishaji. Ushauri wangu ni kwamba, tutafute eneo lingine, lakini eneo hili ambalo linakwenda kumgusa moja kwa moja mwananchi kama Serikali tuliangalie vizuri zaidi na hasa ukizingatia tuna changamoto kwenye dola yetu, haijawa *stable* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka 2018 dola moja ilikuwa ni sawa na Sh.2,276 kwa wastani, leo dola moja ni sawa na Sh.2,398, maana yake ni nini? Mafuta duniani yanauzwa kwa dola na kama yanauzwa kwa dola yanapokuja Tanzania tukiweka kwa shilingi, *peak* yake kuna ongezeko la Sh.122. Unaona kabisa mzigo wote huu unaokuja anaubeba Mtanzania. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha zaidi akaongeza ubunifu zaidi kwenye vyanzo lakini sio vile ambavyo vinakwenda kumuumiza mwananchi na Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sambamba pia na kwenye upande wa kupanda kwa bei ya saruji na yenyewe ni vile vile. Tunataka Watanzania wawe na maisha mazuri, tunataka tuondoe nyumba za tembe, lakini mwisho wa siku gharama za ujenzi unaziongeza. Ukiongeza gharama ya *cement* maana yake umeongeza gharama ya ujenzi na umemnyima uwezo Mtanzania wa kuweza kununua *cement* nyingi zaidi ili aweze kujenga nyumba nzuri zaidi. Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwamba na hili lenyewe kwa sababu linamgusa mwananchi moja kwa moja, Serikali ikalitafakari na itafute ubunifu mwingine kwenye upande wa kodi lakini siyo huu ambao unakwenda moja kwa moja kwa mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kumekuwa na changamoto nyingi sana, Wakandarasi wetu, wazabuni wetu hawalipwi kwa wakati. Leo ukifanya kazi ya Serikali, ukichelewa kumaliza mradi Serikali wanakupiga *penalty,* lakini Serikali inapompa kazi mzabuni au mkandarasi, ikichelewa kumlipa yenyewe haipigwi *penalty.* Nafikiri ni vizuri tuweke utaratibu hapa ikiwezekana Serikali pia inapochelewa kumlipa mkandarasi au mzabuni na yenyewe pia iweze kupigwa *penalty.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mbaya zaidi kwa sababu watu wetu hawa wanakopa fedha benki na kule kwenye benki wanapewa riba. Kwa hiyo, kadri wanavyochelewa kulipwa na wao wanachelewa kufanya marejesho, mwisho wa siku wanapata hasara kubwa zaidi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atoe tamko kwenye halmashauri zetu, lakini pia na kwenye taasisi zote za umma ambazo zina madeni walipe madeni kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alishasema jambo hili "Mtu yeyote asitangaze tenda kama hana fedha za kulipa", lakini huko hali ni mbaya. Nenda karibu kila mahali, halmashauri hazilipi, taasisi za umma hazilipi, kuna madeni kila mahali. Tunaomba hili jambo Mheshimiwa Waziri aliweke vizuri kwa sababu tunajua yeye ni Mchumi mbobezi na tunajua kwenye masuala ya uchumi lazima pia uangalie *circulation* ya watu wako wale ambao wanafanya shughuli mbalimbali za biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye upande wa gharama za bando. Bahati nzuri nimesoma *computer science undergraduate* lakini hata *degree* yangu ya pili nilisoma masuala ya *computer.* Katika kitu ambacho tunatakiwa tukiangalie vizuri ni gharama za bando, zimepanda s*ana.* Majibu tunayopewa hayaendani na hali halisi. Unaambiwa sijui zima *App* hii, unaambiwa fanya hivi, hicho ni kitu kimoja kitakupunguzia matumizi, lakini hapa tunachokisema ukiangalia *data* zetu sisi kwa wastani, kwa mfano mwaka 2020, ulikuwa ukinunua *data* za 15,000 kwa wiki, ulikuwa unapata wastani wa *GB* 10. Leo 15,000 hiyo hiyo kwa upande wa *Vodacom* unapata *GB* 7.38, ukienda Tigo unapata *GB* 7.2, ukienda *Airtel* unapata *GB* 7.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unaona kabisa imetoka kwenye 10, hawajaongeza bei lakini wamepunguza bando, kwa maana nyingine pia wameongeza bei. Kwa maana ya kwamba ukiangalia kipindi hicho *GB* moja ilikuwa ni wastani wa shilingi 1500 ambapo *GB* 10 ilikuwa ni shilingi 15,000. Leo hii *GB* moja kwa upande wa *Vodacom* peke yao unapata kwa shilingi 2,054 kwa hiyo hapa wameongeza shilingi 554. Ukienda *Airtel* wameongeza shilingi 583, ukienda Tigo wameongeza shilingi 583. Kwa hiyo, gharama za bando zimeongezeka na ndio maana watoto wetu wakipewa *assignment* kule mashuleni ukimwekea *bundle* la 5,000 akitumia kidogo tu limekwisha. Kwa hiyo, linaongeza gharama za maisha, inaongeza gharama za shule na inapunguza pia ubunifu wa watu wetu kuendelea kudadisi masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri na nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Nape Nauye, ni vizuri ili suala wakaliangalie vizuri. Nafahamu uzalendo wa Mheshimiwa Waziri, ni vizuri wakakae na wenzetu wa *TCRA,* mitandao ya simu waangalie namna ya ku–*review data* hizi na tusiambiwe kwamba mbona kule duniani gharama ni ndogo. Dunia ni dunia na Tanzania ni Tanzania, tuizungumzie Tanzania yetu ambayo ni bora na ya kipekee, haifanani na nchi nyingine yoyote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nadhani niliseme ni kwenye upande wa kodi ya majengo. Nimeona hapa

Mheshimiwa Waziri amekuja na mapendekezo anataka kodi ya majengo turudi tulikotoka. Maana zamani ulikuwa unafanyiwa uthamini inajulikana *value* ya jengo halafu unalipa. Gharama zilikuwa ni kubwa, rushwa zilikuwa nyingi, Mthamini akija pale jengo la bilioni mbili ukiongea naye vizuri anakwambia milioni 800. Kwa hiyo wanaweka mianya ya rushwa. Baadaye Serikali hii hii ikaja na utaratibu kwamba, badala ya kwenda kwenye masuala ya uthamini, basi tuweke utaratibu wa kuangalia kama ni nyumba ya chini walisema shilingi 10,000. Kama ni ghorofa kila *floor* walisema ni shilingi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wameona hizo fedha ni ndogo ni bora wakae chini waangalie badala ya shilingi 10,000 iwe angalau ni Sh.15,000 na badala ya shilingi 50,000 kwa kila *floor* ya ghorofa basi angalau iwe shilingi 80,0000 au shilingi 100,000, lakini wakianza masuala ya *evaluation,* maana wametuambia kwenye maelezo yao wataanza 2026. Sisi tunafahamu hii Serikali, leo wameanza wamechokoza kidogo, ukienda mbele unasema kuanzia Januari utekelezaji utaanza. Kwa hiyo unakuwa na *statement* ambazo mwisho wa siku unashindwa kujua uisimamie ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, badala ya kuja na mambo ya uthamini, kwanza yatawapa gharama kubwa, wataalam walio nao ni wachache na wataongeza pia mianya ya rushwa. Tutafute namna nyingine kama wanaona hiki ni chanzo kizuri cha mapato, basi tuongeze pale kidogo, lakini tusiende kwenye uthamini kwa sababu watawakatisha Watanzania kujenga nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ana nyumba yake ya ghorofa 10 anamkopo wa kulipa miaka 30 au 40 halafu mkopo hajamaliza, bado Serikali inakuja kumwambia kwamba pengine tumefanya uthamini na kodi ya majengo utalipa asilimia fulani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa sababu namfahamu kuwa ni mchumi mbobezi, daktari na amefanya kazi pia *BOT,* ni mtu ambaye ana uzoefu wa kutosha pamoja na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu watakwenda kuliangalia, kwa sababu hili wameleta kama pendekezo sio sheria wala sio taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili kwa ushauri wangu ni kwamba ni pendekezo ambalo linahitaji kuangaliwa kwa kina…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, muda wako umekwisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliahidi kuniongeza dakika mbili sijui bado zipo au umeghairi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, muda wako umekwisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal, wakati huo Mheshimiwa Stansalaus Nyongo anajiandaa.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenipa nafasi ili nichangie hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema niweze kusimama kwenye Bunge hili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri aliyowasilisha hapa Bungeni, imeleta matumaini kwa Watanzania na ina mambo mengi. Kabla sijaanza kuchangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka ujao, ninaomba nichangie bajeti ambayo inaelekea kuisha tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa kwa bajeti hii ambayo inaendelea sasa hivi. Pamoja na misukosuko ya kiuchumi ya kidunia ameweza kufanya kazi nzuri na miradi yote ya kimkakati imeweza kupata fedha. Ukienda kwenye Mradi wa Bwawa la Nyerere kazi inaendelea, ukifika kwenye Reli ya Kati kazi inaendelea, ukifika Daraja la Magufuli kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni machache nimeona niyaseme kwamba, kazi nzuri wanafanya pamoja na misukosuko ya kiuchumi pia kuna masuala ya kulipa mishahara kwa watumishi hawajakopa, tukiangalia nchi zingine jirani wanakopa mishahara ya watumishi lakini Serikali yetu haijakopa inalipa mshahara ndani ya wakati, nawapongeza sana. Pia fedha za elimu bila malipo kila mwezi wanapeleka fedha bila kuchelewa, hiyo nayo inasaidia watoto wetu wapate elimu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya Kitaifa pia Jimbo la Kwimba tumekuwa na miradi mingi sana imetekelezwa nitaomba niseme machache. Kwanza ni kwenye suala la afya, kwenye masuala ya afya sisi tumepata Hospitali ya Wilaya mpya imejengwa sasa hivi inatoa huduma, tumejengewa vituo vya afya viwili ambavyo vyote vinaelekea kuisha mwezi huu, tumepata zahanati nne zimekamilika, tukienda kwenye elimu madarasa yamejengwa sasa hivi watoto wakiingia shuleni hawakai chini kuna madarasa kuna madawati ya kutosha, tuna Chuo cha *VETA* kimekamilika kinaanza kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye masuala ya maji kuna mradi wa Hungumalwa ambao unaelekea kuisha kukamilika mwezi wa Desemba mwaka huu, tukienda kwenye maji tena tuna mradi wa Nyamilama nao unaelekea kukamilika ndani ya mwezi wa Desemba, tuna mradi wa Jojilo Maleve imekamilika maji yanatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme taarifa ya maji ni kwamba Jimbo la Kwimba tuna Kata 15 kwa sasa hivi miradi hii ikikamilika tutakuwa tumeshapata maji ya Ziwa Victoria, maji safi na salama kwenye Kata 14. Mwakani kuna mradi wa maji wa kupeleka Malampaka - Malya itapeleka kwenye Kata moja inaitwa

Mwankulwe. Maana yake Jimbo la Kwimba hadi kufika mwakani tutakuwa tuna maji salama safi Kata zote. Ahsante sana Serikali kwa kazi nzuri ambayo mnatufanyia wananchi wa Jimbo la Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekeze kutoa mchango wangu kwenye bajeti ijayo, nianze na suala la Kilimo. Mheshimiwa Waziri kama unavyofahamu Jimbo la Kwimba ni Jimbo la Wakulima na Wafugaji. Sisi wananchi wa Jimbo la Kwimba wote ni wakulima, tuna zao la Pamba limekuwa na changamoto mwaka jana, wakati wa msimu mbegu zilichelewa kupatikana, mbolea yule mzabuni aliyechaguliwa na Serikali hakuonekana kabisa kwenye Wilaya yetu, ilibidi tuende Halmashauri, ilibidi ikodoshwe gari kwenda kuchukua mbegu, kuchukua mbolea Mwanza Mjini, tumepata shida sana kwenye mbolea haikufika dani ya muda, wakulima pia ilibidi waende kufuata mbolea Mjini. Kwa hiyo, mimi naomba mwaka huu Serikali itusaidie angalau mbegu na mbolea zifike ndani ya wakati ili wananchi wa Kwimba weweze kulima vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kama Mheshimiwa Waziri umependekeza kwenye hotuba yako kwamba unataka kupunguza ushuru wa forodha, unataka kufanya asilimia 35 ifike asilimia 10 na kwenye mafuta ya kula unataka kufanya kutoka asilimia 35 ifike asilimia 25. Mheshimiwa Waziri kwa kweli mimi sikubaliani na hiyo hoja, ningeomba hilo suala ungeliacha kama lilivyo kwa sababu inaenda tofauti kabisa na malengo ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ilikuja na bajeti yao wanasema mambo mengine ya kuboresha na sisi hapa tunakinzana. Mimi ningeshauri hili suala uliache kama lilivyo pia usaidie wale wanaotaka kuagiza mafuta ya kula na ngano wanunue kwanza mafuta yaliyoko ndani ya nchi na pia ngano wanunue ambayo iko ndani ya nchi inazalishwa ndiyo wapate kibali cha kuagiza nje. Wasipate kibali cha kuagiza bila kuwa na mchango wa kununua mazao yanayozalishwa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kusema ni kwenye suala la umeme. Suala la umeme napongeza sana Serikali kwamba bajeti ya mwaka kesho tutakuwa tumepeleka umeme vijiji vyote, sasa tunaanza kupeleka umeme kwenye vitongoji. Nawapongeza sana Serikali kwa maamuzi haya, lakini tatizo tulilonalo ni kwamba wananchi wetu wana uwezo wa kulipa umeme? Mimi ningeshauri na kupendekeza kwa Serikali kwamba waangalie gharama za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwamba hzi gharama za umeme zilipokuwa zimepangwa na *EWURA* ilikuwa wakati ule tulikuwa tuna jenereta za *Diesel* kama mfano Kigoma ilikuwa inatumia majenereta ya *diesel,* kwa hiyo gharama ya uzalishaji ya umeme ilikuwa juu. Sasa hivi tunazalisha umeme kwa kutumia gesi na mabwawa kwa hiyo bei imeshuka mimi ningependa sana Serikali iangalie tunawapelekea wananchi umeme lakini wana uwezo wa kulipa umeme? Nashauri tupunguze bei ya umeme ili wananchi kwenye vitongoji waweze kuunganishwa na umeme, tusije tukafikisha nguzo lakini haziendi kwenye nyumba kwa sababu hakuna uwezo. Kwa hiyo, lazima tuandae uwezo wa wananchi kupata umeme na kutumia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ningependa kulisemea ni la barabara. Siku chache zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa tamko hapa Bungeni wakati wa Wizara ya Ujenzi. Tunayo barabara yetu ya Hungumalwa - Ngudu kuelekea Magu tunataka ijengwe kwa lami. Miaka mingi tumeomba hiyo barabara tukaambiwa na Waziri wa Fedha kwamba kuna fedha za *African Development Bank* anazifuatilia, akizipata hiyo Barabara ya Hungumalwa-Ngudu kueleka Magu ataitangaza. Bajeti yake ambayo amewasilisha Mheshimiwa Waziri tumeona hiyo kwamba fedha za *African Development Bank* zipo zimekuja. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati unafanya *wind up* ya hotuba yako, tuambie lini unatangaza barabara yetu ya Hungumalwa inajengwa kwa lami, lini unatangaza, hilo tamko lako tunalisubiri siku una-*wind up* hotuba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwamba Wilaya ya Kwimba Mkoa wa Mwanza tumebaki peke yetu hatuna barabara inayotuunganisha kwenye Mkoa kwa lami. Tunayo barabara ya

kutoka Ngudu kwenda Jojilo kwenda Mabuki iko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kujengwa kwa lami. Tunaomba hiyo barabara pia ifanyiwe utaratibu wa kujengwa kwa sababu Wilaya haiwezi kuwa haina barabara ya lami kwenda kwenye Mkoa. Wilaya zote zinaunganishwa na lami lakini Wilaya ya Kwimba imebaki peke yake tunaomba angalau na hilo pia walifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kimkoa, Mkoa wa Mwanza tumekuwa na kero ya jengo la abiria kwenye uwanja wa ndege, miaka mingi tumekuwa na kero, tumekuwa tukisemea. Kuna jengo la abiria limejengwa limekuwa na mapungufu, hilo jengo wameshakabidhiwa *Tanzania Airport Authority* kwamba waliboreshe, wakamilishe. Tunaomba sana uwanja wetu wa ndege uboreshwe na hilo jengo likamilike. Tunaomba Serikali ituambie lini *TAA* watakamilisha hilo jengo ili liweze kutoa huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza na wageni wetu wanaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu Airport ya Mwanza ndio sura ya Mwanza. Mgeni anapokuja anakutana na ile jengo ambalo limekaa pale halikamiliki, limekaa kaa tu pale, tunaomba hilo jengo nalo lipate kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mchango wangu, nakushukuru sana kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunashukuru sana Mheshimiwa Shanif Mansoor Jamal. Nilimuita Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, wakati huo Mheshimiwa Grace Victor Tendega, anajiandaa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi leo niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Watanzania, kwa kweli tumeona miradi mingi sana katika Majimbo yetu. Haijawahi kutokea kuona fedha

nyingi za miradi zinazokwenda katika Majimbo yetu na jinsi wananchi wanavyopokea miradi hiyo wanaipokea kwa furaha, wanaipokea kwa bashasha na naomba niseme tu kwamba mwaka 2025 Watanzania wengi watatoa pongezi hizo au watatoa ahsante kwa Mama kwa kumpa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze sana Serikali kwa kujali Jimbo langu la Maswa Mashariki, tumepata fedha nyngi katika miradi, tumejenga vituo vya afya tumejenga barabara tumejenga barabara za Mjini Maswa tumeweka hadi mataa barabarani na sasa hivi kuna miradi mingi inaendelea ambayo kwa kweli wananchi wa Maswa wanashukuru na wanapongeza na watakwenda kumpa kura Mama mwaka 2025 bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kupongeza Serikali juzi tumeshuhudia Serikali imeingia mikataba ya ujenzi wa barabara saba zenye jumla ya kilomita 2090 na zenye thamani ya zaidi ya trilioni 3.7. Mkataba huu tumesaini kwa mtindo ule wa *EPC+F (Engineering Procurement Construction and Financing)*. Huu mtindo ni mpya tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kuingia katika mtindo huu mpya wa ujenzi wa barabara tunaona kabisa sasa barabara zinakwenda kujengwa maeneo ambayo tulikuwa hatutegemei barabara hizo kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Ilani za Chama cha Mapinduzi mara nne au mara tano Ilani zimeandikwa zinasema kwamba barabara ya Karatu -Mbulu – Haydom – Meatu - Lalago, Maswa inakwenda kujengwa. Ilani zimepita tatu, Ilani hii inakwenda kutekelezwa kwa vitendo chini ya Mama Samia Suluhu Hassan, kazi kubwa kwa kweli Serikali imefanya, tunaomba mtindo huu kwa sababu ni mpya Serikali iusimamie kwa karibu, tuone ujenzi huu unafanyika kwa haraka na hata ndani ya mikataba hiyo kama kuna *interest* kutokana kuchelewesha kulipa au namna ile yoyote ambayo iliwahi kutokea katika ujenzi wa barabara tunavyojenga miaka ya nyuma, basi kuepusha hilo ni kwamba Serikali itekeleze wajibu wake kwa upande wake na wale wajenzi watekeleze kwa upande wao kwa muda uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali yako pamoja na Watendaji wako wa Wizara yako kwa jinsi mlivyokaa na kukubaliana kwamba sasa *MSD* ipewe mtaji. Tunawapongeza sana, tunaomba *MSD* wafanye kazi kwa weledi, wafanye kazi kwa uhakika Watanzania wanategemea makubwa kutoka kwao. *MSD* walikuwa wanaomba sana wapewe mtaji tunashukuru Serikali imekubali na mtaji umetolewa, tunaomba sasa mtekeleze kwa kupeleka fedha na *MSD* ianze kununua dawa ili iweze ku-*supply* dawa kwa wakati. Vilevile kuna ujenzi wa vifaatiba vinavyotokana na Pamba niwaombe sana *MSD,* kiwanda kijengwe kwa haraka, tunatambua mnakwenda kujenga kiwanda hicho katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hili kwa sababu gani? Zao la pamba tumekuwa na changamoto kubwa sana, wakulima wa Pamba tunapolima Pamba, tunapouza Pamba hii baada ya ku-*gin* inakwenda kuuzwa *lint* nje ya nchi tuna-*export* Pamba asilimia 70 mpaka 75, tunatumia asilimia 20 hadi 25 tu kwa ajili ya viwanda vya ndani, tukiendelea hivi Mkulima wa Pamba siku zote ataathirika na bei ya Soko la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *lint* inauzwa kwa dola 0.73, ukisema mnunuzi wa Pamba anunue kwa faida inabidi anunue Pamba kwa shilingi 800 au 900 *maximum* shilingi 1000. *Indicative price* ya Pamba ni shilingi 1,060 ukisema huyu mnunuzi anunue siku zote atakwenda kutengeneza hasara, wakati siku za nyuma bei ya Pamba ilikuwa inaongezeka, siku za nyuma tulikuwa tunaona bei ya Pamba inaongezeka kutokana na soko la dunia linavyosema, lakini tukiendelea kutegemea soko la dunia ambalo linakuwa na *direct impact* kwa mkulima wa Simiyu, mkulima wa Mwanza hatutamkomboa mkulima. Serikali lazima ifanye *intervention* kuangalia namna ya kumuokoa Mkulima wa Pamba, anapolima Pamba basi alime kwa uhakika na auze kwa bei ya uhakika inayompa faida, bila hivyo hatuwezi kuliinua zao letu la Pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wabunge wengi wamepiga kelele baada ya kusikia kwamba bajeti inakwenda

kupunguza kodi ya mafuta ambayo yanaingizwa kutoka nje yaani kwa maana ya *crude oil* kwenye *palm oil.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *palm oil* siku zote inajulikana duniani ni rahisi, ukiileta kwa bei ambayo umepunguzia kodi huyu muingizajiwa *crude oil* ya *palm oil,* muuzaji wa mafuta ya Pamba, mafuta ya Alizeti hawezi kuingia kwenye *competition* kwa sababu mafuta yake yatauzwa kwa bei ya juu. *Crude oil* bei yake ni chini na kibaya zaidi au kizuri zaidi kwa upande wa *crude oil* ukimpa huyo kodi ya asilimia 35 akiingiza atafanya *refine* aka-*refine* yale mafuta, *by product* yake anakwenda kutengenezea sabuni akitengeneza sabuni atapata faida huko. Mkulima wa Alizeti mafuta yake akikamua Alizeti *by product* yake ni mashudu, Pamba *by product* yake ni mashudu hayana thamani kubwa zaidi ya kuwa chakula cha Wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukimshushia kodi mwenye *crude oil* ya *palm oil,* mimi niliona kwamba ina mantiki lakini baada ya Wabunge wengi kulalamika tumekuja kugundua kwamba ukiweka asilimia 35 ya *crude oil* ukamuwekea *import duty,* akiingiza mafuta akafanya *refine* atauza kwa bei ambayo inafaida kidogo sana lakini atatenengeza faida kwenye sabuni ambayo ni *by product* ya *crude oil.* Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri hebu tujaribu kukaa na ku-*rethin*k, kuona ni namna gani ya kufanya ili kusudi Mtanzania asije akanunua mafuta kwa bei ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua *crisis* ya mafuta inakwenda mpaka kwa muuza *chips, crisis* ya mafuta inakwenda kwa Watanzania moja kwa moja. Kwa hiyo, tuiangalie mahitaji ya mafuta ni tani 680,000 kwa mwaka, Watanzania tunaweza kwa kutumia mbegu zote uwezo wetu ni ku-*produce* tani 300,000 tu. Sasa tani 380,000 inabidi tutoe nje sasa tuangalie ni namna gani ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Ngano. Kuna Mbunge mmoja jana hapa amepiga kelele sana jana kuhusiana na suala la Ngano, lakini Ngano tunaambiwa kwamba mahitaji ya Ngano kwa mwaka ni metriki tani 1,000,000, *production* yetu

Tanzania ni *only 20 percent,* sasa hatuwezi kuishi bila ku-*import* Ngano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lile sharti lililowekwa na Wizara ya Kilimo la kwamba mfanyabiashara anayetaka ku-*import* muwekeeni sharti, asilimia 20 mpaka asilimia 30 ya Ngano anayonunua anunue ndani, *70 percent* anunue kutoka nje, liwe ni sharti ili kusudi aweze kununua Ngano ya ndani anunue na Ngano ya nje, kwa sababu yeye ni mfanyabiashara wa Ngano afanye hivyo ili kuipa soko Ngano yetu ya ndani vilevile na ngano ya nje iweze kuingia lakini mkipandisha sana kodi *impact* inakwenda kwa Mtanzania moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi sasa hivi asubuhi Mama Lishe anapika chapati, chapati ikibaki inalika mchana na ikibaki anaenda kuwapa wanae jioni wanakula. Kwa hiyo, ngano imekuwa ni chakula kikubwa sana. Vilevile hata ukiangalia kwenye mafuta *chips* imekuwa ni chakula kinachoshindana na wali, zamani tulikuwa tunakula wali jioni siku hizi watu wanakula *chips* jioni. Kwa hiyo, ni lazima tuwe makini tukicheza vibaya tukakuta kodi imepanda *impact* inakwenda kwa Watanzania moja kwa moja kwa hili Mheshimiwa Waziri lazima tuwe makini na tuweze kuishauri vizuri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo, nilimwita Mheshimiwa Grace Victor Tendega wakati huo Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, anajiandaa. Niwakumbushe Waheshimiwa wachangiaji unapochangia unazungumza na Kiti usimu-*address* Waziri.

**MHE. GRACE V. TENGEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi nichangie katika Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kurudisha Tume ya Mipango ambayo kwa kweli tumekuwa tukiipigania kwamba irudi na iweze kufanya kazi

yake sawasawa. Ukiangalia katika mpango wa maendeleo wa tatu wa 2022/2023 ulitengewa trilioni 15.0 ambayo ni sawasawa na asilimia 36 ya Bajeti Kuu, hadi tunafika mwezi Aprili 2023 Serikali ilikuwa imeshatumia trilioni 11.5 ambayo ni asilimia 76.5 ambayo kwa kweli ni asilimia nzuri, ninaipongeza na ndiyo maana nimesema napongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru kwa kuondoa zile ada za vyuo vya ufundi ambavyo ni *DIT, MUST* pamoja na *ATC*. Wananchi wengi walikuwa watoto wetu wanapata shida kule lakini kwa kuondoa hiyo wanafunzi wengi watasoma na tunaendeleza elimu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa usikivu ameleta katika misingi yake sita, kuna msingi mmoja wapo wa ongezeko la ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji. Hiki ndiyo kitu cha msingi ambacho tulikuwa tukikipigania kwamba Serikali peke yake haiwezi kufanya kazi bila kuwa na *PPP,* hii itasaidia kwenye masuala mengi kuondoa umaskini lakini pia kuleta ajira, kwa kufanya hivyo unakuta kwamba ni nchi nyingi, Serikali siyo Mwajiri Mkuu, Mwajiri Mkuu ni hizi *private sector.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kuna kitu ambacho *concept* hii haieleweki vizuri, tuna shida kubwa sana ya kutokuielewa kwa nini? Wakati tunakusanya labda kodi tunaagalia vyanzo vya kodi kwa mfano tuna vyanzo 50 vya kodi, tunataka bilioni moja mwaka huu, lakini mwakani tena tuna vyanzo hivyohivyo 50 tunataka bilioni tatu, badala ya kuongeza vyanzo viwe vikubwa ili tuweze kupata kodi nyingi. Kodi nyingi tutaipata tukiwa tumeweza kuweka mazingira wezeshi kwa vijana na watu wengine kuweza kupata mikopo kwa bei rahisi ambayo itawawezesha kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidi sana. Nazungumzia hivi kwa sababu kodi imekuwa kubwa. Kodi ikiwa kubwa, wananchi wengi wanashindwa kujiajiri, wanashinda kuajiri wenzao. Nitatolea mfano. Kwa mfano, mtu ana biashara yake, ameagiza kontena, labda la shilingi milioni 300 limefika pale bandarini, Afisa wa kutoza ushuru anakuja anamwambia kabisa, badala ya shilingi milioni 300, lipa shilingi milioni 70 nami unipe shilingi milioni 20. Watanzania

walio wengi wanajikuta wakiingia huko. Mnaweka mazingira ya watu kutoa rushwa, lakini ukitoza bei ambayo ni *reasonable,* watu watakwenda kulipa na Serikali itapata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujitahidi kuongeza ukubwa wa vyanzo vya mapato ili wananchi wengi waweze kufanya kazi yao na Serikali ipate kodi nzuri. Kwa mfano, unaangalia changamoto iliyotokea Kariakoo, wananchi wengi kupiga kelele, lakini yote hii ni kwa sababu ya kodi kubwa. Mmeona jinsi ambavyo mkitekeleza hivyo wananchi wengi watapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tozo zimekuwa kubwa. Mnatoza magari tozo kubwa. Kwa mfano, gari jipya ili lifike hapa, tozo yake ni kubwa sana. Kodi yake ni kubwa sana. Hata lori mnatoza. Kwa nini mnafanya hivyo? Kwa sababu wananchi wanashindwa ku-*afford* kununua magari mapya, ndiyo maana wanaingiza magari chakavu. Tumeona kabisa magari chakavu yanaingia, na yakiangia yanaharibu mazingira na Serikali vilevile inakosa kodi, kwa sababu magari yale yanakuwa chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wasi-*enjoy* kuendesha magari mapya? Punguzeni kodi ili wananchi wanunue magari mapya. Kwa mfano, lori. Lori ni uchumi, linaweza likaajiri watu wengi sana; dereva, fundi, utingo na watu wengine ambao wanabeba mizigo. Sasa ukiweka ushuru ukawa mdogo, malori mengi yataingia, wananchi watakuwa wanawaletea kodi kila mwaka na mtapata magari mengi ambayo yatakuwa yanahudumia watu na wananchi wengi watapata ajira. Mkianza kuweka kodi kubwa, tunashindwa kupata hivyo. Kwa hiyo, naomba mpunguze kodi katika vitu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, nitazungumzia ongezeko la bei ya mafuta. Bei ya mafuta itakapoongezeka, *automatically* vitu vyote vinapanda bei, na hii ni shida. Kwa nini inafika hapo? Kwa nini tusiwe na utaratibu mzuri wa kuweza kuangalia vyanzo gani vitatupa fedha? Napendekeza kwa mfano, matumizi badala ya mafuta, tuangalie namna tutavyotumia gesi. Tunayo gesi na tumekuwa na upungufu wa

dola hapa ndani. Kwa sababu tuna upungufu wa dola, tuanze kutumia gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dangote anatumia gesi. Amekuja kuwekeza kwenye viwanda, lakini magari yake yanatumia gesi. Kwa nini Serikali tusianze na magari ya Serikali, mwendokasi tutumie gesi yetu? Kwanza tuta-*save* dola, tutatunza mazingira na vilevile ajira zitakuwa nyingi. Tukianzia hapo, na wananchi wataanza kutumia gesi katika magari yao, halafu tutakuwa tume-*minimize* kutumia dola yetu kwenda nje na tutabaki nayo hapa ndani. Kwa hiyo, badala ya ku-*import* mafuta kwa kutumia hiyo, tutakuwa tunatumia gesi yetu. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri tuangalie suala hili kwa umakini kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, naomba nichangie pia kuhusu kutengeneza mabilionea. Yaani tutengeneze hata mabilionea kumi ambao ndio watakuja kutuletea mambo mengi katika nchi hii. Hayati Dkt. Magufuli aliweza kuwezesha Kiwanda cha Sukari cha Bakhresa, akatoa eneo, akaiamuru Benki ya Kilimo iweze kum-*support, I think* ilikuwa shilingi bilioni 100 kama sikosei. Sasa hivi tunaanza kuona sukari siyo shida kubwa vile. Kwa nini tusiende tukatengeneza watu kama hao hata kumi ili waweze kufanya vitu vikubwa kama hivyo vikaweza kusaidia nchi yetu kusonga mbele. Kwa hiyo, nashauri tufanye hivyo. Hii itatusaidia sana kuondoa tatizo la ajira, kuondoa umaskini na vilevile uchumi utakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ongezeko la fedha kwenye utoaji wa simu. Tunajua nia siyo mbaya, lakini mnawaonea wananchi wa chini. Kwa sababu unapoweka hiyo ina-*cut across* kwa mwananchi wa kipato cha chini na kipato cha juu. Sasa wote wanatoa, unapofanya hivyo, wale wananchi kule kijijini unakuta mtu anatumiwa shilingi 5,000; shilingi 10,000, au shilingi 6,000, unapokata, ujue wale wote inawakuta. Kwa nini tusiangalie kitu kingine kitakachowasaidia? Kwa sababu wananchi wetu wanapata shida. Unapoweka shilingi 10,000, unamkata tena, anakuwa hapati fedha inayotakiwa. Kwa hiyo, ina-*cut across* kwa wote. Nia ni nzuri, lakini tuangalie namna ambavyo inaweza ikafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo ya pikipiki, sikatai, pia ni tozo nzuri, lakini mimi nilikuwa nadhani, utaratibu wa kupata kodi lazima uangalie *economy*, yaani usitumie hela nyingi kuchukua pesa kidogo. Nataka kujua kwa Mheshimiwa Waziri, anapokuja hapa atuambie, tuna pikipiki ngapi ambazo anatarajia kukusanya hizo kodi zake na ana *staff* wangapi wa kukusanya hizo pesa kutoka kwenye hizo pikipiki? Kwa sababu ni ngumu sana ukiangalia, lakini atakuja atatueleza, ni namna gani atafanya ili aweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi kwa kweli unakuta wana kipato cha chini, wale vijana ndio wanaanza kutafuta maisha. Kwa hiyo, tuangalie namna ambavyo tunapona. Tuna vyanzo vingi vikubwa. Ukiangalia vyanzo ni vingi vikubwa ambavyo tunaweza tukapata fedha nyingi na kuweza kuendesha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la kilimo. Nitajikita kwenye kilimo cha parachichi. Kule Iringa tunalima parachichi, Njombe na kwingineko wanalima parachichi. Tunapenda tuimarishe vituo vya tafiti. Kwa mfano, kuna kile kikonyo kinaitwa sayo. Kile kikonyo ni cha muda mrefu, tuangalie namna ya kuhuisha ili mbegu ile iendelee kuwa na ubora. Ikiendelea kuwa na ubora, wananchi wataweza kuzalisha parachichi nyingi zaidi. Kwa hiyo, hiyo imekuwa ni changamoto na tumeona kule kwetu, kile kikonyo kikiendelea kwa ile ile *privet* ya mwanzo inaleta shida katika uletaji wa mazao. Kwa hiyo, parachichi inapungua jinsi unavyoendelea kama kile kikonyo hakijawa kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke msamaha wa kodi ya magari ya baridi *(cold trucks)*, zile *cold containers*. Mkiweka msamaha wa kodi, wananchi wanaweza wakafanikiwa sana, kwa sababu imekuwa ni gharama kubwa, wananchi wanashindwa kuhimili kumudu hayo magari na kusafirisha nje, na soko linataka uhifadhi katika chombo kama kile. Kwa hiyo, mkikitolea msamaha hapo, mtawezesha wananchi wangu wa Mkoa wa Iringa, wale wakulima wa parachichi na wengine katika mikoa mingine waweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, hata hivyo atanza kwanza Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said na kisha atakuja Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Awali ya yote, naungana na Wabunge wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia kuiona siku ya leo na baraka zake kwa nyakati tofauti tofauti. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu maisha yetu ni rasilimali na hazina anayotujalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mji, nathibitisha kabisa kwamba mambo mengi niliyokuwa nimeahidi kwenye uchaguzi, yametekelezwa kwa asilimia kubwa sana. Nampongeza Mheshimiwa Rais, Mawaziri, kuanzia kwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote. Kwa sababu mwaka jana 2022, wakati tunahitimisha Bunge la Bajeti nilikuwa nimesema nashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri Mwigulu, akanitania siku moja akasema, "kwa umri wako ukishika Shilingi na hurudishi itakuaje?" Nikawa nacheka. Kwa maana ya kuona kwamba ninahofia yale mambo ambayo tuliyaandika kwenye bajeti na hayatatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa staha na furaha kubwa kwa niaba ya wananchi, naipongeza sana Serikali kwa sababu kazi kubwa imefanyika, na pia ndani ya mwezi huu wa Sita nadhani, kuanzia tulipoanza hili Bunge letu la Bajeti mpaka sasa, Jimbo la Mbulu Mji limepokea fedha nyingi sana kutoka Serikalini. Fedha zilizopokelewa, nyingine hata hazikuwa kwenye

mpango ule wa awali, zilikuwa zinazokuja kama fedha za kimkakati kwa ajili ya kutatua matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa sababu Mbulu Mji, sisi wananchi wake kama Halmashauri, tunakusanya mapato madogo sana, lakini mahitaji yetu ni makubwa sana Serikalini, kiasi kwamba wakati fulani unajiuliza, sasa hayo tutayatatuaje? Kwa hiyo, natuma ujumbe huu kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote kuwashukuru sana. Kwa sababu kila sekta katika mwaka huu wa bajeti ni takribani karibu Shilingi bilioni saba au nane zimepelekwa kwenye Jimbo la Mbulu Mji, katika robo hii ambayo tunamaliza sasa kama dakika za mwisho za kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Makamu wa Rais kwa ziara anazofanya katika majimbo yetu. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya hivi karibuni kule Jijini Arusha katika halaiki ya kanisa kwa ajili ya kuelezea hali halisi ya taharuki ambayo Watanzania wanaichukulia kwa hatua ya tofauti zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kutoa mchango wangu mchache sasa. Kwanza niungane na Wabunge wenzangu ambao walikuwa wanaipigia kelele dhana hii ya kuondoa au kupunguza kodi kwa bidhaa ya mafuta kutoka nje, na bidhaa nyingine, lakini tunataka kuingiza bidhaa hiyo, kupunguza na kujenga soko la ndani. Niseme tu kwamba, nchi yoyote ni lazima ijenge uchumi wake wa ndani ili iweze kwenda mbele, kwa sababu nchi nyingi zinajenga uchumi wa chini na uchumi wa kati na baadaye inaenda kwenye uchumi wa kuuza nje na pia kujenga uwezo wa wananchi katika rasimali walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na Wabunge wenzangu kwamba eneo hili la kupunguza kodi kwenye bidhaa za nje pengine itaua viwanda vya ndani na mwisho wake wananchi wetu watashindwa katika uzalishaji. Kwa sababu hali ya uzalishaji itatofautiana na ile ya kipato wanachopata hasa kwenye sekta ya kilimo na sekta zingine kwa ajili ya kupungua kwa gharama kubwa na uchumi kushuka na bidhaa zetu kushindwa

kushindana na bidhaa zinazotoka nje. Kwa hiyo, rai yangu hapa ni kwamba tuangalie kwa umakini sana eneo hili na pia kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita lile la miaka mitano, kwenye Halmashauri tulikuwa na viwanda vya ndani kama 100. Vile viwanda vilishafika hatua ya kuchakata na kufungasha malighafi za ndani, na pia viwanda vile vilikuwa vinatoa ajira kwa wananchi wa chini, wale waliioko kwenye majimbo. Vimekuja kufa kwa ajili ya matatizo ya wataalam na uelewa mdogo wa usimamizi, kutokana na kwamba hatukua na muundo mzuri. Hapa ushauri wangu ni kwamba tuangalie muundo wa *SIDO* na taasisi nyingine zitakazolinda viwanda vya ndani hasa hizi ndogo ndogo ambazo zinafungasha mazao ya wananchi. Pia kule kuna ajira za muda za wale wanaofanya vibarua, na pia maisha ya wananchi wetu yanaendelea na huduma za familia zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kama itawezekana, tuijengee uwezo *SIDO,* na tuwe na matawi ya *SIDO* kwenye wilaya zetu ili kuvilea viwanda vidogo vya chini kwa ajili ya kujenga uwezo wa wananchi. Tunapozungumza uwezo wa wananchi, tunachukua kundi kubwa la viwanda vidogo vidogo ambavyo watafanyakazi, watarudi makwao, lakini Maisha yao yanaendelea, wanasomesha watoto na pia wanapata huduma ya kila siku kupitia familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kuondoa kodi. Miaka miwili iliyopita nilikuwa nimeuliza swali hapa Bungeni kwa ajili ya vijana wa vyuo vya chini na vyuo vya kati kuwa na gharama kubwa ya kuwasomesha, na vijana wengi wanashindwa na familia nyingi zinalemewa kwa ajili ya gharama. Kwa sababu tulikuwa tunakuta mwanafunzi anayesoma pengine Shahada ya Chuo Kikuu anasoma kwa gharama sawa na yule ambaye anasoma chuo cha cheti, wakati mwananchi yule anayemshomesha yule, gharama ile ilikuwa hailingani na kipato chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ajili ya kuondoa ada hizi na

gharama hizi katika baadhi ya vyuo. Rai yangu hapa ni kwamba tuangalie vyuo vingine pia ambavyo kwa uwezo wetu tukijijenga, tuweze kuwaweka na kundi hilo la vyuo vya cheti na vyuo vingine ili kujenga uwezo wa watendaji au watumishi ama wataalamu wa ngazi hizi za chini. Kwa sababu hata kufa kwa viwanda ni pamoja na hawa wataalamu wa ngazi za chini wanakuwa wachache. Kwa hiyo, tatizo hili ni kubwa kwa kadiri mnavyoona. Kwa vyovyote vile, hapa tunamwondolea mwananchi gharama kubwa. Alishamsomesha mtoto shule ya kata na sasa anaenda kwenye chuo kwa ajili ya kumjengea uwezo ili aweze kukabiliana na hali ya ulimwengu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haya ni majumuisho, katika taarifa yetu ya bajeti kuu, tumeongelea eneo hili la wastaafu. Wastaafu wa zamani pensheni yao ni shilingi 100,000 kwa mwezi. Yaani bima anayotakiwa ahudumiwe kwa maisha aliyonayo, inaweza kuwa shilingi 600,000, lakini yeye kwa mwezi anachopata ni shilingi 100,000 au shilingi 150,000. Nadhani Serikali itazame vizuri, iangalie namna gani watumishi hawa waliotumikia Taifa letu tunawaangalia ili nao basi wasiombolezee Serikali yetu, lakini pia wawe na amani wanapoelekea katika uzee wao na waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee eneo la kuongeza ukusanyaji au utaratibu wa ukusanyaji wa mapato. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kwenye kuhitimisha, angetuambia sisi Wabunge basi, kwa Serikali na taasisi za umma, ni lini siku ya mwisho ya matumizi ya mashine za *POS* kukusanya fedha za Serikali? Kwa sababu huko ndiko ambao fedha nyingi tunashindwa kukusanya na pia kuingia kwenye mfumo wa Serikali, kujenga uchumi wa nchi yetu na pia mapato yetu kuwa halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha mbichi zinazopotea katika *corridor* hiyo au katika muundo huo na tutakapotoa tamko; kwa sababu kama tunafanya mambo makubwa sana hayo, tukumbuke kuwa hata na hilo la *POS* linawezekana kwa nchi yetu. Tutafute muundo wa maeneo yote hayo ambayo yanakusanya mapato ya Serikali, yawe yanaingia kwenye mfumo na kuweza kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba bado tunahitaji kujenga uwezo wa wakusanyaji, kwa maana, kuna wilaya zetu nyingi hazina majengo ya wakusanyaji kwa maana ya *TRA*. Pia katika halmashauri hatuna Maafisa ambao wanaweza kukidhi haja na kujaza nafasi hizo ambazo ni muhimu sana katika makusanyo ya Serikali. Nilikuwa nafikiri hilo litatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba tumehangaika sana, hatuwezi kuwaajiri hawa vijana waliomaliza chuo, hawa ambao tayari wengine ni wa *certificate* wengine ni wa *diploma*, wengine ni wa *degree*. Serikali ione kwamba namna pekee ya hawa vijana kupata ajira ni kuangalia sheria za sekta binafsi za ajira, na maslahi katika sekta binafsi kwenye ajira, na pia namna ambavyo tutachochea kupitia viwanda ambavyo tutakuwa navyo ndani ya nchi na vijana wataajiriwa kutokana na taaluma zao ili kuondoa mzigo mkubwa uliopo kwa Serikali. Kwa sababu kwa vyovyote vile, mbele ya safari Serikali haitaweza kubeba jukumu hili la kuwaajiri hao vijana, kwa sababu kila mwaka wanamaliza masomo yao na wanapomaliza wanaiangalia Serikali kama baba yao ili iweze kuwaajiri na hawataajirika kwa sababu ya uchache wa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mwaka wa fedha unaokuja tuone namna ya kuajiri zile takwimu ambazo tumeziombea kwa ajili ya kupunguza idadi kubwa ya hao vijana. Tunajua hatuwezi kuajiri mara moja, lakini angalau tutafute madirisha ya kuajiri. Hata katika nchi zinazotuzunguka kwa uhusiano mzuri tulionao, basi tuwe na sehemu hiyo ya kulielezea jambo hili katika sura ambayo inaweza ikaleta tafsiri nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali, siyo kuilaumu tu; hata kwa hii hatua iliyoichukua ya mazao, kwa maana kuna muundo rasmi unaoandaliwa ili kuona kwamba angalau hata kama tutauza mauzo nje, Serikali itapata kodi, na pia hatutauza yote baadaye tukabaki na njaa ambayo ni janga la Taifa na mwisho wa siku haitawezekana. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri aliyekuwa anatoa tafsiri hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni Mamlaka ya Chakula na Lishe, kwa maana ya hasara inayotokea katika nchi yetu ni kubwa sana, kwa sababu ya uteketezaji wa bidhaa bandia na bidhaa ambazo zinazoingizwa nchini na tunazotengeneza kama bidhaa feki. Nilikuwa nashauri, kama itawezekana, tutazame muundo wetu wa kudhibiti uingizaji na utengenezaji wa bidhaa bandia, kwa sababu wanaoathirika sana sio wahusika, ni wale wafanyabiashara wa kawaida na wanapokamatwa kwa kukutwa na hiyo bidhaa, wanapata hasara kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taasisi hii tukiutazama na namna ambavyo utaweza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nitachangia mengine kwa maandishi kwa sababu nina mambo mengi sana niliyaorodhesha katika mchango wangu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said wakati huo Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa wanajiandaa.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Kuna msanii Zanzibar alisema, "Mungu akitaka kukupa hakuletei barua, hukupa usingizini pasipo mwenyewe kujua." Kuna msanii mwingine akasema, "Mpewa hapokonyeki, aliyepewa kapewa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nikasema hivi? Nafasi ya uongozi ikiwemo Rais na viongozi wengine nafasi hizi hupangwa na *Allah Subhannah Wataala*. Mwenyezi Mungu kama hataki uwe

Rais basi utavaa makoti kila siku ukajitazama kwenye vioo mimi nitakuwa Rais lakini huwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan cheo hichi alitangazwa na Mwenyezi Mungu ndiye aliyempa. Vyeo hivi kuna leo kutenda kuna kesho kuulizwa lakini Mheshimiwa Samia ni mcha Mungu. Mheshimiwa Samia anafanya mambo makubwa kuwatumikia Watanzania na Watanzania wote ni mashahidi na sisi Wabunge ni mashahidi. Siku zote binadamu tunapofanya mazuri tunakuwa hatusifii na lile zuri halisifiwi baya ndiyo linasifiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamzungumza Dkt. Samia tunampigia makofi sana muda wote nafikiri Wabunge wote wanamzungumza Mama Dkt. Samia kwa imani yao na imani ya Mama Dkt. Samia anayafanya lakini Mheshimiwa Dkt. Samia ana jeshi lake. Ana jeshi linalomsaidia kazi ya kumpongeza Mama Dkt. Samia na miaka miwili aliyoifanyia kazi na jeshi hili ni Mawaziri wetu na Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na Wakurugenzi. Hilo ndiyo jeshi la Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini Mawaziri wetu wanapambana. Wanafanya kazi kubwa sana kuwafanyia Watanzania na kazi hizi zinaonekana. Kwa nini tusiwapongeze, kwa nini tusiwaombee? Mawaziri hawa wakiongozwa na Kamanda wao Waziri Mkuu kwa kweli wanastahili sifa zote. Tumpigieni makofi Rais wetu lakini na Mawaziri wetu wanafanya kazi kubwa sana, wanastahili sifa. Kuna jeshi la ardhini na jeshi la angani. Naibu Mawaziri ni majeshi wa ardhini, Mawaziri wenyewe ni majeshi ya angani wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliposoma Bajeti yake aliisoma kwa madaha lakini kwa uelewa mkubwa na tulimuelewa tukamfahamu hata Watanzania waliifahamu Bajeti hii. Sasa basi kazi iliyobakia jeshi la Mama Samia wakaitekeleze bajeti hii ifanye kazi kwa weledi zaidi. Miradi hii ikakamilike fedha zifike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimuombe Ndugu yangu *Comrade* Waziri wa Fedha kwa kweli kwenye makusanyo huko kumechafuka sana bado kazi hii hatujaifanyia kazi. Tuendelee kupambana na ukusanyaji wa kodi. Tunapokwenda kukusanya kodi, wale tunaowafuata ni binadamu na binadamu siku zote ana mbinu nyingi. Kwa hivyo twende kwa nasaha, kwa maridhiano tukawashauri lakini tuwaambie. Tusiende kwa vishindo kuwatukana, kupambana nao itakuwa hatufanikiwi. Letu tunalotaka itakuwa hatufanikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu za makusanyo rushwa ni nyingi, kunanuka rushwa. Udanganyifu ni mwingi, unakwenda kununua kitu anakwambia unataka cha shilingi 100,000 ukimwambia nakitaka nipe risiti anakwambia basi shilingi 150,000, itakuwa hatufiki. Mimi naomba jeshi la Mama Samia tushirikiane na Wabunge tukafanye kazi ya makusanyo jamani ndiyo tutapata maji, barabara na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja suala la Muungano. Viongozi wetu Hayati Karume na Hayati Nyerere walipoungana Muungano huu waliungana kwa makaratasi wakatiliana saini lakini hawakuridhika, ukachukuliwa udongo wa Zanzibar na udongo wa Tanganyika ukaja ukachanganywa. Leo udongo ule nadhani hakuna Mtanzania wala mzungu atakayekuja kuubagua udongo ule kwa muda huu uliofika kwa awamu hii, sisi hatukuungana tena kwa karatasi wala kwa udongo, tumeungana kwa damu. Sisi tumeshachanganya damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uduvi unaupekecha pekecha Muungano huu lakini tunawaambia ole wao jeshi litakuwa ni la Mama Samia lakini wanawake tu ndiyo tutakaopambana nao. Hatuwezi ukavunjika Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja kwenye maliasili. Wabunge wengi wanawake, wanaume wanalia kuhusu tembo. Tembo huyu anatupatia faida, tunapata fedha za kigeni lakini tembo hii pia ni dawa kwa binadamu. Niiombe Serikali tembo sasa hivi anaua watu ni hatari. Tusiachie hii tembo ikawa

inaua watu ni hatari na hatuwezi kuwaua tembo hawa kwa sababu tunapata faida nyingi sana. Nadhani hili janga liwe la Kitaifa wa kuisimamia hii tembo isiue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la maadili ya nchi yetu. Kuna watu kama ni kutoka ughaibuni, kama ni kutoka Afrika, kama Ulaya wamekuwa wanawadhalilisha viongozi wetu wanawatukana kwenye mitandao. Tunasema hii haikubaliki wala hatukubali na tunashangaa leo mwanamke utachukua simu utamtukana mwanamke mwenzio, iweje na lipi unalomtukania? Kama uko Ulaya basi shuka uje huku Afrika tukutane uso kwa uso tutukanane sisi na wewe na kama wewe unatukana uko Ulaya hayo matusi unayoyatukana basi yawe yako mwenyewe siyo ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said lakini zaidi kwa kuketi mwenyewe baada ya kuona muda wako umekwisha. Nashukuru sana. Nilimwita Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo wakati huo Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa anajiandaa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema nami niweze kuchangia Wizara hii ya Fedha kwa maana ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa Rais mwanamke wa kwanza *East Africa.* Ninampongeza sana hiyo ni heshima kubwa sana kwetu lakini pia amekuwa Makamu wa Rais wa kwanza Tanzania. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia kuwa Dkt. Tulia Ackson agombee nafasi ya Urais *IPU.* Pongezi nyingi sana kwako Dkt. Tulia namna ambavyo unakwenda kugombea hii nafasi tunakuombea sana kwa

Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu atasimama na wewe atakwenda kutimiza haja ya moyo wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa. Alifanya kazi kubwa sana pale Dar es Salaam, alisimama kwa muda mrefu sana akiongea na wafanyabiashara. Yote hiyo ni kwa ajili ya kuweka nchi sawa sawa, kutengeneza amani, upendo na mshikamano. Alituliza mioyo ya wafanyabiashara wa Tanzania. Pongezi nyingi sana kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwa nawe katika majukumu yako popote unapokuwa awe pamoja na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaingia kuchangia kwenye Mpango huu wa Serikali. Nipongeze *TRA*, *TRA* wanafanya kazi nzuri ya kukusanya kodi ndipo ambapo maeneo mengi wanatimiza malengo yao ni kwa sababu ya utiifu na nidhamu waliyonayo wafanyabiashara kuchangia ama kulipa kodi kwa sababu wanajua kodi ndiyo maendeleo ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani wafanyabiashara hawa wanapata changamoto hasa pale wanapokuwa wamejipanga na kujiandaa kwa ajili ya kwenda kulipa kodi kuna tatizo kubwa la mtandao kwa maana ya *control number*. *Control number* ni tatizo kubwa. Serikali kwa maana ya *TRA* wanakuwa na *operation* ya kukamata vyombo vya moto. Utakuta wamekamata bajaji, magari na wafanyabiashara wale wako tayari kulipa lakini anafika *TRA* mtandao unasumbua uko chini, wanakwama kulipa kwa wakati lakini bado wanaendelea kushikiliwa vyombo vyao kiasi kwamba wanashindwa kuendelea kufanya biashara kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakati huo kwa wafanyabiashara hawa wadogo wa bajaji inawezekana kabisa amekopa hiyo fedha kwa ajili ya kwenda kulipa. Sasa pale akikwama kulipa mtandao uko chini, *control number* inakwama kutolewa ndipo ambapo shida inapoanzia. Anauhitaji kwa ajili ya kutumia fedha kwa ajili ya familia yake lakini inashindikana sijajua, tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Jeshi la Polisi, Jeshi la Polisi akikamata gari akiona lina makosa, *control number* inatoka hapo hapo kwa kosa alilonalo anatakiwa alipie lakini nikiangalia na tukiangalia Watanzania kwenye Wizara hii ndiyo wenye kihenge, ndiyo mmeshika fedha zote za nchi. Mnashindwa nini kuboresha utaratibu *TRA* wa *control number* kutoka kwa wakati ili Watanzania walipe wakaendelee kufanya majukumu yao? Ni nini kinakwamisha hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mbunge wa Wanawake wa Mkoa wa Mbeya. Wakati fulani napata simu za malalamiko hata nje ya Wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Nataka nitoe jambo hili ambalo nilipigiwa simu kutoka Dar es Salaam ni kero za wananchi. *TRA* wanakuwa na *operation,* siku moja walisimama *TAZARA* pale wakakamata gari ya mfanyabiashara, ile gari ilikuwa inaenda kupakia mzigo kwa bahati mbaya sana tajiri alikuwa hana taarifa kwamba ile gari inadaiwa kumbe kuna makosa ameyasababisha dereva ambaye wakati huo hakuwa kwenye hiyo gari. Tajiri yuko tayari kulipa hiyo fedha, anamwambia kwamba natuma hiyo fedha ilipwe sasa hivi muachie gari ikafanye kazi, *TRA* wanamwambia wanasema, "Hiyo gari lazima iende *yard* Tabata, ikipaki Tabata urudi hapa uende Vingunguti ndipo ukalipie kodi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muda wa nani, kwa gharama za nani na kule *yard* inatakiwa ikalipe kodi? Sasa mfanyabiashara huyu anachelewesha muda, yuko tayari kulipa na pale siyo majembe wapo ni wahusika wa *TRA,* maafisa wa *TRA* wako pale wanasema hawawezi kutoa *control number* kwa wakati, tatizo linakuwa wapi? Mbona Jeshi la Polisi linafanya haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi wenye kihenge ambao ndiyo mnashika fedha za nchi kunakuwa na tatizo gani kulipa, kutoa *control number* papo kwa papo ili kazi zingine ziendelee? Nashauri sana Serikali mlitazame hili la ukusanyaji kodi, yamkini mapato mengine yanapotea kwa sababu ya kutokupokea fedha kwa wakati, kutokupokea mapato kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo kidogo imekuwa changamoto. Wafanyabiashara hawa ni wasikivu kwa

kulipa kodi. Kuna tatizo moja, kaka yangu pale Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anafanya kazi nzuri sana, kuna kipengele kimoja kaka yangu ninaomba sana utazame hili. Kuna hii *service levy; service levy* inakwenda kukata mtaji wa mfanyabiashara. Wafanyabiashara hawakatai kulipa *service levy* kwa sababu wanajua kodi ndiyo kila kitu. Ninaomba sana *service levy* mfanyabiashara analipa 0.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, tunaomba yaani ingefaa angalau basi iwe 0.1 kulipa ni ndani ya Wizara yako hizo fedha zinakusanywa zinakwenda zote kwenye kihenge kimoja. Mkiliangalia hili kwa undani tunaomba msaidie hawa wafanyabiashara najua hili liko ndani ya TAMISEMI ndani ya upande wa leseni lakini hili jambo kwa sababu ni Serikali na huu ni mchango wa Bajeti ninaomba mkalitazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba amefanya kazi nzuri sana pale alipokuwa akisoma na ipo kwenye maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amewaonea huruma sana, amewajali sana wafanyabiashara ameamuru wasifungiwe maduka yao badala yake wanatakiwa waelimishwe ili waende kulipa kodi. Kwa sababu mfanyabiashara huyu akifungiwa duka lake atatafuta fedha wapi za kwenda kulipa kodi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliona hili kwa undani sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa hapa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea nimekatishwa kidogo hapa maana mimi nilikuwa naendelea kufafanua namna gani umewatendea haki wafanyabiashara wa Tanzania. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba umewatendea haki sana. Na mimi kwa niaba ya watanzania, wafanyabiashara ninakupongeza na kukushukuru kwamba hili

umefanya vizuri hasa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya wanakwenda kufanya kazi zao bila kutishwatishwa bila vitisho…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, na muda wako umekwisha.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa muda ulionipatia lakini niseme kwamba Mungu abariki sana mpango huu, na ninaunga mkono hoja, ahsante sana, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba taarifa ni kwa idhini ya Spika au kiti, kwa hiyo sio kwamba ukisema utazungumza tu. Haya tunaendelea nilimwita Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, wakati huo Mheshimiwa Malima na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu wanajiandaa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii, lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia leo hotuba ya bajeti ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uendelevu wa kukusanya mapato ya ndani ambayo ni chanya. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa usimamizi mzuri, na Mawaziri wengine wa kisekta. Kumbukumbu zinanionesha hapa mapato yetu ya ndani, ukurasa namba saba, mwaka 2020/2021 yalikuwa trilioni 20.59, lakini 2021/2022 tukapata trilioni 24.4, hii 2023 ambayo ndiyo tunayo sasa mpaka Aprili tulikuwa na trilioni 21.67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yetu ya kutoka *TRA* kwa mwezi sasa yamepanda kuwa trilioni 2.63. kwa hiyo ukiangalia miezi iliyobaki hapa yatavuka trilioni 24 ya mwaka jana; ndiyo sababu nikasema kuna ongezeko chanya. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba hili limesimamiwa na mapato yetu hayaendi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili vilevile niwapongeze wale waliweza ku-*introduce* teknolojia hapa. Kuna *EFD* inafanya kazi kubwa ya kutoa risiti kwenye maeneo yetu. Kwa bahati mbaya sana watu wengi hawana uzoevu wa kuomba risiti na mwisho wa wakati ni kwamba kuna mahali mapato ya Serikali yanapotea. Kwa hiyo kwa hili pamoja na kushauriana sisi wenyewe lakini tunashauri vilevile wafanyabiashara wote wajiandae kuhakikisha kwamba wanapouza watoe risiti na sisi tunapoenda kununua tuombe risiti kwa ajili ya kuhakikisha mapato ya Serikali yanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *ETS* ambayo nayo imesaidia kwamba bidhaa zetu zimekuwa *stamped* tuongeze tu wigo wa hiyo *stamping* kuhakikisha kwamba sasa tunaweza kuzitambua na mapato yetu yanaweza kuendelea kuongezeka yavuke hiki ambacho tunakiona. Maana tukiendelea kuwa na mapato mengi ya ndani kuna wakati tutafikia kama tukifanya vizuri sana tunaweza ku-*support* bajeti yetu kwa asilimia hata 75. Tukienda huko maana yake ni kwamba sasa tutakuwa tumeanza kusogea mbele zaidi kuliko ambako sasa hivi tuko. Kwa hiyo ushauri wangu kwenye Serikali hapa tuendelee kuangalia vyanzo vingine kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yanaongezeka yaweze ku-*support* bajeti na miradi yetu mingi iwe *financed* kutoka kwenye mapato yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nitakalochangia ni sekta za uzalishaji, mara nyingi hupenda kuzizungumzia sana. Ili uchumi wetu uchangamke hatuna majibu rahisi, ni lazima sekta za uzalishaji zizalishe sana na mchango wa Pato la Taifa kutoka kwenye kilimo, mifugo na hata uvuvi uwe mkubwa. Ukishakuwa mkubwa, maana yake uchumi wetu utachangamka. Kwa nini nasema utachangamka? Mnajua kabisa dhima yetu ni kuwa na uchumi shindani na shirikishi. Sasa ili uwe shindani na shirikishi lazima tuwashirikishe wananchi wengi zaidi; na hawa wengi wameajiriwa kwenye kilimo, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia hapa kwenye ukurasa namba 11 mwaka 2021/2022 tulibajeti kilimo bilioni 294 lakini mwaka 2022/2023 tukabajeti 954.0 billion. Mwaka huu tuna billioni 970.8 kuna ongezeko la kama bilioni 16.8 hivi. Hii nikiangalia mimi

naiona kama ni ndogo kwa sababu ya ushirikishi ule wa wananchi wengi. Ningeomba tu twende tuangalie kwenye *Malabo Declaration* itakayotupeleka kwenye *10 percent* kadiri tunavyozidi Kwenda, ili tuendelee kuhakikisha kwamba kilimo sasa kinaweza kuwa ndio uti wa mgongo wa Taifa. Kwa sababu tulitangaza kilimo uti wa mgongo wa Taifa kikiwa kinapewa bajeti ya bilioni 200. Sasa uti wa mgongo unaopewa bilioni 200 nafikiri maneno yalikuwa yamekosewa. Kwa hiyo niwaombe sana niishauri Serikali tuendelee kuongeza pesa eneo hili ili watu wengi waendelee kuajiriwa na kushirikishwa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaona kwa bajeti ile ya mwaka jana imesaidia upatikanaji wa pembejeo za kilimo lakini imetupatia kilimo cha mashamba makubwa *(broke farms)* ambayo yameanza sasa kuratibiwa na Waziri muhusika. Vilevile imepewa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, imeanza kushughulika na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, na mwisho inatakiwa iendelee kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo. Ukiyaona haya yote yaliyotajwa kama yametekelezwa na yakitekelezwa vizuri maana yake hapa ndipo palipo na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kulima sana ni lazima uchumi wetu uwe unaongozwa na soko, kwamba *demand* ya hiki kitu iko wapi, mahindi yanatakiwa wapi, alizeti inatakiwa wapi. Kama inatakiwa kwa wingi na hicho ambacho kinaonekana kwamba bei yake ikawa nzuri zaidi wakulima wataendelea kulima kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa ruzuku, lakini mwaka jana nilishauri Serikali kwamba ruzuku ile ya mbolea iliyotolewa wakulima wengi hawakufaidika nayo kwa sababu vituo vya upatikanaji wa mbolea vilikuwa mbali na wananchi. Mwaka huu viongezwe ili kuhakikisha kwamba vinawakaribia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ruzuku hii wananchi wengi ambao walitakiwa kujiandikisha hawakujiandikisha wengine. Kwa hiyo tuombe sana sasa daftari la kujiandikisha lifanyiwe uhariri upya ili wajiandikishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hii ruzuku ya mbolea iliyotolewa hapa tuhakikishe kwamba huduma za ugani kutoka kwa hawa maafisa ugani zinapatikana ili wananchi wajue ni namna gani ya hiyo ruzuku ya mbolea kuitumia kwa ajili ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwenye kilimo hapa nizungumzie skimu za umwagiliaji. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwamba niliona hata kule Buzanda kuna skimu sasa hata ya kutengeneza kutoka Ziwa Victoria. Najua na maeneo mengine yanayozunguka Ziwa Victoria yanatengeneza skimu. Kwenye hili upembuzi yakinifu ufanyike mapema kwenye maeneo yetu ili skimu hiyo zianze kufanya kazi; badala ya wananchi kuzalisha mara moja wazalishe mara tatu na uchumi wao utakuwa umepanda, na uchumi ukipanda tutakuwa tayari tumepata uchumi shindani na shirikishi na hivyo uchumi wetu utaonekana sasa ni shindani hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya hifadhi ya chakula. Nimeziona tani 400,000 zinatakiwa kuhifadhiwa, sina uhakika kama maeneo mengine walipata shida kama ya kwangu kwamba debe la mahindi mwaka jana lilifikia shilingi 25,000 mpaka 27,000. Kwa hiyo niombe sana uhifadhi wa chakula ufanyiwe kazi kwa umakini zaidi ili inapotekea *crisis* kama iliyotokea mwaka jana au mwaka huu wa fedha Serikali iwe na uwezo wa kuwasaidia wananchi wasikutane na bei ambazo sasa hawawezi kununua tena. Ninaamini hili likifanyika mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna sekta nyingine ya uzalishaji ambayo ni ya uvuvi. Nimeona wanasema watanunua boti 160 wameshanunua 118. Kuna kitu cha kufanya hapa. Kwenye uvuvi ndani ya nchi hii jirani yangu tu Mwijage hapa boti 160 zikipelekwa hazitoshi, nchi nzima boti 160? Hapa naomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu waangalieni kwa jicho la huruma hawa watu wa uvuvi. Hatuwezi kupeleka boti 160 nchi nzima tukasema tumeenda kuchangamsha sekta ya uvuvi, tutakuwa bado hatujafanya kitu cha maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mifugo ukiangalia bado tuna hoja kubwa ya malisho. Kwa hiyo mifugo tuliyonayo haina tija, tuna mifugo mingi lakini ukiangalia ng'ombe mmoja anatoa lita moja, bado hakuna tija kwenye sekta hii. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili liangaliwe upya kuona namna gani tunaweza kutengeneza sekta yetu hii hizi za uzalishaji zikaweza kuwa na tija na uchumi wa nchi ukaweza shindani na shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii kitu cha tatu nilitaka kuchangia niwapongeze sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri. Kulikuwa na hoja ya vijana wanaosoma kwenye vyuo vyetu vya *DIT,* Mbeya *University* na Arusha Technical Collage. Hawa wanamaliza *form four* wanakwenda kule kimsingi ni kama wale wanamaliza *form four* kwenda *form five* na *form six,* lakini wao walitakiwa walipie ada. Sasa hii ada hawa ni watoto wa wakulima lakini Serikali kupitia Mheshimiwa Rais, Rais makini Dkt. Samia Suluhu Hassan ameliona hili kwamba sasa hawa watu wa *DIT* wameondolewa ada hiyo. Hizi *tertiary institutes* tunazihitaji sana kwa ajili kutengeneza kupata mafundi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi huko nyuma nilisoma nikiwa *tech*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa George Natany Malima wakati huo Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Cosato David Chumi wanajiandaa.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia bajeti hii ya Serikali. Kwanza nianze na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kazi nyingi zinazofanyika vizuri katika nchi yetu. Sisi kule watu wa Mpwapwa tumepata miradi

mingi sana, haijawahi kutokea katika historia ya jimbo letu. Tumepata miradi upande wa barabara, tumejenga madaraja ambayo yalikuwa yanasumbua kwa kipindi cha miaka mingi. Vilevile tumepata madarasa mengi kama ambavyo Wabunge wengine wamepata, na hivi karibuni tumepata shilingi zaidi ya bilioni 735 kwa ajili ya upanuzi wa shule yetu ya wasichana pale Mpwapwa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapanua shule yetu ya wavulana Mpwapwa Sekondari, tumepata milioni 295, tumeendelea, tumepata vituo vya afya. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya juhudi hizi ambazo amezifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimpongeze sana Waziri wa Fedha. Bajeti hii amegusa karibu maeneo mengi sana yanayohusu wananchi, nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na timu yake nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na bajeti nzuri kama hii mimi naona ni jambo moja lakini utekelezaji wake ni jambo lingine. Ninataka kumshauri Waziri waitekeleze katika mapana yake kama ambavyo wameileta. Haya mengine tuliokuwa na shida kwamba bajeti inakuwa nzuri lakini utekelezaji wake unakuwa haufikii malengo ambayo yale tulikuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuchangia upande wa ukusanyaji wa kodi kupitia *ETS* au *Electronic Tax Stamps.* Utaratibu huu mimi nauunga mkono sana uendelee kutumika kama ambavyo umekuwa ukitumika kwa kuwa unatusaidia kuongeza mapato, stamp hizi zinabandikwa kwenye bidhaa zinazozalishwa. Kwa hiyo kwanza tutajua ni bidhaa kiasi gani zilizozalishwa na inakuwa rahisi sasa kukata kodi. Ingawa kuna malalamiko machache yanaendelea dhidi ya mkandarasi anayetekeleza mradi huu. Naishauri Serikali mkae na huyu mkandarasi muweze ku-*resolve* matatizo yote ambayo yameonekana katika utekelezaji wake lakini utaratibu huu nauunga mkono ningeshauri Serikali iendelee naoi li kuongeza mapato ya Serikali yetu hivyo kufadhili miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni upande wa kilimo. Kilimo kama walivyosema wengine ndio uti wa mgongo, na tunajua kabisa zaidi ya asilimia 65 ya ajira za nchi hii zinapatikana kutokana na kilimo. Nimeona Wizara ya Kilimo; niwapongeze sana; wamekuja na mkakati wa kuhakikisha kwamba sasa tunaondokana na kilimo cha kutegemea sasa tutakuwa tunafanya kilimo cha umwagiliaji. Mabwawa yanajengwa sehemu nyingi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishukuru kwa sababu kule Mpwapwa tuna bwawa kubwa lenye thamani ya shilingi bilioni 27.9 ni bwawa kubwa ambalo naamini litaleta ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Mpwapwa. Sasa kitu ambacho ningeomba Serikali izingatie sana hapa ni kutengeneza miundimbinu tunaweza kuwa na maji mengi sana lakini kama miundombinu ya umwagiliaji haipo bado tutaendelea kukutana na shida nyingi za uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo hicho niwapongeze sana ile mamlaka ya kuhifadhi chakula *NFRA* mwaka huu kulikuwa na shida ya chakula katika maeneo mengi katika nchi yetu ni pamoja na Jimbo langu la Mpwapwa. Walifanya vizuri sana kutusaidia. Wakati wanaanza kusambaza chakula bei ya debe moja la mahindi ilikuwa imefikia shilingi 25,000 lakini wao walipoleta mahindi yakaanza kuuzwa kwa shilingi 16,000. Ulikuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi lakini shida ambayo niliiona ni kwamba hawakuwa na uwezo wa kufika maeneo yote ya Wilaya ya Mpwapwa kwa sababu ya nguvu ndogo ya bajeti ama idadi ndogo ya wafanyakazi. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali izingatie hili jambo iwaongezee nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umesema mna mpango wa kununua tani 400,000. Mimi nadhani hizo tani ni ndogo kwa sababu ya uhaba wa mvua iliyotokea mwaka huu bado tunafikiria kwamba kutakuwa na shida ya chakula mwaka unaokuja. Kwa hiyo hawa watu wawezeshwe wawe na chakula cha kutosha. Zinunuliwe hata tani 700,000 ili ikiwezekana basi shida hii ya chakula itakapotokea Serikali iwe na uwezo wa kupambana na hii shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwa upande wa ardhi. Ardhi ni jambo moja kubwa sana ambalo linaleta maendeleo kwa watu wetu. Serikali mmezungumza habari ya kupunguza kodi na tozo mbalimbali kwa wamiliki wa ardhi na mimi naungana nao hilo jambo ni zuri ili watu wengi waweze ku-*afford* kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo bado hatujafanya vizuri kwa upande wetu wa Serikali ni kupima ardhi kwenye miji ya wilaya na miji ambayo inakuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akipimiwa ardhi yake akawa na hati ya kumiliki ardhi kwanza faida yake ni kwamba miji itajengwa kulingana na mipango miji. Kwa hiyo upimaji wa ardhi kwa kawaida unapendezesha miji, miji inaonekana imejengwa vizuri. Faida ya pili yule mwenye kumiliki ardhi ambaye ana hati ya kumiliki ardhi anaweza kuwa na *access* ya kupata mikopo kwenye vyombo vyetu vya fedha, na akishapata mikopo itamsaidia kujitafutia biashara na kufanya ujasiriamali. Kwa hiyo itakuwa ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wengi hawawezi kupata mikopo katika vyombo vya fedha kwa sababu tu hawana dhamana na dhamana kubwa ambayo inatakiwa kwenye vyombo vingi vya fedha ni umiliki wa ardhi, yaani mtu lazima uwe na hati ya ardhi. Kwa hiyo ningeomba sana maelezo yaliyoelezwa kwenye bajeti ni mazuri na namwomba Mheshimiwa Waziri jambo hili Serikali ilitilie maanani. Watu wapimiwe ardhi waweze kumilikishwa ardhi ili waweze kufanya maendeleo ya maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia nimeona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia mpango huu wa kunusuru kaya maskini *(TASAF)*. Mpango huu ni mzuri na umeleta tija katika maeneo mengi ya nchi yetu, na kwamba sasa pia waweza kutambua maeneo kama 186 ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, ambalo ni jambo zuri. Malalamiko yangu, niliwahi kusema hata huko nyuma, utaratibu wa kutambua hizo kaya maskini bado hauko sahihi. Katika Jimbo langu la Mpwapwa wako watu ambao mimi nawajua ni maskini kabisa wana sifa zote lakini hawajaingia

kwenye huu mpango wamekuwa wakilalamika. Kwa hiyo maana yake nni kwamba kuna kasoro katika utaratibu mzima wa kutambua nani ana sifa, kaya ipi ina sifa ya kuingia kwenye huo mpango na ipi haina sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii imefanywa na watendaji wachache wasio waaminifu wamekwenda wamechukua watu wasio na sifa kuingia kwenye huu mpango wamewaingiza wameacha watu ambao kwa kweli wana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imefanywa na watendaji wachache wasio waaminifu, wamekwenda wamechukua watu wasio na sifa, wamewaingiza kwenye huu mpango, wamewaacha watu ambao kwa kweli wana sifa. Kwa hiyo Serikali ningeomba pia tunapotekeleza bajeti hii ya 2023/2024, Mpango huu wa *TASAF* ni mpango mzuri, kama hatuwezi kuusimamia vizuri tutanufaisha watu ambao hawastahili, tutaacha wale wanaostahili. Matokeo yake, lengo na madhumuni ya mpango huu yatakuwa hayajatimia kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia ningependa nichangie ni kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia nadhani amevunja rekodi ya kutoa fedha nyingi sana kuliko wakati mwingine wowote ambazo zimeenda katika ngazi zote za Serikali. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini lengo lake na madhumuni yake bila shaka angetarajia kuona ustawi wa wananchi wake, angetarajia kuona yale ambayo tumekusudia, yale ambayo yeye mwenyewe anawaza mpaka anapeleka hizo fedha yanatokea katika uhalisia wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii miradi mingi ambayo Mheshimiwa Rais ameipeleka katika maeneo yote ama haijakamilika ama imekamilika, lakini iko chini ya kiwango, kama ni majengo hayana ubora, ni kwa sababu ya usimamizi hafifu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kama msimamizi wa bajeti, Waziri wa Fedha, fedha hizi anapozipeleka kwenye maeneo mbalimbali kuwe na mpango mahususi wa kusimamia fedha hizi. Maeneo mengi fedha hizi zinachezewa vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ujenzi wa madarasa, unakuta hayako kwenye kiwango. Fedha ile ambayo wengine wanakamilisha kabisa kwa kiwango bora, lakini wengine hawakamilishi kabisa. Vituo vya afya, ukifuatilia utakuta vingine havijakamilika kabisa, fedha ni ile ile ambayo wengine wamekamilisha. Hii ni kwa sababu ya usimamizi mbovu. Haitakuwa na maana yoyote kama Mheshimiwa Rais atatafuta fedha, ataleta katika maeneo ya wananchi akitarajia kujenga hospitali, kujenga zahanati, kujenga shule imara na bora, halafu yote hayo yasitokee. Pia wananchi wanatarajia sana kuona kwamba mambo yao yanaenda vizuri, kama ni miradi inaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tusimamie fedha za Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima, ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, wakati huo Mheshimiwa Cosato Chumi anajiandaa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2023/2024 ambao imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri kaka yangu Dkt Mwigulu Lameck Nchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujalia uzima na kukutana asubuhi ya leo. Pili, kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki nasema hivi wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki walionipigia kura nyingi sana natamka hadharani kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika muda wa miaka

miwili. Kazi kubwa aliyoifanya katika uongozi wake kudumisha demokrasia nchini, kuweka uwazi wa Serikali, diplomasia na kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo leo tunajivua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya na vijana siku hizi wanasema Mheshimiwa Rais anastahili kupewa maua yake ya kutosha kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa hakika wale wenye nia njema hawatakuwa na kusita kumpa maua yake, tumpe maua mengi Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea tabia ambayo nataka ienee katika nchi yetu, eti kwamba tusipongezane kwa mambo mazuri yanayofanyika, wengi wamefika mahali wanasema ukimpongeza unakuwa wewe ni chawa. Hata kwenye Biblia imeandikwa kwamba: "*moyo usiyo na shukurani hukausha mema yote*" Kwa hiyo Watanzania tusijengewe, kwa sababu tu humpendi Fulani, kafanya jambo zuri, mpongeze afanye kazi zaidi. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais anapofanya kazi nzuri, uungwana wa kawaida unatakiwa umpongeze kwa sababu anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo letu la Singida Mashariki, Wilaya ya Ikungi katika muda huu tunaoenda kumaliza bajeti ambayo tumeletewa, fedha tulizoletewa za kutekeleza miradi ni zaidi ya bilioni saba zimeshuka katika wilaya yetu. Kwa hiyo maana yake ni kwamba fedha nyingi zimeshuka kutekeleza miradi, si kwamba tunatarajia fedha zimekuja na hivi tunavyoongea miradi lukuki imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajivunia sana uongozi wa Mheshimiwa Rais, tunajivunia kiongozi wetu anavyofanya vizuri. Sisi wananchi kuna maeneo yalikuwa hamna madarasa, leo madarasa yapo, kulikuwa hamna vituo vya afya, kuna vituo vya afya, kulikuwa barabara zimejifunga, barabara zimefunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika Wilaya yetu ya Ikungi tulikuwa hatujawahi kuwa na lami, sasa lami inawekwa, tulikuwa hatuna taa za barabarani, tulikuwa gizani usiku, tunalala

mapema, leo taa za barabarani zinawekwa. Tutakuwa watu wa ajabu kabisa bila kumpongeza Mheshimiwa Rais na kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri. Mzee Mkapa alisema kushukuru ni kuomba tena, tunaamini tunaposhukuru tunamwomba tena Mheshimiwa Rais atuletee fedha tuweze kuleta maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa ndugu yangu Peter Serukamba kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za maendeleo, nampongeza sana *DC* wa Ikungi ndugu yangu Thomas Apson kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo na nampongeza Mkurugenzi wetu Justice Kijazi kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo. Hivi tunavyoongea tumepata hati safi kwa sababu ya usimamizi mzuri unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naomba nichangie maeneo mawili makubwa ambayo yatasaidia katika kutoa ushauri kwenye bajeti yetu tunayoenda kuipitisha. La kwanza ni sekta ya uzalishaji, lakini pia nitaongelea ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Katika maeneo haya mawili nitaomba niende haraka kwa sababu yamejaa mambo muhimu kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni sekta ya uchumi, ambayo ni sekta ya uzalishaji upande wa kilimo. Kilimo kimeongezewa fedha katika mwaka huu wa fedha. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, tumpongeze Waziri wa Fedha, tuwapongeze kwa kuleta fedha nyingi katika kutupitisha zikatekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nitakuwa *specific* kwenye eneo la kilimo cha alizeti, kwa maana ya mafuta ya kula. Tulikuwa tukilalamika hapa nchi yetu ina upungufu wa mafuta ya kula mpaka tukalazimika kwenda kuagiza nje ya nchi. Tumekuwa tukitumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kununua mafuta nje ya nchi. Ukaja mkakati kupitia Wizara ya Kilimo, tuzalishe alizeti ya kutosha, wakaleta mbegu, wananchi wakawezeshwa, leo tunavyoongea wananchi wamevuna vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongea bei ya debe la alizeti limeshuka, wananchi wangu wanalalamika. Wanaomba Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba ili ile alizeti yao inawapa faida. Kwa hiyo nataka nimwombe sana Waziri ahakikishe kwamba tunasaidia zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hapa kwenye eneo na namna ambavyo tunapunguza kodi katika *refined* mafuta kwa asilimia 25 badala ya 35 ambayo tunadhani ingekuwepo. Niombe sana kwenye *semi refined* tunayo asilimia 10, lakini kwenye *crude oil* tunayo asilimia sifuri ili kusaidia viwanda vya ndani. Niombe sana kama tunataka kuendana na mpango mzuri wa Wizara ya Kilimo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha turudishe asilimia 35 kwenye *refined* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hivi kutasaidia kupunguza mazao yanayotoka nje kwa maana ya bidhaa ya nje isiingie humu ndani ili tuweze kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha na tumsaidie mkulima aliyoko pale kijijini. Hiyo ndiyo itakuwa na maana kubwa kwa uwekezaji wa kilimo cha alizeti ambacho tunasema, pia itaongeza mafuta mazuri ya alizeti katika nchi yetu ambayo nje ya nchi wanayahitaji, maana yake tutauza mpaka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe ili kumkomboa mkulima na kwenda na kauli moja, kwa maana ya lugha ya pamoja, tunaomba sana tupandishe kuwa asilimia 35 badala ya 25 ambayo tunaipendekeza ambayo kiukweli itaenda kuua soko, itaenda kuua kilimo cha mwananchi wetu wa kawaida kitu ambacho siyo lengo la Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana hilo na Wabunge wengi wameshauri, naomba sana hili lichukuliwe na namwomba Waziri anapokuja kuhitimisha aje atuhakikishie hilo, wananchi wanasubiri huko nje, wanatuambia tusaidieni, tuokoeni tuweze kupata faida ya kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni suala la ununuzi wa ndege ya *cargo* ambayo tumeipokea juzi na Mheshimiwa Rais

ametuongeza, tunapongeza sana. Maana yake ni kwamba leo tunakuwa na uwezo wa ku–*export* moja kwa moja mazao ya mbogamboga mpaka na mazao ya matunda ikiwepo parachichi ambayo inatakiwa sana duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili tumekuwa na mpango mzuri wa mazao ya mbogamboga *horticulture* katika maeneo yetu. Wizara ya Kilimo ina mpango mzuri kwa upande wa *horticulture*. Tunaomba sana sana kumekuwa na changamoto ya vifaa vya kuhifadhia mbogamboga pamoja na matunda. Tumekuwa na hizi *cold rooms* kwa maana ya *tracks* hizi ambazo zinasafirisha mazao yetu ili yasiharibike, lakini tumekuwa pia na *cold rooms equipment's* ambazo zinatakiwa katika maeneo ya mashamba ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali na Mheshimiwa Waziri aje na mpango wa kuondoa angalau ushuru au kodi ili kuingiza vile vifaa ambavyo vinaenda ku–*support* kilimo cha mbogamboga katika maeneo yetu kwa sababu vile vifaa ni vya gharama kubwa. Wananchi wengi hawawezi wenye mashamba ambao wamejitahidi kuingia kwenye jambo hili na ili wawekezaji ambao wameamua ku–*support* na ile ndege ili ipate mzigo mkubwa wa kupeleka nje ya nchi, tuweze kuuza na kupata fedha za kigeni ili fedha za kigeni zije zisaidie hapa nchini, niombe sana Mheshimiwa Waziri afanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri akiweza kufanya hivyo atasaidia kilimo cha wananchi wetu ambao wameamua kujiwekeza kwenye eneo hili, lakini hii ndege ambayo tumeinunua itakuwa na maana kubwa ya kuhakikisha tunasafirisha mzigo kwa maana ya mzigo mkubwa kwenda nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni suala la ushirikishwaji wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na naomba niseme wazi, nimekuwa nikiongea mara tatu hapa katika suala la bandari kwa muda mwingi sana. Niombe sana, eneo hili la bandari, bandari ndiyo kioo chetu. Kumekuwa na kauli mbalimbali na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu jana ametoa kauli nzuri sana kuhusiana na bandari, mawazo tutaendelea kuyachukua, hatutarudi nyuma

tunataka tuwekeze ili tuongeze pato la Taifa, kusiwe na upotoshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili kuna makundi manne ambayo yanatukwamisha. Kundi la kwanza ni suala la wapinzani wetu kutaka kutuzuia tusiendelee. La pili, ni wafanyabiashara wasio waaminifu wameingilia mchakato huu ili wao waendelee kufaidika na udhaifu wa bandari yetu. Watu wa tatu ni baadhi ya wafanyakazi wa *TPA* na wa *TRA* wanaofaidika na mfumo huu mbaya wa kuendesha bandari yetu na watu wa nne ni bandari shindani zilizoko katika ukanda huu ambazo hazipendi sisi tufanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao *DP World* ni wana uwezo mkubwa sana. Niombe sana tuendelee kuwaza kwamba nchi hii haitauza bandari, bandari ni ya Watanzania, Mheshimiwa Rais ameshasema tuondelee hofu kwa sababu hatuna sababu ya kuogopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hofu hii ipo niongee hili neno dogo tu. Tulikuwa na stendi yetu pale Mnazi mmoja Kisutu, stendi ya Wananchi wa Dar es salaam waliandamana kwa sababu inapelekwa Ubungo wakasema ni mbali sana, wakaenda, tukaenda kujenga stendi Ubungo, leo Ubungo imeonekana ni mjini katikati, lakini leo tunavyoongea stendi iko wapi? Iko Mbezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waondoe hofu nia yetu ni njema twende kuiunga mkono Serikali ili iongeze mapato kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja ili iweze kupitisha bajeti hii ikalete maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu. Nilimwita Mheshimiwa Cosato David Chumi, wakati huo

wafuatao wanajiandaa, Mheshimiwa Kavejuru Felix na Mheshimiwa Noah Lembrus Saputu Mollel.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kutoa mawazo yangu katika siku ya leo tunapochangia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza napenda kabisa kwanza kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake. Pongezi hizi nazitoa kwa niaba ya wananchi ya Mafinga, kwa niaba ya wananchi wa Mufindi Kusini ambao wewe umekalia hicho kiti na kwa niaba ya wananchi wa Mufindi Kaskazini kwa kaka yetu Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini natoa pongezi hizi? Nampongeza Mheshishimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yake kwanza kwa ule mpango wa *EPC+F,* watu wengi walikuwa na mashaka kwamba unaweza mpango ule usije ukawa ni kitu cha kikweli kweli, lakini wiki iliyopita tumeshuhudia kusainiwa kwa Mikataba na ujenzi wa Barabara ya Mafinga Mgololo kilomita 81 unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa sababu pia jana wameweka saini mkataba wa Barabara ya kutoka Mtiri kwenda Ifwagi mpaka maeneo ya Mkuta kilomita 14 ambako ni Jimbo la Mufindi Kaskazini, lakini wakati huo huo Nyororo–Mtwango ambako ni kwako wewe Mwenyekiti wameshaanza. Hapa naomba niweke na kaombi kidogo pamoja na kuwa umesema tuki–*address* kiti hapa naki–*address* kiti na naomba pia nim–*address* na Waziri wa Fedha. Tunaomba pale Nyororo – Mtwango tumeshaanza, lakini kwa sababu tunafanya kwa fedha za ndani, tunaomba Serikali itupie jicho, ipeleke fedha ili ujenzi wa ile barabara uende kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, katika hiyo Wilaya ya Mufindi ambao ni tajiri wa mazao ya misitu, maana tumezungumza hapa kuhusu vitongoji 15 kila jimbo kupatiwa umeme, nguzo zitatoka kule. Kwa hiyo itaimarisha miundombinu kutoka Sawala – Iyegeya mpaka Lulanda, jumla kilomita 40.7.

Nafahamu ziko zile thelathini na ngapi na zile kumi ambazo tumeongezewa. Kwa hiyo haya yote mimi binafsi kama nimetoka Mafinga na Mufindi ambako Mheshimiwa Mwenyekiti wewe ni shahidi, sisi kama Wabunge watatu tumesimangwa sana, tumesemwa sana, lakini wananchi walikuwa hawajui, yako mengine tunaweza tukayasema hadharani lakini mengine tunayaficha chini ya meza, hatimaye yamekuwa, barabara zinaanza kujengwa. Kwa hiyo naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi *specific* kwa Wanamufindi, nakuja na pongezi kama mbili, maana pongezi ni nyingi. La kwanza, ni hili la kuondoa ada kwa watoto wetu watakaokwenda kwenye Vyuo vya Ufundi, *DIT,* Dar *Tech* na ile zamani tulikuwa tunaita Mbeya *Tech* siku hizi inaitwa *MUST*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mikubwa ya umeme, tuna Mradi wa *SGR* yote hii itahitaji mafundi wa kuihudumia kama sehemu ya *maintenance*. Kwa hiyo wazo hili ambalo Mheshimiwa Rais amelileta ni jambo jema, kwa sababu tutapata watoto wetu ambao watakuwa na ujuzi, watahudumia miundombinu ya reli yetu, lakini pia na miundombinu itakayotokana na umeme tutakaozalisha kwenye bwawa wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasilishe ombi na ushauri kwa Serikali kwa maana ya Waziri wa Fedha. Naomba sisi tunaotoka kwenye mazao ya misitu, ukienda kwenye msamaha wa *VAT* sana sana unapata kwenye vitendea kazi kama vile matrekta ya kuvuta magogo kutoka shambani kupeleka *site* au kupeleka barabarani. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, ili tuwe na *connectivity,* baada ya kuwa tumetoa ada kwenye hivi Vyuo vya Ufundi, tutoe pia *VAT* kwenye *equipment* hasa hasa za mazao ya misitu ili hawa watoto tukishawasomesha wawe na mahali pa kuanzia. Kwa hiyo hili ni jambo muhimu sana katika ku–*add value*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napongeza ni ambalo linaenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Mheshimiwa Nape. Mara nyingi tunalalamika kuhusu mambo haya ya *bundle*

na kadhalika, napongeza kwa sababu Mheshimiwa Waziri Nape na Serikali kwa ujumla wamekuwa wasikivu na wananchi wengi wanaweza wakawa hawajui, ile kupitisha miundombinu kwa ajili ya masuala ya mawasiliano ilikuwa kwa kilomita moja ukipitisha labda kwenye barabara za *TARURA* au za *TANROAD* kwa kilomita moja walikuwa wanatozwa dola 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limesemwa sana na mimi nilichangia kwenye Mpango na Serikali imekuwa Sikivu, sasa imepungua kutoka dola 1,000 ile kupata *leeway* mpaka dola 200 na ile *annual fee* imetoka 1,000 mpaka 100. Kwa hiyo matarajio yetu kwamba punguzo hili linaenda kuchochea uchumi wa kidigitali. Kwa hiyo, hili hapa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zinaweza zikawa nyingi, lingine ni hili la kuwa na dirisha la kutoa huduma kwa wawekezaji. Napongeza kwamba kutakuwa na mfumo wa pamoja ambapo Taasisi kama *NEMC, OSHA, BRELLA, TRA, TBS* na kadhalika, zitakuwa zinapata kwa pamoja. Hapa napo nitoe angalizo, unakuta mfanyabiashara au mwekezaji amejaza kila kitu, litakapofika suala la *control number, that's a big problem,* mara mtandao uko chini, mara njoo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba Serikali wakiongozwa na Wizara ya Mawasiliano ya Mheshimiwa Nape, hebu turahisishe maana yake yale ni mapato. Mtu ameshajaza kila kitu siku tatu kupata *control number,* anaambiwa mtandao sijui uko chini, mtandao uko taratibu, mtandao sijui umesimama. Naomba kama tunafanya huu muunganisho wa mifumo tuendane pia na kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kuwezesha sasa huu uchumi wa kidijitali uende vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili suala ambalo kwenye ukurasa nadhani wa 50 hadi 51, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ningeomba Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, naona unazungumzishwa hapo hili unisikilize vizuri sana pamoja na kwamba Mwenyekiti umesema tuelekeze kwako. Kwenye suala hili la kukosekana au kuwa na upungufu wa dola, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema jitihada tunazofanya mojawapo ni

kuhakikisha tunazalisha, tuuze nje kuliko kuagiza, sasa hapa nakuja wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuamue suala moja, tunaamua kuwa Taifa la wazalishaji au Taifa la wachuuzi, mimi Cosato Chumi na wanamafinga sisi tunataka tuwe Taifa la wazalishaji na hayo ndiyo maono ya Mheshimiwa Rais na ndiyo maana tukapewa ruzuku ya mbolea, ndiyo maana tunapewa ruzuku kwenye mbegu. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu kwenye suala la mafuta na mimi hili nasema na sitoacha niliseme mpaka litokee, hebu Mheshimiwa Waziri tuende na mfumo wa kwenye sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari viwanda vilikata tamaa kuwekaza kwa sababu tulikuwa tunatoa vibali hovyo hovyo sukari inakuwa *flooded* hapa lakini baada ya kudhibiti na kuweka utaratibu mzuri tunaona uwekezaji na upanuzi kwenye viwanda vya sukari umeongozeka na sasa hivi *deficit* ni kama tani 15,000. Kwa hiyo, naomba kwenye ngano na mafuta ya kula na watu wa Serikali kuna mahali wanataka kutuchonganisha Wabunge na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikiliza juzi Mheshimiwa Waziri vizuri sana kwamba basi tutapandisha, kana kwamba huo ushuru wa asilimia 35 kana kwamba ukipandishwa bei itakuwa kubwa, hata ulipopungua, ulipokuwa *zero rated* Waheshimiwa Wabunge, bei ya mafuta ya kula haikupungua huo ndiyo ukweli, mlaji wa mwisho hakunufaika, yamenufaika ma–*tycoon* lazima tuseme ukweli. Bei ya mafuta imepata ahueni kidogo juzi baada ya kuanza kuvuna alizeti. Kwa hiyo, naomba na wataalam wake Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili la Kamati naunga mkono mapendekezo ya Kamati kwa ujumla imeenda vizuri, isipokuwa kwenye suala la *cement* ile shilingi 20 ambayo ni sawa na mfuko 1,000 Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais ameshiriki mikutano sasa mfululizo mara mbili, ule wa dunia wa mabadiliko ya tabianchi, kuna fedha nyingi kwenye mifuko ya mabadiliko ya tabianchi, na kuna mahali Kamati imempongeza Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kuliko tutwishane mzigo Watanzania bado ziko fedha nyingi. Mheshimiwa Kakoso amesema hapa jana, hii

biashara tu ya hewa ya ukaa kama sisi tunaotoka Mufindi, Iringa, Njombe Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaweza ku *subsidize* kuliko kumtwisha mwananchi hii shilingi 20 sawa na 1,000 kwa mfuko wa *cement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kutoka mwisho, nina barua umoja wa wastaafu Halmashauri ya Mji wa Mafinga wanaomba ile pensheni ya iongezwe. Mapendekezo yao wanasema lile dirisha kwamba wazee kwanza wanapokwenda kupata afya, hapana tuwe na dirisha lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo la mwisho kwa Mheshimiwa Bashe, nimekutumia meseji kuhusu mahindi. Mimi naomba niwatoe wasiwasi Serikali, mmesema tu – *apply* na asubuhi umesema watu wana – *apply* lakini mtandano uko chini. Hii dhana kwamba eti wakulima tutauza hadi tusahau kujiwekea chakula siyo kweli. Sisi tuna akili timamu kwa miaka yote. Kwa hiyo, ni mambo mawili, ama mrahisishe upatikanaji wa vibali kwenye huo mfumo wenu tuuze nje, pili kama hamuwezi *NFRA* nunueni kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Mungu Ibariki Mafinga, Mungu Ibariki Mufindi, Mungu bariki viongozi wetu, mmbariki sana Mama Samia Suluhu Hassan. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo hapa. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge niwatangaze.

Wapo wageni kumi wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma - Mbunge ambaye ni Naibu Waziri, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni viongozi wa UWAMAKIZI na Madiwani kutoka Muheza Mkoa wa Tanga, ahsante. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni mwingine wa Mheshimiwa Hamis Mwinjuma ambaye ni Ndugu Athuman Ramadhan ni dereva aliyewahi kufanya kazi na viongozi mbalimbali akiwemo Hayati Dkt. John Magufuli, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Anthony Dialo na viongozi wengine qaandamizi ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni watumishi wa Taasisi ya *Vuka Initiative* kutoka Jijini Arusha, wako wapi? Wawili wale pale, ahsante. *(Makofi)*

Wapo wageni 20 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni wafanyakazi wa *Dodoma FM* na *TV* kutoka Dodoma Mjini, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Daniel Awack kutoka Karatu Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, amabo ni viongozi 60 wa Taasisi Isiyo ya Kiserikali kutoka Taasisi ya *Young CEOs Round Table Africa* kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na Ndugu Zakayo Shushu, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji nilimuita Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, wakati huo wafuatao wanajiandaa na hawa ndiyo watakuwa wachangiaji kwa leo; kwanza ni Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi pamoja na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye hii Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kwa niaba ya wananchi wa Buhigwe na wananchi wa Mkoa wote wa Kigoma nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya kwa kufungua Mkoa wetu akishauriwa na Makamu wa Rais Dkt. Philip Isdory Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana Mkoa wetu wa Kigoma umeendelea kufunguliwa katika Awamu hii ya Sita kupitia

miundombinu ya Barabara, sasa Mkoa wa Kigoma tunaenda kuunganishwa rasmi na Mkoa wa Tabora. Tunayo barabara ambayo Mheshimiwa Rais ametoa fedha kulikuwa kumebakia na kipande kidogo cha kutoka Kazilambwa mpaka Magu mpaka Chabu pale Nguruka kilometa 36 Mkandarasi yuko *site*. Kulikuwa tumebakia kipande cha kilometa 51.1 cha kutoka Malagarasi hadi Uvinza Mkandarasi yuko *site* tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaenda sasa kuunganishwa na Mkoa wa Kagera kuanzia Kakonko kuja Kibondo sasa ni lami, tuna kipande kingine ambacho sasa ni cha Mvugwe – Nduta kilometa 59 Mkandarasi yuko *site,* tuna Mvugwe – Kanyani kilometa 70.5 Mkandarasi yuko *site,* na tuna Kasulu Manyovu kilometa 68 Mkandarasi yuko *site*, tunashukuru sana. Miradi hii inaenda kugharimu zaidi ya bilioni 560 katika mradi huu mkuu wa kutuunganisha na Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na barabara hii ndani yake kulikuwa na miradi ya bakshishi inaitwa *complimentary projects*. Miradi hii ilitakiwa kwa kadri inavyotekelezwa tuliomba na inatakiwa kwenye mujibu wa mkataba na inatakiwa miradi ile ambayo ni bakshishi ya mradi huu nayo iwe imetekelezwa. Ndani ya hizi bilioni zaidi ya 560 zipo bilioni 23 kwa ajili ya kutengeneza shule ya Sekondari ya kisasa Buhigwe. Tunaomba Serikali sasa iandae utaratibu ili hii miradi ambayo ni *complimentary projects* ya mradi huu mama nayo ianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ujenzi wa kituo cha mabasi kule Manyovu na ujenzi wa kituo cha forodha tuongeomba navyo utekelezaji wake uende sambamba. Upo ujenzi wa kituo cha afya Makere nao tungeomba ujenzi huo uanze mara moja. Pia upo ukarabati wa stendi ya Kibondo pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Kibondo, tungeomba navyo viende sambamba. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais, sambamba na hilo tunamshukuru na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, endeleeni kutoa fedha kwenye miradi inayounganisha na inayoenda kuufungua Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushukuru ni kuomba, tunaomba tena sisi tupo mpakani mwa Burundi na Congo, bado tunazo barabara muhimu ambazo hizo zikitengenezwa kwa kiwango cha lami zitaleta tija, zitaongeza mapato katika nchi yetu lakini zitachagamsha biashara kati ya nchi ya Tanzania na Burundi na Congo. Barabara hizi nazo zimekwishafanyiwa usanifu ningeomba kwenye bajeti hii ya 2023/2024 nazo zitengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ni ya Kalela – Muzenze – Janda kilometa 57 na barabara ya Buhigwe – Muyama – Kilelema – Kitundu kilometa 120 na barabara ya Kakonko – Muhange kilomita 38. Hizo barabara zote zinakwenda kutuunganisha na nchi ya Burundi na Congo ambapo sasa tunaenda kufanya bishara nao. Tukifanya nao biashara, kama Kigoma itafanywa kuwa Mkoa wa kiuchumi, ikafanyika kuwa ndiyo *hub* ya uchumi, Tunaamini nchi hii itaenda kukuza uchumi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo ombi lingine ambalo ni malalmiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara. Wafanyabiashara wana mangung'uniko wana malalamiko kwenye mfumo wa *ETS,* ningeomba sana Serikali pamoja na Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ya *ETS* pamoja na wafanyabiashara, wakae pamoja waangalie namna gani ambavyo wanaweza wakaondoa malalamiko au minong'ono au manung'uniko ya wafanyabiashara ili bei iweze kushushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuchangia tena kuhusu kilimo. Sisi kwenye Jimbo letu la Buhigwe tuna kituo cha *TaCRI* ambacho kinazalisha mbegu na miche bora ya kahawa. Kwa mwaka 2022/2023 tumeona zao la kahawa ndiyo zao ambalo limeongoza kuipatia nchi zaidi ya bilioni 248 fedha ya kigeni. Ninaishauri Serikali ili iweze kupata fedha nyingi za kigeni ni lazima kuwepo na mkakati wa dhati wa kuhakikisha maeneo na mashamba yanayolimwa kahawa yanaongezeka, pia kuwepo na kusudi madhubuti kabisa la Serikali kusaidia Wizara ya Kilimo, iweze kuzalisha miche ya kahawa kutoka milioni 20 ambayo inazalishwa sasa ifike zaidi ya milioni 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia wenzetu wa Uganda kwa mwaka wanazalisha miche milioni 161, ukenda Ethiopia wanzalisha miche zaidi ya milioni 360. Kwa nini sisi ambao tuna eneo kubwa kabisa linalofaa kwa kulima kahawa, zaidi ya Mikoa 16 sasa hivi inalima kahawa, kwa nini tuzalishe miche 20,000 kwa mwaka? Haitoshi! Hili zao lenyewe ndiyo linalotuingizia fedha nyingi za kigeni, ningeomba muangalie wakulima wa zao la kahawa, mtafute namna gani ambavyo mnaweza Serikali ikaongeza nguvu pale miche iongezeke na ikiwezekana zao hili la kimkakati nalo liangaliwe ni namna gani ambavyo hawa wakulima wanaweza kupewa ruzuku, kwa sababu ni sehemu ambayo Serikali inapata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili niende kwenye biashara. Mkoa wetu wa Kigoma umepakana na nchi ya *DR* Congo, Burundi na Zambia. Katika Ziwa letu Tanganyika, bado hatujapata meli. Meli zote zilisimama, tunahitaji meli ili biashara zilizokuwa zikifanyika siku za nyuma kwenda Zambia kwenda Moba, kwenda Kalemi, kwenda Ubwari, kwenda Uvira, kwenda Goma kwenda Gbadolite. Palikuwa pamechangamka na Mkoa ulikuwa umechangamka zirudi. Tunaomba bajeti hii ambayo imeelekeza na imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya nazo zitengenezwe ili kupunguza changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kavejuru Felix. Nilisema atachangia Mheshimiwa Iddi Kassim lakini ameshachangia kwa hiyo tutaomtoa kwenye orodha. Hivyo mchangiaji anayefuata atakuwa ni Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, akifuatiwa na Mheshimiwa Kamguna na baadaye Mheshimiwa Swalle.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii muhimu ya mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametupa uzima

kuwepo katika ukumbi huu siku ya leo, kuendelea kujadili bajeti ya Taifa letu kwa maana ya hatma ya wananchi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa akijishughulisha kwa hali na mali kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma mbalimbali katika afya, elimu, barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu, kwa kazi nzuri na njema ambayo ameendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais, Naibu wake pamoja na Wizara nzima Watumishi wa Wizara ya Fedha ambao wanahakikisha kwamba anafanya kazi nzuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba huduma inapatikana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo kwenye bajeti hii amehakikisha kwanza watoto wanaokwenda katika vyuo vya kati sasa wanakwenda kusoma kwa kupata mikopo. Hii ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwetu Wabunge kwa sababu kila mtoto analia kwamba tunaomba ada. Mheshimiwa Mbunge naomba ada, kwa hiyo hii kwa kweli tunampongeza Mheshimiwa Rais, tunakupongeza na Mheshimiwa Mwigulu kwa sababu mmefikiria jambo la msingi sana kwa Watanzania ambao wana familia maskini. Pia mmeenda kuondoa ada kabisa kwenye vyuo vingine hivi vya *technical,* kwa kweli mmefanya jambo la maana na jambo la muhimu kwa Watanzania na mnapaswa kushukuriwa, Mheshimiwa Rais anapaswa kushukuriwa na Mheshimiwa Mwigulu na timu yako nzima mnapaswa kushukuriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha huu utaenda kuondoa vilio vya Watanzania walio wengi ambao hawakuwa na uwezo kwa ajili ya kupata elimu ya vyuo vikuu hasa vyuo vya kati na itaenda sasa kuleta faraja katika familia ambazo walikuwa wanafikiri kusoma haiwezekani, leo watakwenda kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba basi bajeti hii itakapoanza kutekelezwa katika kipengele hiki cha kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi hawa, tuweke utaratibu ambao hatutasikia tena kwamba huyu kapata, huyu kakosa maadam tu ana vigezo na amekidhi vigezo vyote na amechaguliwa kwenda kwenye chuo husika. Basi ile azma ya Rais wetu na Serikali yetu chini ya Mama Samia Suluhu Hassan ikaendelee kutimia na wananchi waendelee kufurahia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niingie kwenye suala la miundombinu. Kama tunavyojua *TARURA* tumeiongezea fedha. Mimi kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi hivi karibuni kama alivyoeleza huko awali, nimekubwa na mafuriko makubwa sana ambayo yameharibu miundombinu ya barabara, imeharibu madaraja na hata kupelekea kabisa wananchi hawawezi kwenda hospitalini hawawezi kupata huduma za jamii, kwa sababu hali siyo nzuri kwa miundombinu kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu tumeomba fedha za dharura kwa madaraja kama manne. Daraja la Sekei kwa maana ya Kiutu - Naurei, daraja ambalo tumepata zaidi ya milioni 400 kwa fedha za dharura, daraja la Loning'o - Ilboru kwenda Kiranyi tumepata milioni 200 karibu na 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna madaraja matatu sasa ambayo wananchi hawapiti kabisa. Daraja la *TPRI* - Likamba kwenda Musa kwenda kutokea Jeshini Monduli. Kwa kweli hali siyo nzuri, hilo daraja halipitiki tena, hali ni mbaya. Vile vile daraja la kwenda Hospitali ya Oturmeti, maeneo yameharibika sana kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile barabara ya Mnadani – Mwandeti, Mnadani – Mindo kwenda Hospitali hali ni mbaya. Naomba sana Mheshimiwa Mwigulu kwa kuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alishaongea na wewe, utusaidie hizo fedha za dharura kwa sababu, kwa kweli hali kule ni mbaya. Nami kurudi jimboni bila kunisaidia hilo, utakuwa umeniumiza, umewaumiza wale wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi hasa kwa upande wa huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mifumo. Katika Halmashauri zetu Tanzania kumekuwa na changamoto kubwa sana inapofika mwezi wa sita, mifumo yote inafungwa. Mifumo mwezi wa Sita haifanyi kazi, mwezi wa Saba haifanyi kazi, mpaka mwezi wa Nane. Hii nayo ni changamoto kubwa. Kwa sababu, inakwamisha utoaji wa huduma kwenye Halmashauri, inakwamisha utekelezaji wa shughuli za miradi mbalimbali, inakwama kwa sababu mifumo imefungwa. Zaidi ya hapo, mifumo hii ingesaidia wananchi kuendelea kulipa kodi ndani ya Halmashauri na pia kulipa kodi kwenye Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo Wizara ya Fedha iliangalie kwa makini na mapana namna ambavyo litaweza kupunguza kadhia hii ya wananchi kulipa kodi kwa sababu, bila kulipa kodi ina maana uchumi utakuwa umedorora kwa wananchi na Taifa. Kwa hiyo, naomba sana hili nalo liangaliwe kwa makini ili basi wananchi wasione kero katika kulipa kodi na utoaji wa huduma mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitisha bajeti hii, bajeti hii ikipitishwa tunategemea Serikali na yenyewe inahakikisha inasimamia mapato hayo, ukusanyaji na matumizi. Kila mwaka kumekuwa kukitokea taarifa ambazo *CAG* anakuja hapa anatuambia umefanyika ubadhirifu hapa, umefanyika ubadhirifu kwenye taasisi fulani, umefanyika ubadhirifu kwenye Wizara fulani, hii haipendezi. Ni kwa nini sasa Serikali isiweke mkakati? Pamoja na kwamba, kuna *mechanism* kwa maana ya vyombo mbalimbali vinavyozuia suala hili la watu kujiunga na kufanya mbinu ya kujipatia fedha zisizo halali katika miradi mbalimbali na kuanzisha masuala ya rushwa, wizi, ufisadi na mambo mengine kama hayo, kwa nini Serikali isione haja ya kuondoa jambo hili kabisa la *CAG* kuja kila mwaka na maajabu na maajabu na masikitiko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapitisha bajeti hii, lakini Serikali ina mzigo mkubwa. Mheshimiwa mwigulu ana mzigo mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba masuala haya ya rushwa na ufisadi katika miradi mbalimbali inatoweka kabisa. Tufurahie taarifa ya *CAG* inapotolewa, basi tuone *CAG* anasema

mambo madogo madogo ambayo hayaleti karaha na hayawezi kumuudhi Rais, hayawezi kumuudhi mtu yeyote na Watanzania wanafurahia Serikali yao kwa sababu, inasimamia mapato ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu hatua kuchukuliwa kwa wale ambao wanahusika. Kama kweli mtu kabainika kwa mujibu wa sheria na taratibu, basi wahusika wachukuliwe hatua. Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi mbalimbali wachukue hatua, sio mpaka wasubiri labda Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Rais ndio aongee, labda ndiyo ionekane, hapana. Kuna watu wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, kuna watu ambao wanamsaidia Waziri, kwa nini wasichukue hatua? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Noah Mollel kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna na mchangiaji wetu wa mwisho kwa *session* yetu ya asubuhi ya leo atakuwa ni Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupatia ruzuklu ya uhai. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais Samia kwa kazi anazotupambania pamoja na wafanyakazi wake wote wanaomsaidia, Mawaziri, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote tunawapongeza pamoja na Watanzania kila mmoja kwa nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia, ametufanyia mambo makubwa sana katika hii miaka yake miwili ya Awamu ya Sita. Sisi hasa watu wa Malinyi ambao

tuko pembezoni ya miji tulikuwa tunalalamika, kama mwaka juzi nililalamika sana kuhusu barabara, lakini tarehe 16 walienda kusaini mkataba huu wa *EPC + F* kwa ajili ya matengenezo ya ile Barabara. Ninaamini ile shida ya barabara ambayo tulikuwa tunaipata sasa tutaondokananayo, kwani itatuunganisha kutoka Lupilo – Malinyi – Namtumbo na hatimaye Ruvuma. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametutendea mengi. Katika awamu yake hii ameimalizia miradi ile mikubwa ya kimkakati ambapo watu wengi, Watanzania tulikuwa na wasiwasi, lakini wasiwasi ule Mheshimiwa Rais ameumaliza. Mradi wa reli ya *SGR*, Mradi wa Daraja la Busisi, Mwanza na Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo ni bwawa kubwa, tunajivunia na limetumia fedha nyingi sana. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wote tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenda kwenye hoja kwamba, katika Bwawa la Mwalimu Nyerere lile bwawa ni la mkakati katika nchi yetu ya Tanzania, lakini ni bwawa ambalo limepita kwenye Mikoa, na sehemu kubwal imepita katika Mkoa wa Morogoro. Katika ule mkoa kuna sehemu ambazo zimepitiwa. Kwa vyovyote vile, maendeleo yoyote huwa yakifika lazima kutakuwa na baadhi ya watu kuathirika. Katika kuathirika kule, wale wananchi wamekubali na wamesema kwamba bwawa liendelee kwa sababu faida yake ni kubwa kuliko hasara ambazo tumezipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia Mkoa wa Morogoro, hususan Bonde la Kilombero. Bonde la Kilombero ni bonde ambalo lile bwawa ni sehemu ambayo inapatikana maji kwenye chanzo, hasa katika Kijiji cha Ngombo. Kile Kijiji cha Ngombo kilifanyiwa tathmini mwaka 2022 mwezi wa kumi na moja mpaka mwezi wa kumi na mbili, 2022. Baada ya kufanyiwa tathmini ya nyumba, makazi, makaburi, na kadhalika, lakini Serikali tangu pale iko kimya. Wale watu hawajapata fidia. Hatujui wale watu ile fidia wataipata lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kupata fidia, naiuliza Serikali, yule mwananchi wa Ngombo ambaye anatakiwa

kuondoka; na tumekubali kuondoka, na ni wajibu wetu kuondoka kupisha lile bonde: Je, atakapoondoka, anakwenda wapi? Huko anakokwenda, ataishije? Maana hajapata fidia? Kule Ngombo kuna shule ya msingi, wale watoto wao watakapoondoka wataenda kusoma wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ituelekeze hayo kwa sababu, wale ni wakulima, sasa hivi ni kipindi cha mavuno, watu hawaambiwi chochote kwamba mnatakiwa kuondoka, lakini hawajapewa ile *timeframe*. Kitakapofika kipindi cha kuanza tena kilimo, wale watu wataambiwa waondoke. Sasa kwa nini usimweleze mtu kipindi hiki ambacho anavuna, ajue kwamba nikimaliza kuvuna, nitaelekea wapi? Badala ya kumsubiria kipindi cha kiangazi ambacho anataka kuanza tena msimu mwingine wa kulima, watu wanaambiwa waondoke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, chonde. Tunajua Serikali ya Mama Samia ni sikivu. Tunaiomba itupatie fidia mapema iwezekanavyo ili wale watu waondoke eneo husika na hatimaye waweze kupata makazi mapya na waendelee na maisha yao kwa amani, kama walivyofanyiwa wenzetu wa Msowelo, wametoka Ngorongoro, wameenda Handeni, Tanga, wamepewa malipo yao, wameondoka kwa usalama. Nami naamini hata zoezi la Ngombo nalo litafanyika kwa amani ili nchi yetu iendelee kuwa na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili, nazungumzia kuhusu wanyama. Mkoa wa Morogoro ni Mkoa ambao kila siku nasema tumebahatika. Miongoni mwa mikoa iliyobahatika Morogoro ni mmojawapo. Tumepitiwa na mbuga ya Wanyama ya *Selous* ambayo sasa hivi tunaiita ya Mwalimu Nyerere, Mikumi, Udzungwa, na kadhalika, lakini Mkoa ule tuna adha. Tembo au wanyama wakali wanatusumbua. Sasa katika wale wanyama wakali jamani, ukiangalia sana kimkoa, unakuta ule mkoa sisi kama Serikali isipokuwa na huruma ya kutuangalia, kuwe na mkakati wa makusudi kwa ajili ya kuwaokoa wananchi wa mkoa ule. Ukweli sisi tutaisha kwa sababu, ule mkoa unapakana na hizo mbuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninapoongea hapa katika Wilaya ya Mvomero, kuna Wilaya ya Malinyi na Wilaya ya Kilosa. Mfano, Wilaya ya Mvomero ni Wilaya ambayo inapakana na Tarafa ya Mlali ambayo ina Kata za Doma, Lubungo, Merera, Msongozi na Mangai. Sasa hivi ninavyoongea hapa, katika mwaka huu tu, watu 42 wameshafariki katika Wilaya ya Mvomero, Tarafa ya Mlali. Ombi letu ni nini kwa Serikali? Hatuwezi tukasema kwamba zile mbuga hatuzipendi, tunazipenda sana, lakini sababu ni nini ambayo inafanya wale wanyama watoke kwenye njia zao au kwenye maisha yao ya asili waje kwenye miji ya watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni kwamba, unakuta kwenye zile mbuga za wanyama kuna watu wanaishi kule wenye mifugo. Wafugaji wameingia kwenye zile mbuga zetu. Sasa zile mbuga wanavyoingia kule wanasababisha wale wanyama wanashindwa kuishi kwenye maeneo yao ya asili. Wanapika na wengine wamejenga kwenye njia za wale Wanyama. Matokeo yake wale wanyama wanatoka, wanakuja kwenye makazi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye mbuga kuna Askari ambao ni Askari wa Wanyamapori. *Why* yule mfugaji anajenga kibanda, ana ng'ombe labda 2,000? Ina maana wale Askari hawawaoni hao ng'ombe 2,000? Hawawaoni hao wachungaji? Hata hivyo wale wanyama wanatoka wanakuja kwa watu kwa sababu eneo lao la asili limekaliwa na watu ambao wanawasumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba, Wizara ya Maliasili kwa namna nyingine inahusika kupitia Askari wao. Inakuwaje wanyama na wale binadamu ambao wanaingia kwenye zile mbuga wasiwaone, lakini mwananchi wa kawaida akienda kutafuta kuni anaonekana? Ina maana wale wanyama hawaonekani? Ni wadogo kiasi kwamba mwananchi wa kawaida anaonekana? Tunaiomba Serikali, chonde ituonee huruma, ituwekee *fence* ikiwezekana. Tupate angalau tuweze kuzuia wale wanyama wasiingie kwenye makazi ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, sisi Morogoro ni Mkoa ambao una mkakati. Ni Mkoa ndani ya mikoa yenye mikakati ya kilimo. Tunamshukuru Mungu na kweli Waziri wa Kilimo ametupelekea wataalamu kule. Nililalamika sana kuhusiana na suala la kwamba hatuna soko la mazao hasa ya mpunga, lakini kuna wataalamu wako kule, wanakaa wanafanya tathmini kuona ni jinsi gani ya kuendesha hilo soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika huu mkoa, kuna shida ya ushuru. Wakulima wengi wakienda kupeleka mazao yao, kwa mfano, Serikali mlituambia kwamba mtu anatakiwa kulipishwa mpaka ifikie tani moja ya mzigo, lakini sisi mtu akiwa hata na kilo 20 analipishwa; akiwa na kilo 80, analipishwa: Je, Serikali ule uamuzi wa kusema kwamba wananchi wanatakiwa walipie kuanzia tani moja umesahaulika? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. Tunaomba Serikali mtusaidie, ule mkoa jamani ni wa kimkakati, ili tuweze kuishi kama wengine wanavyofurahia maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle kama mchangiaji wetu wa mwisho kwa *session* hii ya asubuhi.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu wa leo kwenye bajeti hii ya Serikali.

Kwanza niseme kwamba naunga mkono kauli ya Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mashariki, Mheshimiwa Miraji

Mtaturu kwamba wapo watu katika nchi hii wanaona taabu mtu akipongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe Watanzania, mtu asiyependa kupongeza ni mtu mwenye wivu au ni mtu msahaulifu kwa mema aliyofanyiwa. Kwa hiyo, nimesoma bajeti hii ya Wizara ya Fedha na nimejiuliza swali moja tu: Je, bajeti hii inajibu kero za wananchi wangu wa Lupembe? Nimekuta jibu ni ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii imebeba matumaini makubwa, imebeba miradi ya umeme kwa wananchi, imebeba miradi ya barabara, imebeba miradi ya maji ya Kichiwa, Maduma na Tagamenda, Nyombo, Matigangila, na kadhalika. Bajeti hii ya Wizara ya Fedha imebeba fedha ya kupeleka mbolea ya ruzuku kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, hii ni bajeti muhimu. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya Taifa letu. Nami kwa niaba ya wananchi wa Lupembe, namwombea Mheshimiwa Rais afya njema na siha njema ya kufanya kazi kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii. Kwa mara ya kwanza Watanzania wameshuhudia kwenye majimbo yetu, tunayo miradi mingi mpaka imefika mahali wakandarasi hawapatikani, fedha ziko nyingi sana. Mambo haya yamefanikiwa kwa sababu, Waziri wetu wa Fedha bila shaka amekuwa ni mshauri mzuri sana kwa Mheshimiwa Rais. Nasi tunamuunga mkono, tuendelee kupeleka fedha wananchi wapate maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi, na kipekee namshukuru Katibu wetu wa CCM, *Comrade* Daniel Godfrey Chongolo kwa kusimamia vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Wabunge tumeshuhudia mahali pengi, Katibu wetu Mkuu na timu yake wanatembea kwenye majimbo yetu wakitoa hamasa kwa wananchi na kutoa wito wa ilani kutekelezwa. Hongereni sana

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chingolo na timu yako yote ya chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye mchango wa bajeti. Nianze kwenye eneo la changamoto za wafanyabiashara. Nimesoma kwenye Bajeti hii ya Serikali na nipongeze kwamba Serikali imetambua umuhimu wa kukuza sekta binafsi. Kutambua sekta binafsi ni kwa sababu sekta binafsi inalipa kodi kubwa sana Serikalini. Namwomba Mheshimiwa Waziri, Serikali imefanya uamuzi mzuri. Kwanza tulimsikia Mheshimiwa Rais akiwaambia wafanyabiashara wanaoanza biashara mpya kupewa muda angalau wa mwaka mmoja ndipo waanze kulipa kodi. Huu ni uamuzi mzuri sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumemsikia Waziri hapa ndani akisema anataka wafanyabiashara wenye madai ya kodi wasibughudhiwe, wasifungiwe biashara, badala yake waelimishwe jinsi ya kulipa kodi zao. Haya ni maamuzi mazuri, yanaonesha kulea na kukuza sekta binafsi ya wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kumekuwa na kero kubwa sana kwa wafanyabiashara. Kule kwangu Lupembe na Mkoa wa Njombe kwa ujumla, wafanyabiashara wengi wanasumbuliwa sana magetini na Maofisa wa *TRA*. Mageti kama ya Migori na Mikumi, kuna usumbufu mkubwa sana kwa wafanyabiashara, mpaka Wabunge tupige simu ndiyo watu waachiwe. Kwa hiyo, imekuwa kama kufanya biashara kwenye nchi hii ni kero, ni usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa uzito kabisa, kwa sababu Wizara ya Jinsia na Watoto wanalo dawati maalum la kushughulikia masuala ya jinsia, nakushauri Mheshimiwa Waziri, anzisha dawati maalum la wafanyabiashara kwenye Wizara hii, ili wafanyabiashara wapate fursa ya kutoa kero zao moja kwa moja kwako Wizarani. Hili jambo likifanyika hivyo, Mheshimiwa Waziri utakuwa karibu sana na wafanyabiashara na kujibu kero zao kwa wakati. Dawati hili ni muhimu, aajiriwe mtu maalum kupokea kero za Watanzania hasa wafanyabiashara. Hii ni kuhusu wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu kilimo. Nimeongea mara nyingi hapa ndani kwamba Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe ni msemaji wa wakulima, ni mkombozi wa wakulima wa Tanzania. Mheshimiwa Bashe anafanya kazi nzuri sana. Mwaka 2022 Mheshimiwa Bashe ametangaza maeneo kadhaa hapa nchini kwamba, mkulima wa Tanzania aachwe kuuza mazao yake anakotaka. Aachwe kama walivyo wafanyabiashara wengine wa soda, sukari, na kadhalika. Nataka nikuhakikishie uamuzi ule wa Serikali wakulima wetu waliupokea vizuri sana. Sasa ushauri wangu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siku za karibuni huu mkanganyiko wa wafanyabiashara kutokwenda kununua haya mazao, hizi taarifa kwamba wamezuiwa kununua mazao na kwenda nje, Mheshimiwa Waziri, asubuhi na jana ametoa kauli nzuri sana hapa ndani kwamba, Serikali haijazuia wananchi kuuza mazao popote wanakotaka. Nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kuna jambo moja kubwa sana nyuma ya hili suala, kuna urasimu mkubwa wa kutoa vibali vya wafanyabiashara wa haya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wanazinguliwa sana huko maofisini. Vibali havipatikani, leseni hazipatikani. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu jambo hili limeshakuwa kero, kule kwangu Lupembe, watu wa Ikondo, Ninga, Mtwango, Kichiwa, Igongolo, Ikula, na kadhalika, mahindi yameanza kushuka bei kutoka shilingi 15,000, wameanza kuuza kwa shilingi 5,000. Ni mporomoko mkubwa sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri mambo mawili; jambo la kwanza atangaze mamlaka yetu ya kununua nafaka ianze mara moja kununua nafaka kwa wananchi; pili, atoe bei elekezi, wanunue kwa bei gani kwa wakulima? La tatu,…

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, naomba sana Serikali iongeze fedha za kununua haya mahindi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ameamua kuwasaidia wakulima wa Tanzania, afuatilie kwa ukaribu upatikanaji wa vibali vya kununua mahindi na mazao kwa wananchi wetu… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kabla hujamaliza, nafikiri kuna Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuhusiana na hoja hiyo.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe na wakulima wa Tanzania. Wakala wa Chakula wa Serikali *(National Food Reserve Agency)* ameshaanza kununua mahindi, na bei ya chini anayonunulia ni shilingi 600 mpaka shilingi 700 na tumeanza kufungua vituo katika Wilaya zote na Serikali itatoa tangazo. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Mfumo wa kutoa vibali vya *export* kwa watu wote watakaokuwa na *Business License,* badala ya kutoa leseni *manually,* tutaanza kutoa leseni za *export* na kuuza mazao kuanzia tarehe 1 Julai kwenye mtandao ili kuondoa hiyo adha anayoisema kwamba, Wilayani wanasumbuliwa. Kwa hiyo, leseni zote zitatoka *online* kuanzia tarehe 1 mwezi wa saba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swalle unaipokea Taarifa?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa heshima kubwa sana. Nilisema hapa ndani kwamba, mzigo mzito wa kulima amepewa Mnyamwezi, Mheshimiwa Bashe, hongera sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye suala zima la ajira. Hili jambo la ajira limesemwa mara nyingi na watu wengi hapa nchini. Sisi kama chama, tumeahidi ajira milioni nane kwa Watanzania. Kwa takwimu zilizopo, kila mwaka karibu Watanzania milioni moja wanaingia kwenye soko la ajira kutafuta ajira, lakini uwezo wetu wa kuajiri hauzidi 70,000 pengine. Sasa maana yake

kundi kubwa halipo kwenye mfumo rasmi wa ajira. Ushauri wangu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, juzi hapa ndani tumetunga sheria kama Bunge ya kuanzisha Tume ya Mipango kwa ajili ya kushauri mipango mbalimbali ya Serikali. Ninaomba Serikali kupitia tume hii ikaanzishe mpango maalum wa kufufua viwanda vingi ambavyo vimekufa. Sisi kule Njombe kwa mfano, tulikuwa na kiwanda cha maziwa ambacho kingetoa ajira nyingi sana, kimekufa. Tulikuwa na kiwanda cha parachichi *(Urivado)* kimekufa. Viwanda vya chai vina hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoweka mpango wa kufufua viwanda vilivyokufa, hatuwezi kuongeza ajira. Serikali duniani kote haiwezi kuajiri wananchi wote wakapata ajira rasmi Serikalini. Kwa hiyo, hili ni jambo la kwanza ambalo Tume yetu ya Mipango lazima iliangalie kwa ajili ya kuongeza ajira kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nataka niseme kuhusu barabara yangu ya muhimu sana; barabara ya Kibena – Lupembe mpaka Madeke. Hii barabara imekuwa na ahadi ya muda mrefu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwaka 2022 Rais wetu amekuja Njombe na Mheshimiwa Waziri alikuwepo. Barabara hii Mheshimiwa Rais ameagiza ianze ujenzi. Nimeambiwa mchakato wa kuandaa tenda umeanza. Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye bajeti hii ambayo mimi naiunga mkono, barabara hii ianze kujengwa kwenye bajeti hii ya 2023/2024 ili kusudi mwakani tukija hapa tukupongeze kwa kazi nzuri ambazo unafanya huko Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naona umeinua *mic,* natoa rai kwa Waziri wetu wa TAMISEMI pamoja na watu wa fedha, wananchi wetu wanayo maboma mengi ya zahanati, maboma mengi ya madarasa, vituo vya afya, na kadhaliak. Wekeni mpango maalum wa kumaliza maboma haya ili kuwatia moyo wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa majadiliano yetu kwa *session* ya asubuhi. Tutakaporudi mchana tutaendelea na wachangiaji mbalimbali tukianza na Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge pamoja na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma na wengine wataendelea kutajwa kadiri itakavyokuwa imepangwa.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala ulio mbele yetu, Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Tutaanza na Mheshimiwa

Maimuna Ahmad Pathan, atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia hoja ya mjadala wa Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, na wote tuliopo humu ndani tumepewa uhai na Mwenyezi Mungu, tunatakiwa tumshukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuendeleza miradi mbalimbali ya zamani na kuanzisha miradi mipya. Kwanza kuna miradi ya kuchochea uchumi; pili, kuna miradi ya huduma za jamii. Mama huyu amefanya kazi kubwa na kazi zote zinaonekana, mama huyu tumpe maua yake kwa kweli. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha, kwa kazi zao nzuri ambazo wamezifanya kwa kutuletea bajeti yenye mashiko. Bajeti hii ni bajeti nzuri ambayo inakidhi kwa mwananchi wa kawaida, kwa kweli ni bajeti nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi tunampongeza na kumshukru sana mama Dkt. Samia kwa mradi wa *EPC+F* wa barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale. Barabara hii kwa kweli kila siku nilikuwa nikiinuka, nikisimama hapa nalia na hii barabara. Maswali yangu ya msingi kila siku ilikuwa ni hii barabara. Lakini tunamshukuru sana mama huyu kwa kutukubalia sisi watu wa Mkoa wa Lindi, tumesaini mkataba tarehe 16 Juni; kwa kweli tunashukuru sana, mama ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamshukuru mama Dkt. Samia kwa kutuletea Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko. Tunashukuru sana, kazi zimeanza kufanywa pale, hatua za mwanzo za ujenzi zinaendelea; tunamshukuru sana mama Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna wastaafu kwenda kuhakikiwa mkoani. Sisi wote hapa, asilimia kubwa sisi ni wastaafu, tuko hapa ndani wastaafu wa Serikali. Tunajua kuna wastaafu wengine walistaafu miaka mingi, hali zao za uchumi ni mbaya. Fedha wanayopata ni ndogo sana. inakuaje hili suala la kuhakikiwa kila mwaka watoke kule vijijini wapite wilaya, waende mkoani? Kitu gani kinashindikana Wizara ya Fedha kufanya utaratibu wakafuatwa kwenye wilaya zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela walizokuwa nazo za mafao yao ni ndogo sana jamani. Niombe sana, kwa mfano umtoe mtu wa Kilima Rondo afike Nachingwea, aende Lindi, aisee, ni mbali sana. Umtoe mtu wa Kilwa huko ndani ndani, afike mjini, aende Lindi, nafikiri hii siyo sawa. Hebu tufanye marekebisho watumishi waende kila wilaya kuwasaidia hawa watu kuhakiki taarifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni ajira ya maafisa ustawi wa jamii, siyo maendeleo ya jamii, maafisa ustawi wa jamii. Sasa hivi kuna matatizo sana ya afya ya akili, watu wengi kutokana na msongo wa mawazo wamekuwa na matatizo ya afya ya akili. Lakini cha kushangaza kwenye nchi yetu hawa maafisa ustawi wa jamii wako wachache sana. Mbaya zaidi hao wachache waliokuwepo wanapewa kazi za maendeleo ya jamii kuzifanya badala ya kazi za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ndiyo *consultants* ambao wanatakiwa kuwasaidia watu wenye msongo, watu wenye matatizo ya afya ya akili. Sasa inakuaje badala ya kufanya kazi zao au watu wengine waongezeke, wale wanakwenda kufanya kazi za maendeleo ya jamii? Nafikiri hii siyo sawa. Kwanza tujitahidi maafisa ustawi wa jamii waajiriwe wa kutosha, waongezeke, wako wachache sana. Wale ni watu *hot cake,* wanatakiwa sana kwa matatizo tuliyokuwa nayo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine kwa Serikali ni kwa ajili ya tembo. Huyu tembo huyu, kwa jina lingine ndovu, anatuchanganya sana akili. Naona maeneo mengi ya Tanzania wanalalamika kuhusu ndovu. Sasa huko kwetu Mkoa wa Lindi ndiyo kichekesho, maana yake sasa imekuwa ni *too much,* mpaka saa 12 asubuhi wako nyumbani kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekula mazao yote mashambani yamekwisha, wanachofanya sasa hivi wanabomoa nyumba za watu. Juzi kuamkia jana kuna Kijiji kinaitwa Nambalapala huko Wilaya ya Nachingwea, wameingia ndovu wametafuta mashambani mtama, wameshamaliza kila kitu, kilichofuatia wamekwenda kubomoa nyumba kutafuta vyakula ndani. Hivi sasa tutakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, nitoe ushauri wangu mdogo kama wataweza kuusikiliza ili tunusuru wananchi wa Tanzania. Naomba tuweke *solar electric fences.* Kuna nchi mbalimbali ambazo wamefanya hiki kitu kama India, *South Africa,* hata hapo Kenya kidogo wameanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoijua Serikali yetu inaweza hiki kitu. Kama tumeweza kuweka umeme sasa hivi tunategemea kila kijiji kutakuwa na umeme, sidhani kama tutashindwa kuweka hiki kitu. Kwa sabbu hizi *solar electric fences* siyo kila sehemu, ni sehemu zile ambazo zinazungukwa na mbuga za wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *solar electric fences* zikifungwa vizuri, mnyama yeyote hawezi kuvuka. Wanavyotengeneza pale yule mnyama akisogelea tu karibu na ile fensi kuna kashoti fulani kanatokea, mnyama anaogopa, anarudi ndani. Niombe sana Serikali yangu, najua hii Serikali ni sikivu – iweke hizi *solar electric fences* kwenye mbuga za wanyama ili kunusuru wananchi hawa ambao tunasumbuliwa na tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yaliyochukuliwa na vikosi vya jeshi 41KJ Nachingwea na kikosi cha JKT hapohapo Nachingwea. Kulikuwa na mashamba ya muda mefu ambayo

yanahudumiwa na wananchi pale tangu mababu na mabibi zetu wanahudumia yale mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali yetu sikivu iwalipe kiinua mgongo angalau wale watu wapate pesa za kwenda kuanzia sehemu nyingine kununua mashamba. Hali ni mbaya, watu hawana uwezo wa kununua mashamba, hela imekuwa ngumu, ndovu ndiyo kama hao, vyakula mashambani hakuna, hali ni mbaya. Tunaomba wasaidiwe watu hawa walipwe ili waweze kusaidiwa kupata hela kwenda kununua maeneo mengine. *(Makofi)*

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Chinguile, karibu.

**TAARIFA**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza sasa kwamba haya maeneo ambayo wananchi wana mgogoro na Jeshi letu la Wananchi, siyo tu kwamba wanapaswa kulipwa, maeneo haya kumekuja na taarifa mbili tofauti. Taarifa za awali ni kwamba walielekezwa watapata malipo, lakini taarifa nyingine walivyokuja maafisa wengine wa Jeshi wakaeleza kwamba eneo hili hawatalipwa. Kwa hiyo kwa sasa wananchi wamebaki bila kujua hatma yao ni nini. Naomba kumpa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna, taarifa unaipokea?

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matengenezo ya viwanja vya ndege; Kiwanja cha Ndege cha Lindi Mjini na Nachingwea. Tunaomba viwanja vile vitengenezwe. Nimeangalia kwenye bajeti sijaona, sijui labda kama macho yangu yamekuwa yana matatizo. Tunaomba viwanja hivi vitengenezwe kwa sababu sasa

hivi tunategemea mradi mkubwa sana wa gesi pale Lindi tusije tukatia aibu viwanja vikiwa vibaya jamani. Tunaomba tuangaliwe kwa macho mawili, tutengenezewe viwanja hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia pia suala la ofisi za *CAG*. Kila mwaka na kila siku tunazungumza masuala haya, tukiangalia kwenye ripoti za *CAG* makosa mara nyingi ni yaleyale yanajirudia kila mwaka. Leo utaona kosa hili, ikija ripoti ya mwakani kosa ni hilohilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipendekeze kitu kimoja; hawa ma-*internal auditors* walioko kule nafikiri wanashindwa kufanya vizuri kazi zao. Ombi langu kwa Serikali, hawa maafisa wa *CAG* sasa wapelekwe kila Wizara ili waende kushauri kule na kupunguza haya matatizo. Tupunguze hoja nyingi zinazojirudia kila siku kuja Bungeni. Tunaona makosa yanayotokea kwenye ripoti zile za *CAG* kila siku yanarudi yaleyale. Mnashauri vizuri, Bunge tunakaa tunashauri lakini inapokuja ripoti ya mwaka mwingine yaleyale tena. Sasa inakuaje?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kuniruhusu nami nichangie hoja hii ya hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango, lakini pia mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii yenye mapato na matumizi ya mwaka 2023/24 ni bajeti ya wananchi. Na hii

tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, bajeti imebeba unafuu wa maeneo kadhaa muhimu kwa ajili ya wananchi. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan lakini pia kwa kuweka vipaumbekle vya sekta zifuatazo; elimu, maji, barabara, nishati na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hizi ndiyo zinazongoza kwa maendeleo ya wananchi. Wananchi wakipata mafanikio katika haya mambo matano, ndiyo watakuwa wamesema tumepata maendeleo. Maeneo haya matano yanagusa wananchi wote Tanzania na ndiyo maana nasema kwa kweli bajeti ya mwaka huu ya mama Samia Suluhu Hassan na ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Wizara yake, ni ya wananchi. Hongereni sana Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa mliyoifanya kuandaa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje maeneo ambayo yametugusa sisi wananchi, na haya ni baadhi tu; moja, tozo ya *SDL* au ujuzi wa elimu. Tozo hii nilipoingia Bungeni hapa ilikuwa ni asilimia sita ya kila mfanyakazi wa sekta binafsi mshahara wake analipiwa na mwajiri asilimia sita. Na hii ilikuwa taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya kuomba kazi katika Nchi za Afrika Mashariki, ile gharama ya ajira kwetu ilikuwa iko juu sana. Hii tozo haipo Uganda, haipo Rwanda wala Burundi, Kenya ipo asilimia ndogo tu kwenye sehemu ya utalii. Lakini Tanzania ilikuwa asilimia sita. Leo nasimama hapa – na ninaomba nitoe taarifa kwamba ni mwajiri imepunguzwa kutoka asilimia sita mpaka asilimia tatu; sisi waajiri tunampongeza sana mama. Na hili hakika hatutamsahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, kuondoa ada za vyuo vya kati. Nimesoma vyuo vya kati hivyo, vinaitwa elimu ya ufundi ama elimu ya amali, kutokea shule ya msingi na kwenda shule ya upili (sekondari) *form one* mpaka *form four* (kidato cha kwanza mpaka cha nne) unachagua masomo ya kiufundi, halafu unakwenda chuo cha ufundi. Wakati huo zilikuwa shule mbili tu, Shule ya Sekondari ya Ufundi Ifunda na Moshi *Technical. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunalipwa hela na Serikali sisi kusoma pale. Sijui ilitokea nini wakaondoa ikalazimu wanafunzi walipe ada pale, wazazi wenye uwezo wa chini walishindwa kupata wataalamu wa ufundi kwa sababu hatukuweza kulipa tena ada; tunamshukuru sana mama Samia na kwa hilo mama Samia hatuwezi kukusahau kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni Serikali kutofunga biashara kwa sababu ya migogoro ya kodi kati ya wafanyabiashara na Serikali. Suala la kufunga biashara ilikuwa inafunga mapato ya Serikali, ilikuwa inafunga kodI za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, umepiga ndipo. Kwa kuondoa hizo gharama za kuwafungia watu, wengine wamepoteza roho zao, wengine wamekufa, ilikuwa taabu sana. Hebu fikiria una biashara yako unakula na unaishi halafu imefungwa kwa sababu ulikosea kidogo mahesabu na siyo watu wote ni wataalamu; umefanya jambo zuri sana, Mungu akuongoze na hatutakusahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne; mapendekezo ya Serikali yanalenga kuendeleza miradi iliyopo. Nimepitia bajeti yote hii, inalenga matrilioni ya fedha ili kumaliza miradi inayoendelea kimkakati. Niitaje hapa; Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR,* Daraja la Magufuli, ununuzi wa ndege, ujenzi wa meli, ujenzi wa barabara, kuendeleza *REA* (umeme), ujenzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa vituo vya afya, elimu bure, kuongeza bajeti ya kilimo. Haya siyo mambo madogo. Ndiyo maana nasema leo hii, na ninaweza kusema kifua mbele kwamba bajeti hii ni ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kulijali sana jimbo langu. Jimbo la Tabora Kaskazini ukifumba macho ukaangalia mambo yaliyopita lilikuwa la ajabu ajabu sana. Leo tumepata hela nyingi sana kupitia Halmashauri ya Uyui, tumepata fedha nyingi sana kutekeleza miradi ya elimu, maji, umeme, barabara, afya na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Uyui ilikuwa hana majengo, tulikuwa chini ya mti tumejishikiza kwa *DC*. Tumepata majengo ya shilingi bilioni nne, majengo mazuri ya kisasa. Tena ndiyo ghorofa la kwanza kijijini kule lipo; tunamshukuru sana mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaka unda haneni, maana yake akinena kishapata, naogopa kuyasema mambo mazuri yanayokuja kwangu, lakini wacha niwatajieni machache, hamtayaondoa. Kwa ufupi, bajeti hii iliyomalizika imefanya mambo yafuatayo katika Jimbo langu, na nimesema niyataje; tumejenga kituo cha *VETA,* tumejenga madarasa mengi ya shule za sekondari na msingi, tumejenga mradi wa *BOOST,* tumepewa shule mpya ya msingi (milioni 500), mpya kabisa tujenge; tumepewa shule ya sekondari mpya tujenge (milioni 470). Na kuhusu afya tumepewa vituo vya afya vitatu tumejenga na vimekamilika. Lakini pia tumepewa zahanati mbili na zahanati nyingi tumekarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya siyo madogo ya kuacha kupongeza. Ni lazima tumpongeze mama huyu ambaye ana utu, ana mapenzi na wananchi wake, lakini ni mlezi wa wananchi wake, ametuona sisi Uyui. Nani kama mama? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, nikwambie, ndiyo nimesema mtaka hunda haleni msione wivu kidogo. Jimbo la Tabora Kaskazini lina vijiji 68 tunafungua maji ya bomba chini ya miti kutoka Mwanza Ziwa Victoria na haya hayakuwepo kabisa. Leo tuna maji ya bomba ya Ziwa Victoria lakini pia mradi wa ile miji 28 katika vijiji vyangu 82 utaongeza vijiji vinavyopata maji mpaka vifike 72. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mwigulu na Wizara yako, mmetutendea mambo mazuri sana Jimbo la Tabora Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na umeme, umeme tulipoingia madarakani sisi hata Kijiji kimoja hapakuwa na umeme. Leo hii nasimama hapa nasema vijiji 58 tunawasha umeme, bado vijiji 24, na ambavyo mpaka mwezi wa nane unakamilika. Hii ni

bajeti ambayo sisi wana Uyui tunaiona kama ni ndoto vile lakini ni bajeti ambayo tunafikiria kwamba imetubeba vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, Jimbo langu ni jipya, Wilaya yangu ni mpya tulikuwa hatuwezi kutembeleana barabara hakuna tumejenga barabara. Mama ametupa ela nyingi karibu bilioni tatu tujenge barabara na barabara zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeitaja miradi hii ambayo ni alama za utu, upendo na ulezi wa Mama Samia Suluhu Hassan jimboni kwangu. Pongezi nyingi kutoka kwa wana Uyuwi Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge hoja mkono, Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali ambayo ipo ndani ya Bunge letu na sisi kama Wabunge tunaendelea kuichangia na kuiunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba Waziri wa Fedha na timu yake nzima ya Wizara yake kwa namna ambavyo wamejipanga kuhakikisha kwamba wanaleta mapinduzi ya kweli katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa bajeti iliyokuja sina mashaka nayo na mimi nawatakia kila la kheri Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza katika kuhakikisha kwamba trilioni 41 na zaidi iweze kupatikana ili mipango ya kimaendeleo katika nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anachapa kazi lakini kwa namna ambavyo ametekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na ya

kimaendeleo inayogusa jamii yetu. Sisi kama Wabunge kupitia majimbo yetu tumeshuhudia kuona miradi mbalimbali imetekelezwa na tumeendelea kupiga hatua kubwa. Mheshimiwa Rais wetu ni mzalendo wa kweli na kweli anataka kuleta mapinduzi ya kweli kuhakikisha kwamba anapunguza umaskini nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze ndugu zetu wa *TRA* kwa namna ambavyo wameendelea kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kwa miaka mitatu mfululizo kama taarifa ya Kamati ilivyotueleza. *TRA* wanatufanyia kazi nzuri, lakini kulipa kodi ni uzalendo. Wako wafanyabiashara ambao mteja anapoingia dukani kununua bidhaa na kumuuliza kwamba unataka bei ya risiti ama bei isiyokuwa ya risiti, huu si uungwana. Ninawaomba wafanyabiashara Watanzania tuwe wazalendo wa kweli tuhakikishe kwamba tunaiunga mkono Serikali kwa kutoa risiti. Watanzania wanapaswa wawe wazalendo kwa nchi yao kuhakikisha kwamba wanaponunua bidhaa basi waweze kudai risiti ili kwa pamoja tuungane kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Wizara ya Nishati; Wizara ya Nishati wanafanya kazi nzuri na sisi tunaiona, na mimi naendelea kuwabariki kwa sababu tunaendelea kunufaika na suala zima la nishati. Lakini wamekuja na mpango mahususi wa kumtua mama kuni kichwani. Mpango huu ni mzuri, Watanzania sasa tumechoka kutumia kuni na mkaa, na Watanzania walio wengi wanapenda kutumia umeme na gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Hasa sisi wanawake wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tumechoka kutumia kuni na mkaa. Kwanza vinaathiri afya yetu ule moshi tunaovuta ukiingia ndani ya mapafu tunaathirika afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Waziri wetu wa Fedha kuhakikisha kwamba vifaa vya matumizi kama majiko ya gesi, majiko ya umeme, pasi na vinginevyo vinaondolewa ama vinapunguzwa kodi ili wananchi Watanzania waweze kumudu kununua majiko haya na waachane na matumizi ya mkaa na gesi. Wenzetu wameanza na kampeni nzuri na Wizara ya Fedha tuunge mkono kampeni hii inayofanywa na

Wizara ya Nishati kwa kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapunguzwa bei ili Watanzania waweze kumudu kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Wizara ya Kilimo. Niwapongeze Wizara ya Kilimo kwa sababu wameongezewa bajeti ya milioni 900. Tuna mfumo wa ununuzi wa pembejeo, ninaomba Serikali waangalie kwa sababu mfumo huu hauendani na kalenda ya upuliziaji wa dawa ya mikorosho. Kwa hiyo ninaomba wabadilishe mfumo huu wa manunuzi wa pembejeo ili uendane na kalenda ile ambayo wakulima wanahitaji pembejeo kutumia katika zao hili la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia ndugu zetu wa *TAWA* pamoja na *ASA* aongezewe bajeti yao kuhakikisha kwamba wanaendelea kufanya utafiti wa kuzalisha mbegu bora ili wakulima waweze kupata mbegu yenye kuleta tija katika uzalishaji wa mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie suala la wazalishaji wa chumvi. Wazalishaji wa chumvi mpaka unapata kiroba cha kilo 25 gharama yake inafika takriban shilingi 4,500. Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto mbalimbali, chumvi isiyotiwa madini joto maana yake haiwezi kutumika. Wizara ya Afya walitoa mafunzo na madini joto yalitolewa bure, lakini ikaenda madini joto kilo moja ikafika shilingi 30,000, na sasa hivi madini joto kilogram moja ni 150,000. Hii imekuwa ni changamoto na ni hatari tunaweza tukatumia chumvi ambayo haina madini joto kwa sababu ya gharama kubwa ambayo wanaifanya hawa wazalishaji wa chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kama ambavyo tunatoa pembejeo basi kwenye wazalishaji wa chumvi tutoe madini joto kwa ruzuku ya Serikali ili wazalishaji wa chumvi waweze kupata unafuu na urahisi wa kutumia madini joto na chumvi yetu iweze kutiwa madini joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ujenzi. Nipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali tunazoendelea nazo za kuhakikisha kwamba njia ya kukua kiuchumi zinaboreshwa. Lakini tunayo changamoto, naomba tufanye mapitio tena ya sera na

kuangalia sera ya barabara. Barabara hizi ambazo zinaunganisha Bandari na nchi jirani, barabara kuu za kiuchumi hazijengwi kwa ubora ule unao stahili, ama zikijengwa hazichukui hata mwaka tayari zimekufa. Pamoja na kwamba tunayo mizani ya kudhibiti uzito wa magari barabarani lakini bado barabara zetu zinaendelea kuwa mbovu na Serikali inatumia gharama kubwa sana kuhakikisha kwamba kila mwaka barabara zinafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba barabara hizi zinakuwa imara na zinaweza kudumu zaidi ya miaka miwili mitatu ili kuokoa fedha ya Serikali na iweze kwenda kufanya kazi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwazungumzie wakandarasi wa Tanzania hasa wale walioanzia *class seven*. Tunajua kwamba wao wanapata kazi ndogondogo lakini bado wana changamoto, kwanza wanapopata mradi wanakwenda kusajili mradi *TRB,* pia wanasajili mradi OSHA, na bado wanalipa madini, kokoto, mchanga na mawe wanalipa *SBL* kwa maana ya *Levy* kwa vibarua lakini bado wanalipa *fire*, wanalipa *NEMC*, bado wanalipa kodi ya *TRA*. Utakuta mlolongo wa tozo unakuwa mkubwa sana kwa hiyo wanatumia gharama kubwa lakini wakati mwingine viwango vinakuwa tofauti tofauti kila mara. Niombe Serikali kuhakikisha kwamba viwango basi viwe vinafanana kila wakati visiwe vinabadilika. Kwa hiyo niombe sana Serikali kuhakikisha kwamba wanaendelea kuwatazama wakandarasi hawa ili nao wawe wakubwa ili waendelee kufanya kazi zetu na wasaidie watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. Tumeona matunda mazuri katika maeneo yetu, tumefarijika sana. Miradi mikubwa ya maendeleo iko katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti kuu ya Serikali. Kwanza kabisa napenda nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba Watanzania tunaishi katika maisha mazuri. Ni ukweli usipingika kwamba katika kipindi chake cha uongozi hakuna hata jimbo moja katika nchi hii ya Tanzania ambalo limekosa mradi mkubwa wa maendfeleo kutoka kwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu za pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa wanayoifanya, na hasa hii ya kutuandalia bajeti, ambayo itakuwa mkombozi kwa wananchi wetu wa hali ya chini katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa vipaumbele vyake vya bajeti ya mwaka 2023/2024. Kwanza kabisa nianzie katika miradi mikubwa ya maendeleo; Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili litakapo kamilika litakuwa mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Tanzania na hasa kwa kutupatia umeme wa uhakikia na wenye unafuu. Ni matumaini yangu kabisa, litakapokwisha Bwawa hili, la Mwalimu Nyerere, Watanzania wengi watanufaika na kufaidika na umeme wa bei rahisi kama ilivyoelezwa na viongozi wetu hapo nyuma, kwamba Bwawa la Mwalimu Nyerere litakapokwisha basi hali ya umeme nchini itarudi katika ubora wake na wananchi watapata unafuu wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa Mradi wa *SGR*. Mradi huu utakapokamilika utaleta maendeleo makubwa sana katika nchi yetu. Pia nipongeze Wizara ya Fedha kwa kuongeza bajeti katika Wizara ya Kilimo

hadi kufikia bilioni 170.8. Haya ni maendeleo makubwa sana ambayo tunakwenda kuyapitia katika nchi yetu. Pia nipongeze Wizara kwa kutenga fedha katika vipaumbele vyake kujenga mabwawa 100 kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Hii itasaidia sana katika sekta ya kilimo na wananchi wa Tanzania watapata manufaa makubwa kupitia mabwawa haya 100 ambayo yanakusudiwa kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu zingine nizitoe kwa Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa ujumla katika kipaumbele cha Mradi wa *SEZ* Bagamoyo. Mradi huu ni wa miaka mingi. Tangu wananchi walipofanyiwa tathmini yapata miaka kumi na nne. Lakini sasa Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi pamoja na viongozi wake wameamua sasa mradi huu waupe kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu. Hii ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo ya Zinga Bagamoyo wanafaidika na wananufaika ili miradi ya maendeleo ya viwanda pale iweze kuanza na wananchi pamoja na nchi nzima iweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala moja, jana wachangiaji wengi sana walizungumza kuhusu suala la kodi ya ngano, na mimi nataka nilizungumzie kidogo suala hili. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba pamoja na Mawaziri wenzie wa Afrika Mashariki kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Wameona ni jinsi gani hizi nchi za Afrika Mashariki zinavyotaabika katika suala zima la chakula. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kabisa, mwaka 2019 uchumi katika kwa upande wa mfumuko wa bei ilikuwa 3.5 *percent* lakini mpaka kufika mwaka 2022, mfumuko wa bei umefikia asilimia 8.7 hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii inasababishwa na Vita ya Ukraine pamoja na Ugonjwa wa *Covid* ambao ulitupitia. Sasa basi naomba kitu kimoja, tuiunge mkono bajeti hii na hasa katika suala zima la kupunguza kodi katika chakula. Mimi nikupongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mawaziri wenzio wa Afrika Mashariki kwa hatua mliyochukua. Leo hii kwa mfano suala la ngano, wafanyabiashara wa Tanzania, uzalishaji wao wa ngano ni tani milioni moja na laki moja mpaka tani milioni moja na

laki mbili. Uzalishaji wetu katika nchi sidhani kama unazidi tani laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukisema kwamba unawapandishia kodi ya ushuru wa forodha asilimia 35, Mama Ntilie wetu, wapika chapati, wapika mandazi hivi watakuwa katika hali gani? Kwa sababu mfanyabiashara utakapompandishia kodi lazima na yeye atapandisha bei ya bidhaa, na atakapo pandisha bei ya bidhaa wanaokuja kuathirika ni wananchi wakawaida. Kwa hiyo nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hatua hii, hakuna jambo baya ambalo limefanyika, jambo ni kunusuru maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza. Naomba Mheshimiwa Waziri hili kidogo alitilie mkazo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake wametoza bidhaa za viwango vya asilimia 20 kwenye mashine za kamari zinazoagizwa nchini. Mimi kwa maoni yangu hizi mashine za kamari ni janga kubwa sana katika Taifa letu. Pamoja na kwamba tunapata mapato kwa kupitia mashine hizi za kamari lakini kipato tunachopata ni kidogo kuliko athari ambayo wanaipata wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii baba ana shilingi 15,000 yake baada ya kwenda kununua unga wa watoto wakale nyumbani anakwenda kucheza kamari, akifika kule fedha zote analiwa, akirudi nyumbani hana chakula cha watoto, fedha yote kaibwaga katika kamari. Halafu Je, tuna *control* gani ya hawa wanaochezesha kamari kama hizi fedha wanapeleka benki? Asilimia kubwa wakitoa fedha kwenye mashine zao wanapeleka majumbani mwao kuhifadhi, mzunguko wa mabenki unapungua.

Mheshimiwa Waziri nikuombe sana hili suala mliangalie kwa kina *either* kama tunahitaji kupata kodi katika hizi mashine za kamari basi tuongeze kodi kubwa sana. Na kama hatupati kodi ya kutosha basi tuziache kwa sababu hazituletei faida, zinaumiza wananchi wetu. Wananchi kwa kweli wamekuwa mateja wamekuwa *addicted* na hizi kamari, uchumi wao unakuwa mbaya, maisha yao yanakuwa magumu kwa kwa sababu ya kucheza kamari kila siku. Mheshimiwa Waziri mimi naomba sana,

kuna vitu vingi vya mapato vya kubuni lakini hiki sio chanzo ambacho ni afya kwa maendeleo ya wanajamii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala taasisi zinazokopesha. Kuna taasisi ambazo zimezuka mitaani huko zinakopesha watu, hizi taasisi kwa kweli ni janga kwa wananchi wa Tanzania. Kuna taasisi ambazo wananchi wanafikia hatua mpaka wanakimbia majumbani kwao. Leo mwananchi wa kawaida mama wa Bagamoyo ambaye hakusoma unamwambia nitakukopesha kwa asilimia ya 45 riba, hajui maana ya asilimia 45 ni nini, anachukua mkopo baadaye anaambiwa katika laki moja uliyochukua unatakiwa ulipe shilingi 45,000, anashangaa. Yeye anafikiri kaambiwa kwamba alipe shilingi 45,000 ya kuchukua laki moja, sasa hii inaleta changamoto kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taasisi mmezipa vibali nyingi sana, hazifanyi kazi yenye kutukuka kwa wananchi wetu. Watu wanaacha nyumba zao, wanakimbia kwa sababu ya kukimbia mikopo ambayo inakopeshwa na hizi taasisi. Naomba Wizara ichukue hatua kuhakikisha kwamba kunakuwa na taasisi maalum ambazo zitapewa vibali zenye kukopesha tena kwa masharti ya riba maalum ili wananchi waweze kupata hiyo mikopo na wasiathirike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya, kazi ya kuandaa bajeti sio kazi ya mchezo. Bajeti hii ni bajeti ya mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa anayoifanya. Kazi ya kuandaa bajeti sio kazi ya mchezo. Bajeti hii ni bajeti ya mfano wa kuigwa. Bajeti ambayo itakwenda kurejesha uhai wa wananchi wa Tanzania. Nimshauri Mheshimiwa Waziri, maneno yapo mengi, watu wanasema sana, lakini kazi wanayoifanya ni kubwa. Leo hii mmekaa katika hizo nafasi sio kwa nia mbaya ya kuwadhulumu au kuwanyanyasa Watanzania. Lengo na madhumuni yao ni kuwajenga Watanzania. Kwa hiyo, wajitahidi, pale ambapo wataona panafaa, basi wahakikishe kwamba

bajeti wameitengeneza vizuri na wananchi wapate faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti yetu Kuu. Kwa kuanza naomba nitambue kazi kubwa ambayo inafanyika. Si haba kupandisha pato la Taifa kutoka bilioni 69.9 mwaka 2021 kwenda bilioni 89.4 dola za Kimarekani ni kazi kubwa sana na matumaini ya kwamba bajeti yetu au pato letu la Taifa litaendelea kukua kwa asilimia 5.2, ni kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya kilimo imeongezwa kutoka bilioni 294 mpaka kufikia bilioni 970.8 mwaka 2023/2024. Hapo tunajihakikishia kwamba tutapata pembejeo, viuatilifu vya kutosha, zana za kilimo lakini wakulima wetu wataendelea kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa afya tumejenga vyumba 111 vya huduma za dharura na pale Hanang sisi tumepata chuma kimoja ambacho kinakaribia kukamilika, vyumba vya wagonjwa mahututi 70 navyo vinakwenda kujengwa, navyo vinaenda kukamilika, nyumba za watumishi wa afya 150 zimejengwa na sisi Hanang tumepata nyumba moja na tumeipeleka pale Zahanati ya Gidagharibu pale Kata ya Simbay. Hii ni kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepeleka vifaatiba katika maeneo mbalimbali. Hanang tumepata *x–ray* ya kisasa katika Hospitali ya Wilaya ya Tumaini, lakini vifaa kama *CT-Scan* zaidi ya 30 zimepelekwa, *MRI* na vifaa vingine. Hanang tunatarajia kupata *ambulance* mbili, ni kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya nishati, miradi mikubwa inaendelea. Bwawa la Mwalimu Nyerere linaendelea kukamilika, lakini na miradi mingine inaendelea kukamilika ili kujihakikishia kwamba gridi yetu inakuwa na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika kwa upande wa *TARURA*, barabara nyingi zimejengwa. Tumejenga kilometa 798.1 za lami, lakini kilometa elfu 23.2 hizo za changarawe pamoja na madaraja kadhaa. Mpango wa kutengeneza *P4R* kwenye upande wa ujenzi wa barabara, hii itatusaidia sana. Ndio maana unasikia Wabunge hapa wanasifia kazi nzuri inayofanyika na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wengine wanasema tumpe maua yake, naunga mkono maua yake apewe kwa kazi nzuri inayofanyika na sisi kwenye majimbo yetu kila sehemu amegusa, ni kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kukumbusha kwenye eneo la *TARURA,* tunayo majimbo tofauti. Kwenye Jimbo la Hanang kwa sensa ya sasa hivi tuna watu 367,391, kaya ziko karibu 70,000. Vilevile tuna majimbo mengine madogo ambayo hata watu 100,000 hawafiki, kupewa mgao sawasawa sio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye upande wa nishati hilo pia limefanyika, kwamba kila Jimbo lipewe vitongoji 15 kwa mwaka huu wa fedha. Hilo sio sawa kwa sababu haitaleta tija, tumefanya sensa tumetumia fedha. Hii sensa itumike na wataalam ili hatimaye mgawanyo wa rasilimali uende sawia kwenye majimbo yetu, maendeleo yaende sawa sawa kwenye majimbo yetu. Idadi ya watu izingatiwe ndio maana tumeingia gharama, jiografia ya maeneo yetu izingatiwe ili hatimaye maendeleo yaende sawasawa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewekeza sana kwenye sekta ya kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anafanya kazi kubwa sana na timu yake. Nampongeza sana rafiki yangu Mheshimiwa Bashe. Hata hivyo, nimhakikishie tumeanza kuingia mashambani mwezi wa 11, kila mtu amepambana kwa namna yake, wengine wamepata na wengine wamekosa. Sasa hivi tuna changamoto na leo hii mimi niko hapa Bungeni kule kwangu wamekaa kikao,

maelekezo ni kwamba ukitaka kusafirisha gunia moja la mahindi kwenda Babati, kwenda Arusha mpaka upate kibali kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, hii inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wameenda mashambani kipindi kile Serikali hatukuiona. Sasa hivi tumevuna, tumehangaika wenyewe mbona *control* zinakuwa nyingi? Kwa nini Serikali isiwe *proactive* inakuwa *reactive?* Sisi tunachotaka tukiingia mashambani, Wizara tumeweka fedha za kutosha, wachochee uzalishaji. Wasiende kudhibiti baada ya watu kuwa wamesota mashambani, wao wanazuia sijui watu wasiuze, sijui wasifanyeje. Hii si kazi ya Serikali, Serikali itusaidie tuzalishe zaidi na itusaidie kuweka mifumo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa inajulikana kwamba kuanzia mwezi Machi hadi sasa tutavuna. Kwa nini mipango hai isiwepo kabla hata muda huu haujafika? Tusiwakwamishe wakulima. Sisi wana Hanang na Watanzania wengi wako kama wana Hanang wanategemea yale wanayopata mashambani, wanategemea mifugo yao kupeleka watoto shule, ni kipindi cha shule kufunguliwa. Sasa hivi biashara ya mazao haieleweki, mifugo tumeuza wakati tunakwenda mashambani. Sasa, unategemea watoto watarudije shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itusaidie wakati tunakwenda mashambani, watusaidie mbolea na vitu vingine ili angalau wakati huo tukishazalisha watutengenezee na masoko. Vile vile, kwenye eneo la masoko iwe *streamline* tuijue, suala la masoko yanakuwa Wizara ya Kilimo au Viwanda na Biashara ili mwishoni sasa tum–*task* Waziri wa Kilimo kwenye suala la uzalishaji ili upande wa viwana na biashara wahangaike kututafutia masoko. Watusaidie kwenye eneo hili mambo haya yanawachanganya wananchi wetu na hii haikai sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujawahi kumwona Mkuu wa Wilaya wakati tunakwenda mashambani na hatutarajii kumwona Mkuu wa Wilaya sasa hivi wala kwenda kuomba kibali kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo suala la miundombinu. Pia kwenye eneo hili, kazi kubwa yamefanyika. Nikisoma kwenye upande wa uchukuzi, reli hesabu zinasomeka vizuri, lakini napata changamoto kubwa kwenye upande wa barabara. Mwaka 2022 kwenye bajeti kama hii, nilipata nafasi ya kukaa na Waziri wa Ujenzi, tukachorachora Barabara, lakini mpaka sasa sioni kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Kondoa inayokwenda Gisambalang inayotokea Nangwa tulichorachora na Mheshimiwa Waziri mwaka 2022, lakini hakuna kinachoendelea. Vilevile barabara ya Katesh – Haydom, mara zote nimeambiwa hapa Bungeni ni sehemu ya barabara inayotoka Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago mpaka Maswa. Juzi wamekwenda kusaini mkataba hata mwaliko Mbunge wa Jimbo la Hanang sikupata na tuna tawi letu hilo ambalo kila mwaka tunaambiwa ni sehemu ya barabara hiyo. Je, yale niliyokuwa naambiwa hapa nilikuwa nadanganywa au wananchi wa Hanang wanadanganywa au Mbunge nilikuwa nadanganywa? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwa pale Katesh, babu zake nilivyosema hiyo barabara, nikawambia unabeba pochi ya Mama na yeye ni mtoto mwaminifu wa mama, hiyo pochi ambembeleze mama aifungue kidogo hiyo barabara ijengwe. Wana-Hanang ni wale waliopiga makofi Waziri akatikisa kichwa, lakini mpaka leo hakuna kitu alichoweka pale, hakuna kinachoeleweka. Sasa sisi tufanye nini? Kwenye bajeti hii nikisema naunga mkono bajeti, narudi Hanang wananipokeaje? Tusemezane tu ukweli si aliwambia mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa Kampeni amesimama Bassotu, Katesh, Gehandu, tumeongea barabara hiyo hiyo. Tukirudi nyuma Dkt. Magufuli alifanya hivyo hivyo. Tukirudi nyuma Dkt. Jakaya Kikwete naye alifanya hivyo hivyo, mimi nikirudi sasa hivi naenda kuwaambia nini? Tuelezane tu ukweli, barabara hii tumeisema sana na si mimi wa kwanza kuisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 Dkt. Mary Nagu alisimama hapa Bungeni akidai barabara hiyo…

**MHE. MIRAJI J. MTATURU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji mtani wetu ambaye ametuita sisi babu zake kwamba, unapoambiwa barabara ni kiungo maana yake barabara kuu itakamilika *feeder road* itajengwa. Kwa hiyo, maana yake ndiyo hiyo tafsiri halisi ya barabara ambayo inaungiwa pale. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Hhayuma, unapokea taarifa?

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namheshimu sana mjukuu wangu lakini naomba asitumie muda wangu na naomba tu unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara hii limesemwa mara nyingi kwamba ni *feeder road* na maneno yamekuwa ni mengi. Sisi tunachotaka barabara hiyo ijengwe na wala hatutaki maneno mengine na ili nijiridhishe kwamba kwenye bajeti hii tuko pamoja nipate maelezo ya kina na wala sina lingine zaidi ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako ndio umekwishayoyoma hivyo. Malizia sentesi yako.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi na naamini Mheshimiwa Waziri atakuwa

na maelezo ya kina ili tukubaliane bajeti hii ni ya kwetu au ya kwake?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti ya Serikali ya mwaka 2023/2024. Kwanza kabisa, nichukue nafasi ya kuipongeza Serikali kwa kuchukua hoja nyingi sana za Wabunge katika kupanga Bajeti yake. Pia jioni ya leo nitaongelea maeneo mawili ambayo ndio hasa napenda kuyaongelea yaliyochukuliwa katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kabisa ni ile ambapo Serikali imedhamiria kuanzisha akiba ya dhahabu kupitia Benki Kuu. Katika ukurasa wa 18, hotuba ya Waziri inasema, naomba ninukuu: "Serikali imekamilisha taratibu za kununua dhahabu kupitia Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuanzisha akiba ya dhahabu ya Taifa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni njema kwa sababu kwanza itaimarisha sarafu yetu ya Tanzania, lakini pia ni akiba kwa vizazi vijavyo, yaani hata kama migodi ya dhabu itaisha, lakini tutawapeleka watoto wetu na vizazi vijavyo kwenye *vault* na kuwaonesha kwamba hebu angalieni urithi wenu. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani Mheshimiwa Waziri afanye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kule Benki Kuu ya Tanzania kuna kilo 418 ambazo zimekuwa zikitaifishwa kwa sababu ya makosa ya utoroshaji na kwa sababu sheria inasema kwamba, ukipatikana umetorosha hiyo itataifishwa. Sasa hizi kilo 418 zina thamani ya bilioni 53.2. Pendekezo langu achukue hizi kilo 418 apeleke zikasafishwe *(refinery)* ili iwe kianzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ili pendekezo la Mheshimiwa Waziri liweze kuthibitika, yaani maneno yake yathibitike kwamba Serikali inaanza, kwa nini asitaje kwamba mwaka huu anaanza na kilo ngapi katika kuanzisha akiba ya dhahabu ya Taifa? Nadhani hapo atakuwa ametenda haki kuliko yaendelee kubaki kama maneno kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niongelee uanzishwaji wa Tume ya Mipango. Hili pia ni jambo ambalo limeongelewa sana na Wabunge wengi na tumeona Serikali imelichukua na hatimaye kuliweka katika utekelezaji na katika hili tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna matarajio ya wananchi katika uanzishwaji wa Tume ya Mipango. Moja kabisa, tunataka kuona kwamba Tume yetu inaondoa *duplication of efforts* (kurudiwa rudiwa jambo kufanywa na Wizara zaidi ya moja lakini jambo ni lile lile). Wakati fulani nilikwishasema hapa kwamba, Wizara ya Maji imekuwa ikijenga mabwawa, Wizara ya Mifugo nayo imekuwa ikijenga mabwawa, lakini Wizara ya Kilimo, kazi hiyo hiyo. Hebu tuombe sasa kwa sababu ya kuwepo kwa Tume ya Mipango hii *duplication* iweze kuondolewa na tuweze kupata tija kuliko mradi unaofanana ukafanywa na Wizara zaidi ya moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba tunategemea Tume yetu ya Mipango iweze kuiangalia nchi na Jiografia yake na idadi ya watu waliopo na maendeleo yaliyokwishafanyika katika eneo lile na maendeleo yanayohitajika. Mifano ambayo ni halisi, Jimbo moja unaweza ukakuta lina kata nne lakini Jimbo lingine lina kata 45, lakini wote wanasema wanapewa kilometa moja ya lami, kwa nini? Yaani kata nne, kata 45 kilometa moja ya lami? Hapana. Au *VETA* moja, hii inawezekanaje? Tunategemea Tume yetu ya Mipango iweze kuondoa kutokuwa na usawa katika maeneo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta hapa nchini kuna wilaya moja ina kilometa saba tu za lami tangu iwepo, nyingine ina kilometa 200, lakini zote ziko katika nchi moja. Tunategemea Tume

yetu ya Mipango iweze kuangalia mahali ambapo pako *disadvantaged* ili waweze kushiriki keki ya Taifa sawasawana hili linajenga umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine, wakati mwingine utakuta mikoa mingine inazungukwa na Maziwa makubwa lakini huduma ya maji ni hafifu katika maeneo hayo. Tunategemea Tume yetu ya Taifa iliangalie hili ili kuweka msawazo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wakati mwingine zao moja linapokuwa linapata bei nzuri katika soko, utashangaa mikoa yote ya Tanzania wanataka wawe wakulima wa zao hilo hilo. Hii haiwezekani lazima kuwe na kanda za ikolojia na mazao yanayostawi katika eneo husika ndiyo yalimwe. Sio kwamba Tanzania nzima baadaye tunakuja tunakuta kwamba kuna mikorosho kila mahali, hapana hii haiwezekani. Kwa hiyo, tunategemea Tume yetu ya Mipango iangalie hali ya hewa, wingi wa mvua, joto, halafu iseme jamani hapa sio pa korosho, hapa ni pamba ni hivyo na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matarajio ya Tume ya Mipango, katika mipango yake ya kitaifa, napenda sana Tume ya Mipango izingatie *cultural integration,* nilikuwa natafuta neno zuri hapa mwingine akanishauri kwa kuniambia ni mwingiliano wa kiutamaduni. Hili naomba nilisema hivi, tulipo hapa wote, Taifa hili lina makabila 120 lakini limeweza kulinda umoja wake kama tulivyo kwa sababu ya mwingiliano ambao tumekutana JKT, vyuoni na wengine tumeoana na kuoa kwa kuingiliana hivyo na tukalinda umoja wetu wa kitaifa na ndio maana hapa hakuna mgogoro ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kuna shule za Kata. Kwa hiyo mtu atasoma *primary* pale pale, *secondary* pale pale, halafu utakuta watu wanasema naomba mkoani kwangu peleka chuo kikuu. Kwa hiyo, mtu atakuwa m-*local* akiwa m-*local* utashangaa tunajenga ukabila na ukanda. Kwa hiyo, lazima katika mipango ya kitaifa kuwe na vyuo ambavyo vitabaki katika Kanda moja ili watu tuendelee kuingiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sivyo, kinyume chake utakapotengeneza Taifa la wa–*local* wenye ukanda mmoja, wa kabila moja kwa sababu tangu *primary* mpaka chuo kikuu kama ni Kagera yaani ni hao wenzako tu hao hao, hapana. Lazima tuangalie *cultural integration* kiasi kwamba tuendelee kuingiliana. Kwa hiyo, katika mipango yao lazima waangalie kwamba inapofikia *level* fulani tuwaruhusu watu waende sehemu nyingine ili tuendelee kuingiliana ili tuweze kuendelea kujenga umoja wa kitaifa, tuondoe ukanda, tuondoe ukabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo matarajio yetu katika utendaji kazi wa Tume ya Mipango ambayo tunaamini itapewa meno na kuweza kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hii Bajeti Kuu pamoja na Mpango wa Taifa. Kwa kuanza tu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, lakini shukrani za dhati kwa Mama Samia kwa suala ambalo tumelipigia kelele, lile suala la *bureau de change* ambalo wamelifanyia kazi nimeona kwenye ukurasa wa 53 na 54 wa Hotuba ya Bajeti Kuu, lakini inaonekana wamefanyia kazi Arusha peke yake na ameahidi kuendelea kuondoa au kurekebisha vile vigezo ili na maeneo mengine basi waweze kufanya hii biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza Serikali kwa namna inavyoendelea kusimamia uchumi wetu, uchumi wetu umekua sasa karibu bilioni 85 ikilinganishwa na bilioni 69, ni hatua kubwa na mengine mazuri yanakuja mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mapendekezo maeneo matatu kabla sijaendelea na maeneo yale ambayo nafikiria kuyachangia. Kwenye eneo la mazao nimeielewe vizuri sana nia

ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo Mheshimiwa Bashe, nia yake ni njema kabisa na tukimsikiliza tutaona haya ambayo anakusudia ili mazao haya yaje kuonekana kwenye *export* zetu kwa maana ya thamani zake. Niendelee kumshauri yale masoko ya ukanda huu wa pembezoni wayawekee nguvu sasa, ina maana upande ule wa Namanga upande huu wa kila maeneo yenye mpaka ambayo kunapitisha mazao waimarishe yale masoko na kule Kilimanjaro tulikuwa tuna eneo lile la Lokolova ili haya mambo ambayo ambayo amekusudia ambayo Mheshimiwa Rais amekusudia yaweze kufanyika kwa uzuri zaidi bila kuleta usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili ni kwenye kodi inayotaka kuwekwa kwenye *cement*. Mimi nadhani ukiangalia sensa yetu inaonesha uwiano wa watu na umiliki wa makazi, kwa sababu kwenye dodoso kulikuwa kuna umiliki wa makazi pale, sasa na makazi yaliyoandikwa pale ni makazi ya aina gani, sidhani tumefikia mahali pa kuweka kodi kwenye *cement,* watu bado wanalala nyumba za tembe ni viizuri tuangalie chanzo kingine hii ya *cement* tena ilitakiwa tu-s*ubsidies* ili watu waendelee kujenga nyumba tutoke kwenye nyumba za Tembe tuwe tunalala kwenye nyumba za *cement*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mafuta pia natoa ushauri, sioni kuweka shilingi 100 kwa wote inaleta tija. Hebu Wizara ikae na wataalam waangalie ni namna gani tunaweza tukawa na bei *uniform* ya mafuta nchi nzima. Kwa sababu kule Kigoma wanalipa bei ghali sana mafuta na wanakipato kidogo, wakati Dar es Salaam wanalipa kidogo sana na Tanga kwa sababu wapo karibu na bahari. Ni vizuri tuangalie uwezekano wa kuzifufua zile *depot* za maeneo kule Moshi kulikuwa kuna *depot,* sijui huko *Mwanza depot* na Serikali iangalie uwezekano wa kuisimamia tuwe na bei moja kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *CocaCola* na kampuni za maji wanaweza, kwamba nchi nzima kuna bei moja na kama bei ya usafiri ndiyo inaleta shida Mheshimiwa Bashe alitoa zile pikipiki kwa Maafisa Ugani zimewekwa *GPS* zote tunaweza kufunga magari yote yanayosafirisha mafuta *GPS* kuhakikisha kwamba ile gharama haiwezi kutuletea utofauti mkubwa wa bei, tukawa na

bei moja ya mafuta nchi nzima ninaamini linawezekana badala ya kuongeza shilingi 100 kwa watu wote wakati watu wa Dar es Salaam mafuta ni bei rahisi, huku Kigoma Mikoani Arusha huko tunapata mafuta ni bei ya juu. Kwa hiyo, nimesema hayo masuala matatu nitoe ushauri ili tuweze kusonga mbele tuone namna ambavyo tunaweza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la utalii. Ninakumbuka kwenye semina ambayo tulifapewa na Wizara ya Utalii walisema Tanzania inategemea maliasili tu kwenye utalii. Pamoja na maliasili ambayo inaleta mpaka *conflict* kwa baadhi ya maeneo kwa maana ya wakulima sijui na wafugaji na maeneo ya hifadhi maana yake bado tuna nafasi ya kuweka vivutio ambavyo ni *man-made*. Dubai vivutio vyake asilimia kubwa karibu vyote ni *man-made* na wanapata watalii milioni 14, 16 kwa mwaka. Sisi na hii Maliasili pamoja na zile changamoto ambazo zimetajwa tunapata 1,400,000 ambayo ndiyo *the highest* tumepata mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kwa yale maeneo ambayo tunaweza kuongeza vivutio ambavyo ni *man-made* ambavyo havina madhara *negative* kwa jamii yawekwe na ndipo hapo niliposema kwa mfano suala la *cable car* kuna *argument* kwamba haina madhara na kuna *argument* kwamba ina madhara, msimamo wangu na msimamo wa wananchi ni kwamba kama *cable car* haipunguzi mapato ya Serikali, haiharibu mazingira, haipunguzi ajira, haina madhara *negatively* kwa mapato ya Serikali wanaihitaji ili iongeze mapato. Kwa hiyo, kama *negative impact* hazipo tunaihitaji lakini kama zipo basi hilo tunaona haina tija kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kidogo ambacho ninadhani Wizara inatakiwa ikifanyie kazi na ni Wizara ya Viwanda na Biashara, inaingia Wizara ya Afya tuliondoa *TFDA* tukaweka *TMDA* lakini *aspect* ya chakula hasa kwenye *import* na *export TBS* hawawezi kuifanya lakini ukiacha *TBS* hawawezi kuifanya pia siyo *international practice,* ni vizuri suala dogo kama hili ni suala la uamuzi leteni sheria hapa turudishe *TFDA* watu wakiweka miguu chini nje kwenye vyakula tunavyo-*export* hatuwezi kabisa kusimama kwa sababu hatuna *TFDA*. *TMDA* hifanyi ile kazi ilikuwa

inafanya *TFDA* na badala yake TBS pia hawawezi kupima vitu kama maziwa haya ya watoto hizi formula, kwa hiyo tufanye tu mara moja siyo kila kitu mpaka Rais aseme ndiyo tufanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mitumba ya nguo viatu ambavyo ni *second hand* kwenye nchi yetu. Kwa hali ya sasa mitumba inayokuja Tanzania ni ya hali ya chini sana, kwanza wale wafanyabiashara wanapoteza fedha kwa sababu wanafungua mtumba wanakuta nguo zinazouzika ni chache lakini wananchi wetu wananunua nguo nza mitumba za bei kubwa ambazo hazina ubora. Kuna watu wananunua mitumba Kenya wanaileta mpaka Tanzania Mikoa mingi tu, tumeona wana-*advertise* ni mtumba wa Kenya una ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu katika usimamizi wa eneo hili, hebu Serikali iende iangalie namna ya kulisimamia ikiwa ni pamoja na hizo hatua ambazo mnazifikiria mbele za kuondoa hii, lakini wakati mnai-*ban* mitumba mhakikishe kuna nguo zinazotoka kwenye hizi nchi zinazo-*import* zina *quality,* kwa sababu sasa hivi tuna-*import* vitu kutoka baadhi ya nchi, zikija hapa tunaambiwa ni Ngozi lakini vikivaliwa siku mbili vimechanika huwezi kulinganisha na vile vya mtumba ambavyo vipo, kwa hiyo hatua ya ku-*ban* mitumba iangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Moshi kuna Kiwanda cha Karanga *Leather*. Serikali ime-*invest billions of moneys* zaidi ya bilioni mia moja lakini Serikali haijaweza kusimamia kile kiwanda, kiwanda kinategemea kiajiri watu 10,000 wale wa moja kwa moja 3,000 lakini mpaka sasa hivi kimeajiri watu 250 na hela imeenda pale. Rais kila siku anasema mumwambie Mashirika na Makampuni ya Serikali ambayo hayafanyi vizuri sasa tusiendelee kutengeneza matatizo, kama kuna hao Wabia waletwe waingie kwenye kile Kiwanda cha *leather* pale Moshi kiweze kuleta ajira, tulete Pato la Taifa na kodi iweze kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi ambayo bado sijaweza kupata mantiki yake, kodi tunazotoza kwenye magari chakavu. Ukiangalia *dumping* ya kwetu haiakisi kusudio la kuanzishwa kwake. Maana ya *dumping* ilikuwa magari ambayo ni ya zamani

sana yasiingie nchini na kwa bahati mbaya *dumping* yetu ina-*charge percentage* ya *value*. Sasa gari linavyozidi kuwa la zamani zaidi, *value* yake kule inazidi kuwa ndogo kwa hiyo hata kukata *percentage* maana yake gari ya zamani utaikuta bei ya kufika hapa ni rahisi kuliko gari ya mwaka jana. Hebu tuangalie tutafute *dumping* ambayo itasaidia magari ya karibuni yawe na bei nafuu kuliko magari ya zamani sana ili ilete tija. Kwa hiyo, magari hapa Tanzania yamekuwa aghari bila sababu na maana yake ni kwamba hatumsaidii Mtanzania, lakini gari lina faida lina mafuta, kuna mambo ya gereji, kuna udereva hapo leseni zinakatwa, kwa hiyo ni vizuri mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya 2023/2024. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya nami nimeweza kusimama na kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nizungumze kwenye hizi barabara. Tumeona wenzetu wa Kusini sasa hivi wanasheherekea, wanashangilia wanasifia lakini yapo maeneo ambayo na sisi tumekuwa tukipiga kelele sana kuhusiana na barabara angalau za kuunganisha Mkoa na Mkoa ama Wilaya na Wilaya ambazo bado ni changamoto kubwa sana. Mimi ningeomba sana kwa Wizara ya Fedha tunayo barabara ambayo inatoka Mpanda inapita Kaliua kwenda Kahama, ningeomba sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi naye atusikie kwenye barabara hii, tumeshapigia kelele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo kwanza ipo pembezoni lakini pili Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo ina wakulima wengi, yaani sisi shughuli zetu za kutuingizia kipato ni kilimo. Sasa kama tunalima

sana halafu tunakuwa hatuna barabara kwa ajili ya kusafirisha mazao yetu, hili jambo kwa kweli haliwezekani. Kwa hiyo, na sisi tuombe sana, tunaomba barabara inayotoka Mpanda kwenda Kaliua kufika Kahama ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kurahisisha usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ambayo inatoka Tabora Mjini inakwenda Bukene kupitia Mambali. Hii barabara nimeiongelea sana Mheshimiwa Naibu Waziri hapa aliniahidi mara kadhaa kwamba hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie katika bajeti hii angalau hata kilomita chache ili zingine ziweze kuingia baadae, nakuomba sana tusaidie ili kuweza kusaidia wananchi wetu wanaotoka Tabora, badala ya kuzunguka kwenda mpaka Nzega ili waende wakatokee waende Kahama wapite hapa wapite Mambali-Bukene waingie Kahama na mwisho wa siku wanafika mpaka Mwanza. Kwa hiyo, itatusaidia pia kupunguza safari kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na hili ongezeko la kwenye masuala ya Utalii. Bado tuna safari ndefu sana kama mpaka sasa tunazungumzia ongezeko la kutoka dola 1,310 tumefika 2,527 kwa nchi yetu ya Tanzania yenye vivutio vya kutosha, yenye vivutio vizuri, yenye mambo mengi ya ajabu, mpaka leo tunazungumzia 2,527, bado tuna safari ndefu. Tuna sema tuko kwenye asilimia 93, Tanzania sasa hivi tulitakiwa kuwa tunazungumzia asilimia180 mpaka 200 kwa jinsi tulivyokuwa na vivutio vizuri, tulivyokuwa na vivutio vya kutosha, tulivyokuwa na maajabu mengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe Wizara ya Fedha huku mnapata fedha na nilishawahi kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha "ukitaka kula sharti uliwe". Mheshimiwa Waziri wa Fedha anachukua fedha katika hizi taasisi lakini fedha hazirudi kule kwenda kutekeleza majukumu. *TANAPA* sasa hivi wanazo hifadhi 16, *TAWA* wana mapori ya akiba ya kutosha, *TFS* wana misitu chungu nzima, sikuambii na huko Ngorongoro lakini kote huko tunakusanya mapato, katika mapato yale lazima tufike mahali tukubali kutoa ili tuweze kutengeneza tupate zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha huku kuna hela, huku fedha ipo, lakini tuwekeze ilituweze kupata tija kwenye hili suala la utalii. Kama Mheshimiwa Rais aliamua kwa dhati ya moyo wake kutangaza utalii, kazi aliyoifanya ni kubwa sana, kama Wabunge tunaendelea kushauri Wizara iangalie kwa jicho la tatu kwenye hii sekta ya maliasili na utalii ili tuweze kuongeza mapato pia yaweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya maliasili ina changamoto nyingi ikiwemo wafanyakazi wake kulalamikia maslahi yao, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha waangalie namna gani ya kuweza kuwasaidia watumishi hawa kuhusiana na maslahi yao, wanafanya kazi ngumu, wanafanya kazi hatarishi. Kwa kweli, mimi nimewahi kuhudumu kwenye Kamati hii ya Maliasili nimejionea mwenyewe, kuna maeneo unakwenda unasema hivi kuna Askari wako huku wanafanya kazi unaambiwa wapo wanafanya kazi. Sasa kwa nini tusiwaangalie na kuona ni namna gani tunavyoweza kuwasaidia ili kuweza kuongeza maslahi yao. Pia kazi hizi zinafanywa na wote ni za aina moja siyo tofauti lakini maslahi yao wanalipwa tofauti tofauti, sasa hii inavunja moyo wale wengine kufanya kazi kwa sababu wanaona kwa nini wengine wapate zaidi kuliko mimi wakati kazi tunayofanya ni ya aina moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara ya Fedha liangalieni hili jambo, ondoeni matabaka ili kazi ziweze kufanyika kwa ufanisi. Kuna wakati mwingine mnasikia watu wanauawa, wanyama wanakufa, saa zingine watu wanakasirika wanaona ngoja na mimi nilale zangu bwana kwani nini? Lakini mkitengeneza mazingira mazuri kwa wafanyakazi wa sekta hii ya maliasili na utalii mimi naamini kabisa tutaongeza mapato kutoka hizo dola 2,527 tutafika mapa dola elfu tano na kitu, ushauri wangu kwa Wizara ninaomba sana wakichukua fedha wapeleke fedha ili kazi ziweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya utalii zipo taasisi za utafiti, hizi taasisi haziguswi kabisa, yaani hata ukifika bajeti yao yenyewe pia inakuwa haieleweki. Kwa hiyo mimi niombe sana kwenye Wizara ya Fedha angalieni hizi taasisi za utafiti ili ziweze

kufanya kazi zao vizuri na waweze kuongeza tija katika suala zima la utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa mwanasiasa ni lazima uwe unaangalia mambo yote yanayoendelea, unasikiliza unajua kwamba wapi nini kinafanyika. Juzi katika harakati zangu nilimskia Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM Mheshimiwa Chongolo akiwa Kondoa, migogoro inapunguza sana kasi ya uchumi katika nchi yetu, kama hatukuwa makini huu uchumi tunaouimba utaishia kwa watu ambao huku Mjini tu, lakini kwenye maeneo yenye migogoro tutausikia kwenye bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Katibu Mkuu wa CCM Mheshimiwa Chongolo alikuwa kule kwenye pori la Mkungunero. Pale Mawaziri Nane wameshakwenda na pori lile wakasema kwamba tayari wameshalishughulikia lakini mpaka hivi tunavyozungumza wananchi wamekwenda kulalamika mbele ya Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM. Nazungumza hivyo kwa sababu Tabora tuna mgogoro uliopo Kaliua na mgogoro huu hauna sababu hata kidogo, Mawaziri Nane wamekwenda katika Jimbo la Kaliua, Kata ya Ukumbikakoko na Usinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri hawa walisema hawa wananchi Mheshimiwa Rais ameruhusu waendelee kukaa hapa hapa na ikiwezekana waongezewe na maeneo mengine pale, kwa sababu Serikali haina mpango wa kuyachukua. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujali wananchi hawa, lakini cha ajabu Mawaziri Nane wameondoka kinachoendelea huko ni mgogoro ambao mtakuja kusikia mauaji ambayo hayana hata sababu zozote za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia uchumi lazima uwaguse Watanzania wote bila kujali watu wanaishi wapi. Sasa hawa wanaoishi na migogoro, ambao hawajui kesho yao itakuwaje leo Mheshimiwa Rais ameruhusu wananchi hawa waendelee kubaki lakini anakuja mwingine ndani ya Serikali hiyohiyo anapinga maoni ya Mawaziri Nane walivyokuja na kauli ya Mheshimiwa Rais. Sasa hivi tuseme hii Serikali iko tofauti ama shida ni nini?

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nimeona niliseme hili ili mjue kwamba tunapozungumzia bajeti humu, tunapowasemea Watanzania, tunapomshukuru Mama kwa kuleta bajeti ya Watanzania lakini ajue kuna Watanzania ambao hawanufaiki na haya tunayoyazungumza kwa sababu ya migogoro waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe sana kama inawezekana watenge fedha ziweze kusaidia hii migogoro iweze kupungua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwaifunga dakika kumi zimeisha.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni waliopo Bungeni jioni hii, yupo mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Asha Abdullah Juma ambaye ni ndugu yake kutoka Kakonko, Mkoa wa Kigoma Ndugu Asha Chubwa. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaao wanafunzi 120 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo, Kampasi ya Dodoma Mjini, wakiongozwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Ndugu Farijala Saidi Kunga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili tukufu ili niweze kutoa mchango wangu wa mawazo ambao binafsi naamini unaweza kusaidia Taifa langu kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru awamu zote sita za Uongozi wa Taifa letu. Namshukuru Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mzee Mwinyi, Hayati Benjamin Mkapa, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Hayati Dkt. Magufuli na sasa tuna Mama Samia Suluhu Hassan. Watu wote hawa

wanaendelea kupeleka Taifa letu mbele. Mimi kama Mtanzania nina kila sababu ya kuwashukuru kwa sababu wamefanya maisha yangu yamekuwa bora kwa mambo waliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ambacho nimezoea kukisema kila siku, na nitakirudia tena na tena kwamba tuna Rais *smart, intelligent and clever,* na nitatoa sababu. Huko nyuma niliwahi kusema, alipewa fedha za barakoa akajenga madarasa. Sasa nataka niwaambie kitu kingine leo. Tanzania inauza zaidi Kenya kuliko inavyonunua, la kwanza. La pili, uchumi wetu umekua ndani ya miaka miwili kutoka Dola bilioni 69 mpaka 85. La tatu, ndani ya muda mfupi amefanya kile ambacho wengine kiliwashinda kwa upande wa demokrasia. Amefanya jambo lililokuwa linamtia hofu kila mtu la kuruhusu mikutano ya hadhara ya wapinzani. Amefanya jambo kubwa sana la kwenda mpaka kwenye mkutano wa Umoja akina Mama wa CHADEMA. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba amebadilisha taswira ya nchi yetu Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwona Makamu wa Rais wa Marekani amekuja hapa akatamka, Marekani ikatamka ya kwamba *Tanzania is a democratic country,* tumemaliza. Ile peke yake ni *smartness.* Nataka niwaambie, hiyo ni *smartness,* subirini muone misaada itakavyomiminika kuja hapa nchini kwa sababu ya kitendo hicho kilichofanyika. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais na namtia moyo aendelee kufanya kazi. Aelewe ya kwamba watu wote hawatakubaliana na anachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimtie moyo sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kazi yake ni ngumu. Anafanya kazi ngumu sana ambayo siyo rahisi kueleweka. Ila tukumbuke Henry Ford alipotengeneza gari, watu walikuwa wamezoea farasi, wakakataa gari, lakini baadaye walipozoea gari, wakakataa farasi. Kwa hiyo, yapo mambo ambayo siyo lazima sisi wote tukubali, ilimradi lina maslahi ya Taifa, ilimradi jambo hilo siyo maslahi ya mtu binafsi, lifanywe hata kama wengine hawakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana kwa jimbo langu. Jimbo langu mimi Shigongo Eric la Buchosa limepiga hatua kubwa ndani ya muda mfupi kuliko miaka kumi yote iliyopita. Barabara zinapitika, miradi mingi ya maji, tumejenga madarasa, tuna Chuo cha *VETA,* tuna kivuko kipya cha kwenda Kome cha shilingi bilioni nane, haijapata kutokea. Nisipomsifia Rais wangu, nimsifie nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, niwaambie kitu kimoja, hakuna jambo baya kama kumsifia mtu sifa za uongo. Ni sawa na mimi uniambie nina *six packs* na wakati nina kitambi, unapunguza heshima yako. Niseme ukweli, ukisifiwa sifa za uongo unamdharau anayekupa sifa. Nami natoa sifa hizi kwa Rais kwa sababu ni mambo ya ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niendelee. Nachangia mambo makubwa mawili tu. La kwanza, kukua kwa Taifa letu. Tanzania nchi yangu ninayoipenda inakua. Ni rahisi sana sasa hivi mtu kuzunguka huko akafanya mikutano yake ya hadhara, akawaaminisha watoto wetu kwamba hakuna kinachoendelea na watu wakaamini. Mimi ni wazamani kidogo, nimeshuhudia Marais wengi, lakini ngoja nitoe takwimu chache hapa kuonesha kwamba Taifa letu linakuwa ili kusudi tutembee kifua mbele, tusitembee kwa unyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 tulipopata uhuru barabara za lami zilikuwa kilometa 1,300. Leo ninavyoongea tuna kilometa 14,000. Mwaka 1961 *life expectancy,* umri wa Mtanzania kuishi ilikuwa miaka 38, leo tuna miaka 68. Tulikuwa tuna chuo chetu kimoja, leo tuna vyuo vikuu 47. Tulikuwa na hospitali za wilaya na mikoa 96, leo 1,030. Tulikuwa na vituo vya afya 22 nchi nzima, leo tuna vituo vya afya 4,030. Tulikuwa na zahanati 1,332 leo tuna zahanati 7,458. *This country is growing.* Hii nchi inakua. Tufike mahali tukubali kwamba nchi yetu inakua, asije mtu hapa kutuaminisha kwamba hakuna kinachoendelea, *that is a lie.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tunaweza kutofautiana kuhusu *speed,* wengine wanaona tunaenda polepole, lakini *this country is growing.* Watoto wetu wanaonisikiliza huko nje, wasidanganywe na mtu yoyote, nchi yetu inakua tuendelee

kufanya kazi, muda siyo mrefu tutakamata uchumi wa Afrika na hatimaye kuheshimiwa zaidi ya tunavyoheshimika hivi sasa. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni umaskini wa kipato. Mimi nimetoka katika familia maskini sana, na kwa kweli nauchukia sana umaskini kwa sababu ulinitesa sana nikiwa mtoto. Mungu kanitoa huko, lakini mimi peke yangu kutoka siyo kwamba umeisha, kuna watu nimewaacha wengi huko nyuma. Ndiyo maana napambana na umaskini kila siku. Kwa miaka 23 nimezunguka nchi hii kwenye vyuo, kwenye Makanisa, napambana na umaskini, kuwaelimisha watu mbinu za kutoka kwenye umaskini. Nimeandika mpaka vitabu kwa sababu siupendi umaskini *practically* kwa sababu una mateso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ni Tajiri. Tanzania nchi yangu ni tajiri. Ngoja nikupe *data* kidogo. Tanzania kwa makaa ya mawe ni ya 87 duniani; Tanzania kwa gesi ni ya 82 duniani; Tanzania kwa *Helium* ni ya kwanza duniani; Tanzania kwa dhahabu ni ya 19 duniani; Tanzania nchi yangu kwa almasi, ni nchi ya 17. Nchi hii tajiri, hatutakiwi kuendelea na umaskini wa kipato. Ilitakiwa tuwasaidie watu wetu kubadilisha utajiri huu uweze kuwa pesa na maisha ya watu yabadilike. Tunahitaji pesa kwenye mifuko ya watu wetu. Unapowaambia Watanzania wanajilipia shilingi bilioni 85, wakati mchele ni shilingi 3,500 hawaelewi. Tufanye nini? Muda ni mchache. Tufanye nini kuwasaidia Watanzania wawe na kipato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, *let us invest in agriculture*. Nataka kumsifia sana Mheshimiwa Rais wangu, kumsifia Mheshimiwa wangu Waziri Bashe kwa jinsi ambavyo Tanzania imeamua kuwekeza kwenye kilimo. Ni kilimo pekee yake kitawasaidia Watanzania kutoka kwenye umaskini wa kipato. Naomba tuwekeze kwenye mbegu, tuwekeze kwenye masoko, tuwekeze kwenye teknolojia, watu wetu waweze kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ya kwamba, tuwekeze kwenye kilimo hasa cha mazao ya chakula *(food crops)*. Unaweza ukalima maparachichi, *it is okay*, ukilima pamba *it is okay*, ukalima chai *it is okay,* lakini Wazungu wanaweza

wakaweka sera zao za ushoga hapa, ukakataa sera zao wakasema unajua maparachichi ya Tanzania yana *Sodium Bicarbonate*, wakasema hatuyanunui, lakini tukilima chakula na tukawa ni soko la chakula cha Afrika nzima, nataka kuwahakikishieni, hatuna sababu ya kufunga mipaka. Kwa nini tusiwe soko la chakula la Afrika nzima, watu waje wanunue chakula Tanzania? Tukifanya hivyo, watu wetu watakuwa na pesa mfukoni. *Agriculture*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la muhimu sana, nataka kuona Watanzania wazawa wanawezeshwa kiuchumi. Bajeti ya mwaka huu, shilingi trilioni 44, natamani fedha hizi zibaki kwa vijana wa Kitanzania. Nilishaongea mara nyingi, Watanzania wamechoka kuona wageni wakija hapa wanatajirika wao wanaendelea kubaki maskini, *that is not right*. Siwezi kwenda India leo nikapewa tenda ya kuchapa vitabu vya sekondari. *That is a lie,* lakini Wahindi watakuja hapa watachapa vitabu vya watoto wetu wa shule. Kwa nini? Nataka kuona wazawa wanawezeshwa kushikiklia uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Sheria ya Manunuzi. Hebu sikiliza sasa uone. Sheria ya Manunuzi ambayo nailalamikia kila siku, inasema eti kwenye ku-*supply tender* ikifika shilingi bilioni moja, hiyo *tender* inabadilika inakuwa *international*. Hebu ona sheria hiyo. Mmetunga humu humu ndani kwamba *tender* ikifika Shilingi bilioni moja, inaenda *international.* Eti mimi nipambane na Mturuki, nipambane na Mchina, nipambane na Mwingireza, haiwezekani. Nataka hiyo sheria ibadilishwe. Watanzania hawawezi kushindana na watu wenye mikopo ya dola mbili, sisi tuna mikopo ya dola 22 ya *CRBD*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, sekunde 30.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuisaidia nchi yetu tuwasaidie Watanzania washike

uchumi wa nchi yao. Mambo ya kuwa mashuhuda, wamechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie jambo la mwisho kabisa kwa upendeleo ulionipa. Namwomba Mheshimiwa Waziri apanue wigo wa kodi. Naomba nikushauri, kutegemea kodi pekee yake kama chanzo cha mapato, haiwezekani. Nataka uwezeshe sekta zetu kwa pesa za kodi ili sekta ziingize fedha kwenye pato la Taifa. Kwa mfano,…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eric.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nami kuwa mchangiaji wa jioni hii ya leo. Kama ilivyo ada nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai nami kusimama jioni hii kutoa mchango wangu. Nitaendelea kumsifia na nitaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kwamba baadhi ya watu hawataki. Ni bora niitwe chawa lakini niseme ukweli ili nafsi yangu ibaki huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya makubwa sana kwenye nchi hii, nami niendelee kumwambia Mheshimiwa Rais, yuko kwenye njia sahihi, yuko kwenye taaluma sahihi. Wanaotaka kumtoa nje ya reli hawataweza sisi tukiwepo hai. Tutaendelea kumuunga mkono na tutaendelea kumsifia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunamsifia Mheshimiwa Rais? Leo kwenye Jimbo langu, niliposimama kwenye Bunge hili kwa mara ya kwanza, nilisema tuitoe Liwale Kisiwani, ilikuwa haifikiki kwa mawasiliano ya simu wala kwa barabara, leo Liwale inawasiliana kwa simu, inafikaka. Kesho Liwale inaenda kutoka

Kisiwani kwa upande wa Barabara. Sasa naachaje kusifia? Kwa wananchi wa Liwale, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, jina lake linakwenda kuandikwa kwa wino wa dhahabu. Liwale ilipata wilaya mwaka 1975, mwaka 2023 Mwezi wa Sita tarehe 16 tunaenda kuandika mkataba wa kujenga barabara ya lami kutoka Nachingwea - Liwale mpaka Masasi. Makofi kwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeisoma hii bajeti. Hii ni bajeti yangu ya nane kwenye Bunge hili. Napenda kukipongeza chama changu cha Mapinduzi, na nina uhakika kitaendelea kudumu. Kwa sababu bajeti yake ukiangalia mwaka hadi mwaka inaenda kujibu changamoto za Watanzania, inaenda kujibu matatizo ya Watanzania. Kwa hiyo, kwa namna hii bajeti inavyokwenda kutekeleza; kwa mfano, kwa upande wa kilimo, tumeona fedha nyingi zimepelekwa pale. Lengo letu ni ku-*modernize* kilimo chetu kiende zaidi kwenye kilimo cha kisasa kiwe ni kilimo ambacho kinaongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo ya bei za mazao ya wakulima. Ufumbuzi wa haya matatizo ya bei ya wakulima ni tija. Kama mkulima anaweza kuzalisha korosho kwa Shilingi 1,000/= kwa kilo, hata akiuza kwa Shilingi 1,500/= anapata tija. Kwa hiyo, nai-*support* hii bajeti kwa sababu inaenda kujibu matakwa ya wananchi wa nchi hii. Nani asiyejua kwamba tulikuwa na matatizo ya majengo ya shule za msingi, sekondari na vyuo? Hayo yote yametekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye jimbo langu, kwa upande wa afya, naingia madarakani tukiwa na kituo kimoja tu afya, na tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya. Leo tuna hospitali ya wilaya, leo tuna vituo vitano vya afya. Sasa nani ataweza kusema kwamba hashukuru? Kwanza kwenye dini zote wanasema, usiposhukuru kwa kidogo na usipomshukuru mwenzio, basi hata Mwenyezi Mungu naye huwezi kumshukuru. Sasa sisi tunaendelea kupongeza kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa, mimi nimekabidhiwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye Jimbo

langu la Liwale. Leo hii nakwenda kifua mbele, nina miaka miwili mbele tayari asilimia zaidi ya 70 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa. Kwa nini Chama cha Mapinduzi kisiendelee kuongoza? Baada ya kuyasema hayo, naomba nitoe ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti tumesema tumefuta ada kwenye vyuo vya ufundi na tumeweka mkopo kwenye vyuo vya kati, lakini turudi nyuma tuulize, zamani mimi nakumbuka waliokuwa wanafanya vizuri shule ya msingi walikuwa wanapelekwa shule za ufundi, nami ni muhanga wa watu hao. Hebu chukua historia, wewe umekwenda shule ya ufundi, umemaliza; umeenda chuo cha ufundi, umemaliza; mchukulie yule uliyemwacha darasa la saba akaenda shule hizi za kawaida, akachukua uhasibu, baada ya miaka 10 mkutane. Wewe una *FTC* yako, yule ana *CPA* yake ya uhasibu. Nani ana maisha mazuri? Mzazi gani atampeleka mwanaye akasome ufundi? Utakwenda kuhangaika na vyuma huko miaka nenda rudi wakati yule uliyemwacha darasa la saba, amekwenda amechukua uhasibu, leo ana maisha mazuri. Kwa hiyo, watu wanachotafuta zaidi ni maisha mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ni nzuri. Naomba tunapowahitaji hawa wahitimu wa vyuo vya ufundi, tuangalie wanakwenda kuishi maisha ya aina gani? Mchukulie fundi *refrigeration.* Amesoma *refrigeration,* yupo pale Muhimbili. Atahangaika na *refrigeration* pale miaka nenda rudi, lakini kuna mtu amekwenda pale kama mhasibu, kesho kutwa unasikia ana *CPA,* ana mshahara mzuri. Kuna mwingine anakwenda pale kama muuguzi, leo ni Mganga Mkuu. Wewe utakaa pale miaka 20 unahangaika na *switch* za umeme pale kwenye ma-*fridge* mpaka unastaafu. Kwa hiyo, tatizo kubwa lililowafanya watu waache huko kwenye ufundi, ni kwa sababu ya maisha yao. Kwa hiyo, tunapokwenda kuboresha hili, tuangalie na hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu alisema mwenyewe kwamba, kama walipa kodi kwenye nchi hii wakiwa wachache, wanaenda kubeba mzigo mkubwa. Kwa hiyo, kodi inakuwa kubwa. Ili kupunguza hii, ni kuongeza

walipakodi. Ushauri wangu katika hili, tuje na mikakati ya kuongeza walipakodi kwenye nchi yetu. Watanzania kwa asilimia kubwa hawalipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchangiaji mmoja alisema asubuhi, na hiyo ni kweli kabisa. Leo ukienda Kariakoo kuna bei mbili. Kuna bei ya *VAT* na kuna bei isiyo na *VAT*. Maana yake ni kwamba wewe uchague. Ukitoa shilingi 10,000 utalipa *VAT,* ukitoa shilingi 7,000 hupati risiti. Kwa hiyo, twende na mikakati sahihi. Siyo tu kukabana na hao wachache, tuongeze na idadi ya walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, niingie kwenye vifaa vya ujenzi. Nimeona hapo, Mheshimiwa Waziri amesema ameongeza ushuru kwenye *cement*. Hili jambo siyo sawa. Hili jambo haliwezi kuwa sawa. Kwa sababu gani? Leo hii yenyewe ni kwamba tayari vifaa vya ujenzi vipo juu. Sasa ukiongeza kodi tu kwenye hiyo *cement,* mambo yanaenda kuharibika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine wa mwisho kabisa, naiomba Serikali, tumezungumza sana masuala ya wanyamapori. Bahati mbaya sana kwenye Wizara ya Maliasili sikuchangia. Nataka niwaambie, pamoja na ngonjera zote, riwaya zote, sera zote, maelezo yote, hayatoshi, watu wanauawa, watu wanakufa, tembo wanakula mazao. Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yako, Waziri wa Kilimo kwenye bajeti yako, tenga kabisa fedha za kutosha tuletewe chakula sisi wakazi wa Mkoa wa Lindi. Hakuna mazao kule, mazao yote yameisha na tembo. Hakuna neno lolote lile mimi leo nikirudi Liwale kumwambia mwananchi wa Liwale jambo lolote juu ya tembo, akanielewa haiwezekani. Sana sana nitapigapiga chenga tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanyamapori, suala la tembo limetuharibia sana na linaharibu kabisa kabisa sura yote. Unajua mwenye njaa hafundishiki, mwenye njaa haelewi, mwenye njaa siyo mwenzako. Mtu ukitaka kumuadhibu mtu muadhibu na njaa. Sasa sisi Liwale tuna njaa na hii njaa siyo kwamba wavivu na hii njaa siyo kwamba mabadiliko ya tabianchi; ni tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ije na mkakati maalum unaoeleweka. Tunaomba kadhia ya tembo ichukuliwe kwa uzito mkubwa, vinginevyo inaenda kuharibu mazuri yote yanayoendelea kufanywa na Serikali hii na nimesema hapa tunampongeza sana Mama anafanya sana lakini kwenye hili la tembo…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** …linakwenda kumuharibia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deus Clement Sangu atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya katika Taifa hili lakini kipekee kwa miradi mikubwa anayoifanya ndani ya Jimbo langu la Kwela na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla sisi tunampongeza na tunamuombea maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu na timu yote ya wataalamu niwape pongezi kubwa kwa kazi kubwa mnayofanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Leo pamoja na mambo mazuri yaliyosemwa katika *Speech* yako ya Bajeti Mheshimiwa Waziri nina mambo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nililifurahia ni kati ya Wabunge waliosimama kuchangia juu ya hali ya mtaji kwenye Benki zetu za Serikali kwa maana ya *TCB (Tanzania Agricultural Development Bank)* pamoja na *TID Development.* Nimeona katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri mmetenga kiasi cha shilingi bilioni 235 kwenda kuziwezesha benki hizi ili walau

kuzinusuru katika hali ya mtaji lakini kwa namna ambayo nimeona *plan* yenu ya kutenga shilingi trilioni moja ndani ya miaka 10 ili kila benki hizi tatu ambazo ni benki za kimkakati za Serikali ziwe na fedha au mtaji wa shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema lakini muda mliojiwekea miaka 10 ni muda mrefu sana. Ninachoomba mfanye kwa *TCB* mmetanguliza fedha shilingi bilioni 30 na hivi karibuni mnaenda kupeleka shilingi bilioni 101. Jambo hili nawapongeza kwa fedha hizi mnaenda kuinusuru hii Benki inakaa vizuri kimtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo *deficit* ambayo tunatakiwa kuweka pale ni shilingi bilioni 700. Katika Bajeti hii mnapeleka shilingi bilioni 100. Niwaombe ndani ya muda mfupi mfikishe hii shilingi trilioni moja kwenye Benki hii ya Kilimo ili kusiwe *gap* kubwa kwa maana huu mtaji mnaoweka shilingi bilioni 100 msipokaa vizuri mkasubiri hiyo miaka 10, nao utamezwa kutakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika Benki ya *TID Development* (Benki ya *TID* Maendeleo). Ile pale ina *deficit* ya mtaji karibia shilingi bilioni 370. Napo pale mnapeleka shilingi bilioni 100, kutabaki *deficit* karibia ya shilingi bilioni 270. Naomba nazo hizi mzitengee muda mfupi mkakamilishe, mkishindwa kufanya hivyo maana yake hata shilingi bilioni 100 hii itamezwa kutakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkifanya hivyo wazo la kuja na shilingi trilioni moja litafuata baadaye wakati tayari mme-*stabilize* vitabu katika Benki hizi hizi tatu za Serikali. Ni jambo muhimu sana nililotaka kushauri Mheshimiwa Waziri na ulichukulie kwa maanani makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limepigiwa kelele ni suala la ununuzi wa mazao nitaongelea zao la mahindi na Mheshimiwa Waziri Bashe kwenye bajeti hii umesimama zaidi ya mara nne, mara tano umetoa maelezo mazuri kabisa sina mashaka naye. Umetoa maelezo na ulivyosema kauli yako unasema kwamba hatufungi mipaka lakini mnataka m-*regulate*

*export* ya mahindi mkuze wigo wa kodi *(tax base)* ili tayari *export* ya mahindi iwe *reflected* kwenye mapato ya Taifa ni jambo zuri lakini mnapofanya hiyo *approach* muangalie pia *stabilization* ya *price* kwenye zao hili la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya wiki mbili hizi ambapo mko kwenye *transition period* hapa mahindi yalikuwa kilo moja shilingi 800, hivi ninavyoongea ndani ya wiki mbili hapo ambapo mnakuja na hizo *measures* za ku-*control export* ime-*drop* kwenye Mkoa wa Rukwa kutoka shilingi 800 mpaka shilingi 450. Maana yake gunia la shilingi 80,000 lime-*drop* mpaka shilingi 45,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Chochote unachowaza kufanya, *control measure* yoyote unayofanya iwe ya kudhibiti *export* ya mahindi ili nayo ichangie kwenye kodi ya Serikali siyo jambo baya, hakikisha *stabilization* ya *price* ya mahindi isiyumbe kwenye *measures* unazochukua. Kufanya hivyo hakutakuwa unachofanya, madhara yake yako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaenda huko mtaweka hizo sijui *control,* sijui hivi masharti mengi mengi, mta-*discourage* hawa wanaotaka kununua mahindi yetu. Mkisha-*discourage, competitor* wetu wa zao la mahindi mkubwa ambaye anafanya vizuri katika viwango vya juu ni nchi jirani ya Zambia. Ita-*capitalize* masoko hayo na baadaye hata tuje tufungue mipaka, tupunguze nini hatutaweza kupata wateja wa mahindi yetu yatakuwa tayari zao la mahindi lime-*collapse. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo kwamba ni mara ya kwanza itatokea, hapana. Mwaka 2017, 2018, 2019 tulifanya jambo hili hili tukafunga mipaka kwa nia tu moja tu ya usalama wa chakula nchini kwa gharama ya mkulima yaani tunataka tuwe na *food security* kwa *expense* ya mkulima. Tukafunga mipaka, tulipofunga mipaka Zambia ika-*take over* masoko yote ya mahindi. Soko la mahindi likaanguka, tulikuja Bungeni hapa tukapiga kelele Wabunge wote wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tukajenga hoja hapa ikalazimika twende tukachukue *overdraft* ya shilingi bilioni 50 *CRDB* tukanunua na bado Serikali

haikuwa na *capacity* ya kununua kwa sababu mazao yalikuwa yamezagaa hakuna kwa kupeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *measures* zote mnazochukua *we must be very sensitive*. Tuwe tuna *balance,* tuna *balance* hicho tunachosema *food security* ya nchi lakini tunaangalia mkulima tusimuumize kwa sababu unakuta tunafanya haya yote 45, wakulima wameshindwa kukopesheka mahindi mwaka huu. Hamna benki iliyojitolea, *commercial bank* zote hata Benki ya Kilimo ilikataa. Unakopeshaje zao la aina hii ambalo lenyewe halitabiriki? Benki gani inataka kupata hasara? Hamna benki inayomweza kukubali mambo ya namna hii kwa sababu hata ukiangalia Ripoti ya *BOT, performance* kwenye Sekta ya Kilimo mikopo imekuwa ikiyumba sana kwa sababu ya sera zisizotabirika kwenye mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizeti Wabunge wengi wamesema wa Singida na wengine ilikuwa ni zao ambalo tulili-*encourage* wakulima walime na ukienda kwenye *portfolio* ya Benki ya Kilimo walitoa viwanda shilingi milioni 700, 800. Leo hii mikopo ile hailipiki tayari tunaenda kupeleka *non-performing loan* nyingi kwenye Benki ya Kilimo kwa sababu ya sera hizi zisizotabirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kodi zetu tuanvyo-*set* hizi kodi hizi Mheshimiwa Waziri umesema aah tunapunguza mafuta ghafi ya kuingia nchini mjue huko huko benki zetu mnazopeleka huu mtaji mlikopesha wakulima. Tutarudi mwakani benki mitaji ime-*collapse* kwa sababu hakuna *repayment* kwenye Sekta ya Kilimo tumei-*paralyze*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo mliangalie kwa umakini mkubwa muende mkaangalie tu-*balance* mazao hasa mahindi tusikubali wananchi kwa mara ya kwanza wanavuna wakiwa na shilingi 80,000 leo hii shilingi 45,000. Niombe tu utakachofanya chochote Mheshimiwa Bashe iwe *between* shilingi 75,000 na wewe mwenyewe unasema *NFRA* nimeona kwenye Hotuba ya Waziri mnaenda kununua tani laki nne lakini kwenye mfumo tu wa *NFRA* una *ambiguity* na una *anomalies* nyingi sana ambazo zinakwanza kwenye manunuzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza moja, hamna *infrastructure* za kutosha, vituo tu vya kutosha vya kukusanya mazao ya wakulima havitoshi kwa sababu inabidi mkulima asafiri kilometa nyingi kuja kufuata *NFRA* ilipo. Jimbo langu la Kwela unajua kwa mfano mtu anatakiwa asafiri kilometa 100 na zaidi kufuata kuuza unakuta anaenda kuuza tena anaondoka pale anakuta tena pale kuna *bureaucracy* nyingi. Watu wenye nguvu za fedha wanateka masoko, wao ndiyo wanakuwa wa kwanza kupima. Mkulima anayepeleka mahindi kwenye toroli kamwe hawezi ku-*access NFRA* kwa hiyo, niombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bado wananchi wamekuwa wana *complain* hata vipimo vinavyotumika pale sehemu nyingi tuna analogia. Wakulima wanakuwa wananung'unika tuna punjwa. Nendeni hata *NFRA* na *CPB* taasisi zako mtakazoenda muende na mizani ya *digital* ili mkulima asiibiwe mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu kwa sababu tumeona zao la mahindi ni tija, kwa nini tusiendelee ku-*pump* hela nyingi? Siyo lazima tuchukue huko, twendeni kaongezeni *overdraft* na nyie mnunue kwenye *competitive price* mahindi kuliko haya mambo mengi tunayoongea ni mazuri tu ni lugha *very cosmetic* lakini *implication* yake kule siyo hivyo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimekwambia *very frankly* na hiyo *measure* tukachukue tuhakikishe mkulima wa mahindi hatumuumizi tukanunue bei ya kuanzia shilingi 75,000 na kupanda. Chini ya hapo ni maumivu. Tuli-*subsidize* mbolea maana yake nini?

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sangu taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Swalle.

**TAARIFA**

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Deus Sangu kwamba

hii bei ya mazao ya wakulima wameuza bei nzuri ya shilingi 800, 700 kwa kilo shambani na yako mashamba yako umbali wa kilometa zaidi ya 150 kwenye masoko ya *NFRA* kwa hiyo, tukisema wakapeleke huko sokoni watapata hasara. Hili Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alizingatie sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus taarifa unaipokea?

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea ni msisitizo wa jambo hili. Hili tunalo Mheshimiwa Bashe tunaendelea nalo mpaka tufikie *consensus* mahali ambapo kutakuwa *win win,* Serikali i-*win* na mkulima a-*win.* Nihame hapo nadhani *message* itakuwa imefika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa nataka kuchangia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ifikapo nyakati kama hizi tunapoelekea mwisho wa mwaka wa fedha mifumo yote halmashauri ina *paralyze* haifanyi kazi. Mfano kwenye halmashauri yangu siku 20 sasa hamna *business* yoyote inayo-*transact.* Wanasema mifumo imekwisha. Tumefika mahali tulikuwa tunachukua hata kwa wazabuni mafuta, sasa hivi hata *ambulance* zinaenda kukosa mafuta ya kujaza pale kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni kama inafikia hatua mnapofuga mwaka wa fedha kuna shida kwenye mifumo yenu, muwe na *alternative* ya ku-*attend emergencies* za Serikali kwa sababu hatuwezi tukasema mifumo imekufa, kwa hiyo, watu wafe mahospitalini? Kwa hiyo mambo yale *basic* ya muhimu yasiende? Lazima mtafute *alternative* ya kuwa na namna ya ku-*rescue* yale mambo ya dharura ili sasa isiwe kwamba mifumo ime-*paralyze* nchi nzima hamna kinachoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya kwenye halmashauri tayari kuna wazabuni, wazabuni ambao walifanya kazi. *Maturity obligation* zao kwa maana ya wanahitaji kulipwa sasa mifumo imefungwa tutakuja tuletewe riba ya kucheleweshewa malipo tunaingiza hasara Serikali, kwa hiyo niwaombe jambo hili utakapokuwa una *wind up* utueleze vizuri limekaaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umeisha.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Juma Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi, nishukuru Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa Bajeti ambayo hii tunaendelea nayo. Hii inatupa moyo sana na ninaanza kwa kuiunga mkono Bajeti hii mpya ambayo tunakwenda nayo kwa sababu Bajeti iliyopita imetufanyia makubwa na imewatekelezea wananchi kazi kubwa za kimaendeleo kwa maana hiyo ninaanza kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Bajeti hii kwenye vipengele vingi lakini hasa hususan hapa kwa kuondoa ada kwenye vyuo vya ufundi kwa kweli umewapunguzia, Serikali imewapunguzia sana mzigo wananchi lakini pia kwa kuweka mikopo katika vyuo vya kati kwa kweli wazazi wamepunguziwa mzigo mkubwa na watoto sasa wana uhakika wa kwenda shule. Kwa hiyo kwa ujumla niipongeze Bajeti ni nzuri na ni ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina baadhi ya ushauri wa mambo ili twende sawa. Katika utekelezaji wa Bajeti iliyopita bado kuna miradi ambayo haijakamilika kwa sababu tofauti tofauti. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba miradi ile inakamilika, tuangalie vipaumbele vyetu ambavyo tuliviweka halafu tuhakikishe vinakamilika. Mfano miradi ya maji, iko miradi ya maji ambayo inaendelea katika majimbo yetu. Ni vyema ile miradi ya maji tuhakikishe tunapoelekea mwisho huu wa bajeti tuhakikishe ile miradi inawekewa mipango mizuri ya kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya maji wakandarasi wamekuwa ni dhaifu sana, wamekuwa hawana uwezo na hata wakipewa fedha na Serikali wanakimbia kimbia. Sasa sijajua hii miradi ambayo wakandarasi wamepewa hela na Serikali wanakuwa na visingizio. Mfano kuna miradi miwili ya maji visingizio vikubwa vinakuwa ni ukosefu wa mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii inachukua muda mrefu sana. Mradi wa shilingi milioni 800 unatekelezwa toka Bajeti ya mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na mwaka huu unakwenda ni wa tatu lakini Bajeti hiyo inaendelea kutekelezwa, kutekelezwa mpaka sisi sasa wawakilishi wa wananchi tunashindwa kwenda kufanya mikutano kule kwa sababu kila siku ukienda hadithi ni hiyo hiyo. Kwa hiyo, nataka hili hebu lifanyiwe kazi na liishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano pale kwetu kuna wakandarasi wawili walipewa hela na Serikali lakini visingizio mwaka mzima mabomba hakuna. Sasa kama mabomba hakuna lazima Serikali ione namna ya kuikwamua hii miradi ili wananchi waanze kufikiria miradi mingine. Lakini miradi mingine kama mradi ule wa mjini tunaishukuru Serikali juzi imetoa shilingi milioni 600, *certificate* ya yule mkandarasi na amepata matumaini ya kuendelea na mradi. Mradi uko 72% na zaidi lakini alikwama kwa sababu fedha zilichelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba miradi hii ambayo ni muhimu sana, ni miradi ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Rais ameweka ahadi ya kuwatua ndoo wakina mama kichwani tuiangalie lakini miradi mingine ni miradi ile ya visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Bajeti mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na huu ni mwaka wa tatu. Mwaka wa kwanza tunachimba visima, mwaka wa pili tunafanya *feasibility study,* mwaka wa tatu ndiyo tunaanza usambazaji. Jambo hili linatukatisha tamaa, ni bora miradi hii yenyewe siyo gharama kubwa sana. Mradi wa kuchimba kisima na kusambaza kwenye mitaa yetu yawezekana shilingi milioni 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri Serikali inapokuja na miradi ya namna hii ya muhimu ya maji basi ije na mradi uliokamilika, wachimbe kisima kwa wakati huo huo wakati wana chimba kisima, basi wataalamu wawe wameshafanyia *feasibility study* ili waanze kusambaza kuliko kisima kinakaa mika mitatu hakijapelekewa fedha za usambazaji. Kwa maana hiyo tuna visima zaidi ya 10 kwenye Jimbo la Kondoa Mjini vinahitaji usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii kwa Bajeti hii tutachimba tena visima vingine, vile vya mwanzo hatujavisambaza. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali hebu iangalie miradi yote ambayo tayari imekwisha peleka fedha nyingi basi tuimalizie kwa kuikamilisha ili iweze kuanza kutumika na tuanze kubuni miradi mingine kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo jingine la kukumbusha. Ilani ya CCM bado nazungumzia Barabara inayotoka Tanga kuja Mrijo kwenda Kwa Mtoro kwenda Singida. Ninaamini Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiyo Mwenyekiti wa CCM anaifahamu barabara hii ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na imetamkwa vizuri sana itatoka Mondo itakuja Mpaka Bicha. Sasa tumeweka juzi tulihudhuria sherehe ya kusaini mkataba wa hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika matamko ya Mheshimiwa Waziri kile kipande hakijatajwa. Ninashukuru kwenye Hotuba ya Bajeti kipo nimekiona. Kwa hiyo, nadhani Serikali izingatie ule Mpango uliopo kwenye Ilani ya CCM kwa maana hiyo ninaomba wakati tuanendelea kujenga ile barabara tujue kabisa barabara iliyotajwa kwenye Ilani ya CCM inatoka Mondo kuja Bicha na yenyewe izingatiwe katika hii hatua hii ambayo tumesaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tumekuwa tukizungumza mara kwa mara hili Daraja la Munguri B. Ni muhimu sana daraja hili likajengwa mapema kwa sababu sisi Wanakondoa na Watu wa Hanang' tunalitegemea sana kwenye shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi alikuwepo Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Daniel Chongolo katika Jimbo langu kuzungumzia na alimwita mtaalamu kuzungumzia. Sababu ambazo zinatolewa haziridhishi kusema kwamba daraja lile lisijengwe. Wamekwenda kufanya *feasibility study* kwenye eneo refu la mita 500 wakati daraja la awali lilikuwepo mita 100 ambalo linaweza likatumia fedha ndogo ambayo walikuwa wanaangalia kwamba *economic not viable* wakashindwa kulijenga kwenye hiyo mita 500 ilitakiwa wale wataalamu wangeenda kuchukua vipimo kwenye eneo la zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa lazima wataingia gharama mara mbili. Wamekwenda kufanya uchunguzi lakini wamekwenda wamekuja na matokeo ambayo Serikali wanasema haiwezi kujenga daraja kwenye eneo lile ni refu wanatakiwa waanze tena upya kuja kupima kwenye eneo la zamani ambalo ni mita 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa kwa nini kwa gharama ile ile wasingepima kule pafupi ili wafupishe huu mlolongo mrefu wa kujenga hiyo daraja? Daraja hiyo inapoteza magari ya watu yanazama, watu wana umia, watu wanaingia gharama kuvushwa kwenye daraja lile hata kama haifai kiuchumi lakini Serikali yetu lazima ijue maeneo yale ni maeneo ya wananchi na wananchi wanaingiza vipato kwa kilimo ng'ambo ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishapeleka fedha eneo lile kwenye Pori la Swagaswaga. Wamejenga mageti, wamejenga hosteli unasemaje sasa tena kiuchumi haifai wakati tayari umekwishapeleka fedha upande ule? Kwa hiyo, lile daraja likijengwa hata hao watalii ndiyo watapita, vinginevyo masika yote hata kama tutakuwa na watalii hawawezi kupita kwa sababu daraja linapitisha maji na mto unapitisha maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara ya Ujenzi ichukulie *serious* ujenzi wa daraja hili ambalo linaunganisha mikoa miwili Dodoma pamoja na Mkoa wa Manyara. Kwa hiyo nilikuwa nakumbusha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na ujenzi wa sekondari unaendelea huu wa mradi wa *SEQUIP*, tulikuwa na ile awamu ya kwanza tunashukuru Serikali ilituletea fedha. Jimboni kwangu tumekamilisha ile sekondari na leo wanafunzi wanasoma kidato cha kwanza na kidato cha pili, tunasubiria basi ile awamu nyingine ya pili. Na sasa hivi halmashauri ndio hivyo zinakwenda kufungiwa yao tunakwenda kumaliza. Sina uhakika kwamba hizo fedha zitakuja katika kipindii hiki kabla mwaka wa bajeti haujaisha ama tutatarajia zitakuja kwa mwaka mwingine unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tujenge sekondari nyingine hiyo Kata ya Bolisa ambayo miaka mingi wamekuwa wakisubiri kata yao wanakwenda kusoma kata nyingine. Kwa hiyo tunataka tujue sasa ile fedha itaingia sasa au tutaivusha kwenda kwenye bajeti? Na kama tukiiivusha mwaka unaofuata sekondari tutajenga nyingine? Kwa hiyo nilitaka nifahamu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kufanya kazi nzuri ya uhifadhi. Leo ukiona Waheshimiwa Wabunge wote wanalalamika tembo wamekuwa wengi maana yake Wizara imefanya kazi kubwa ya kuwalinda hao tembo ambao walikuwa wanakwenda kupotea kutokana na majangili. Tunawapongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa namna walivyoweza kulinda hifadhi zetu mpaka leo sisi Wabunge wote takriban, maeneo mengi tunalalamika tembo wamekuwa ni kero maana yake kazi yao wameifanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachotakiwa kufanyika ni lazima sasa ipangike mikakati kama Serikali tumeweza kupanga mikakati mizuri ya kuhifadhi hifadhi zetu wanyama wetu leo wameongezeka basi wasije wakawa tena kero kwa wananchi. Bajeti hizi zinatakiwa zizingatie mambo haya. Kwamba tumeweza kuhifadhi sasa, tembo wamekuwa wengi ni namna gani tunaweza kuwadhibiti tena isiwe ni dhahma kwa wananchi. Maeneo mengi na Serikali inatumia fedha nyingi sana kwenda kulipa vifuta jasho na vifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa kwenye jimbo la dada yangu Dkt. Ashatu Kijaji juzi wakati wa Katibu Mkuu, mwananchi anaongea kana kwamba sasa anajua kabisa anakwenda kulima,

nikishalima tembo watakuja kula Serikali ijiandae kulipa kifutamachozi sio sawa. Kwa sababu kifutamachozi chenyewe kinachotoka tunafahamu wote hakitoshi. Mtu analima heka kumi analipwa hela za kununua gunia mbili; hii haifai. Kwa hiyo Serikali iweke mikakati mizuri ya kuwadhibiti hawa tembo kwa sababu wamekuwa waharibifu. Ikiwezekana kama wanauzika watangaze soko, wawauze tembo kwa mwenye kuwataka ili wapungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nashukuru sana ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nina imani kwa sababu ni wa mwisho nitapata hata dakika 15. Cha kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa nafasi hii ya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutoa mchango wangu kwenye bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wakulima hapa nchini hasa wakulima wa tumbaku, wakulima ambao walifkia hatua ya kukata tamaa. Lakini kwa uwepo wa Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan; wanunuzi walikuwa wameshaondoka nchini; hivi tunavyoongea leo wanunuzi wa tumbaku Tanzania ni wengi. Bei ya tumbaku sasa imepanda kutoka dola 1.4 leo wastani wa bei ya tumbaku inayozunguka kwa wakulima wetu katika mikoa yote inayolima tumbaku ni wastani wa dola 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, niendelee kukuomba sana wakulima wa tumbaku wanahitaji waione dola 4 kwenye bei yao, wakulima wa tumbaku wanataka waone bei inazidi kuongezeka. Tunaomba uendelee kutupunguzia kodi ambazo zinabana wanunuzi wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kazi unayoifanya ni nzuri sana, bajeti yako imekaa vizuri, hotuba yako ilishiba vizuri sana. Ombi langu hili; mwaka jana kwenye bajeti nilikuomba sana tuondolee kodi kwenye *Hanson cross* ili wakulima wa tumbaku waweze kupata faida kubwa. Tuondolee kodi kwenye ushuru wa *duty twine* ili wakulima wa tumbaku waweze kupata faida kubwa. Waondolee wanunuzi ushuru wa mionzi wanapata shida kubwa sana. Tunahitaji ushuru uendelee kupungua kwa sababu Mheshimiwa Rais anahitaji wakulima waende kulima, wakulima waweze kupata faida kubwa sana. Kwa hiyo niendelee kukupongeza Mheshimiwa Waziri ulianya kazi kubwa sana bajeti yako imeshiba vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais. Kwenye Jimbo la Ushetu leo tunavyoongea tulikuwa na barabara zetu ambazo zilikuwa hazijafunguka. Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani tulikuwa na mtandao wa barabara kilometa 400 tu lakini leo mtandao wa barabara katika Jimbo la Ushetu ni zaidi ya kilometa 1029 ni kazi kubwa imefanywa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ilikuwa haifanyi kazi, leo tumewekewa *x-ray* tuna vifaa vyote vimejaa, watalamu wetu kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu inafanyika, *operation* zinafanyika pale pale. Wananchi wa Ushetu sasa hawaendi tena katika Manispaa ya Kahama kazi inafanyika vizuri katika Halmashauri yao ya Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumwomba tu Mheshimiwa Waziri. Tuliahidiwa Kituo cha Afya Ulowa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Kata ya Ulowa aliahidi ujenzi wa kituo cha afya tangu mwaka 2017, leo miaka zaidi ya mitano hakuna kituo cha afya hakijajengwa, Mheshimiwa Waziri tupelekee fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuiomba Serikali walituahidi kilometa 54 za lami, nashuhudia tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu wana-*sign* mikataba, mikataba inazinduliwa kwenye majimbo ya wenzangu. Mheshimiwa Waziri hebu nipelekee fedha na mimi kwenye kilometa 54, kwenye hii

barabara ambayo iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Aliahidi marehemu Magufuli sasa barabara ile bado haijaanza kujengwa. Tuombe basi angalau kwenye bajeti hii tukazindue, tukasaini na wewe uwepo kwenye uzinduzi wa barabara inayotoka Kahama inapita Nyandekwa, inapita Ukune, inapita Kisuke, inapita Nyambilangano inaenda Uyogo inaunganisha mpaka kwenye Jimbo la Kaliua kwa ndugu yangu Mbunge wa Kaliua. Tuwekee na sisi historia kwenye Jimbo la Ushetu tupate angalau hata lami ya kipindi cha utawala wa Mheshimiwa Rais pamoja na wewe ukiwa Waziri wa Fedha ya kuweza kupigia picha wananchi wa Ushetu, tunakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais mwaka jana ametupa zaidi ya 2,080,000,000 madarasa yamejengwa vizuri; lakini ametupa shule mpya mbili zaidi ya milioni 800 shule zimejengwa na zimeshakamilika zinafanya kazi. Niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba, tuna kilio kwa wakulima wa pamba. Hali ya wakulima wa pamba bei inazidi kuporomoka niendelee kukuomba kuwepo na mfuko wa pembejeo. Kuwepo na mfumo wa kinga ya mazao hasa mazao ya kimkakati kipindi bei ya masoko inapokuwa imetikisika. Leo hii wakulima wa pamba wametumia gharama kubwa kuzalisha zao lao, wamelima pamba nyingi, wamehamasika hasa baada ya kupelekewa mbegu za pamba kwa bei ya ruzuku. Tunaomba sasa, kama mtikisiko wa bei ya pamba inapokuwa mkubwa hivi kwenye mazao yetu ya kimkakati tuwe na maandalizi, tusisubiri mpaka tukio litukute halafu ndipo tuanze maandalizi. Leo hii bei ni 1,060 mpaka inaenda mpaka shilingi 1,000 lakini wakulima wanalia wanasikitika bei ya pamba imeporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe sasa, kama mwaka mmoja korosho ilishuka bei Serikali yetu iliweka mkakati wa kuzinunua korosho zote na bei iliongezeka na Serikali ikaja kuuza. Mafuta yalipanda bei Mheshimiwa Rais akaamua kuweka bilioni 100 kwa kila mwezi; lakini pembejeo pia mmeweka ruzuku kwa nini sasa mtikisiko huu wa bei msijifungie wataalamu ambao Mheshimiwa Rais akaamini mkaweka ruzuku ili wakulima wetu wa

pamba waweze kupata bei nzuri? Kwa sababu wamehamasika kulima pamba vizuri. Sasa wanapopata beii ndogo imeshuka, tunawashusha tena wanashuka chini hawawezi kulima pamba mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa sababu uko hapa lichukue hili kwa ajili ya kuweka kinga ya mazao tuwe na mfuko wa kinga ya mazao ya kimkakati tunapoingia kwenye mtikisiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa tumbaku wanahitaji kulipwa fedha zao kwa dola. Tunapata taarifa kwamba wakulima wa tumbaku inawezekana wakalipwa shilingi kitu ambacho ni hatari sana. Wakulima kwenye mkataba wetu wa halmashauri ya tumbaku malipo yanafanyika kwa dola, makato ya bei yao wamekatwa kwa dola iweje sasa malipo yaende kwa shilingi? Na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anahutubia hapa kwenye mpango wa bajeti yake amesema Serikali ina akiba ya dola zaidi ya 1,177,000…

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu iweje leo dola…

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kakoso.

## TAARIFA

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi ya kumpongeza ndugu yangu Cherehani na kutoa taarifa juu ya anachokizungumzia. Zao la tumbaku limekuwa na uhimilivu wa kuuzwa kwa bei nzuri kwa sababu ya makubaliano yado la, pembejeo zinakopwa kwa dola, mauzo yote yanafanyika kwa dola. Sasa tunapofikia hatua ya kutaka kuuza kwa shilingi ni kuwaua wakulima naomba sana dola iendelee kuliko mapendekezo yalivyo kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani taarifa unaipokea.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii kwa sababu wakulima wana matumaini, wana imani kubwa na Mheshimiwa Rais, wana imani kubwa na Waziri wa Kilimo lakini wana imani kubwa na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo tunaomba wakulima wetu wa Tumbaku waendelee kulipwa kwa dola kama utaratibu ambao tumejiwekea kwenye Halmashauri ya Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukuomba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, kuhusu Kahama. Kahama ningeomba tuitenge kuwa lango la biashara kwa Kanda wa Ziwa pamoja na nchi za maziwa makuu kwa sababu ninavyoongea tu mawasiliano katika Manispaa ya Kahama ni makubwa. Nikikutajia tu hapa na wewe unaweza ukajua kwamba kweli Kahama inastahili kuwa lango la kibiashara kwa sababu wakulima wetu na viongozi wetu na wananchi wetu sio lazima waende Kariakoo kuhemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa sasa kanda ya ziwa na sisi tuwe na ukanda wetu tutengeneze Kariakoo katika ukanda wa maziwa makuu. Ukiangalia mwaka 2019 Manispaa ya Kahama ilikusanya bilioni saba, mwaka 2021 walikusanya mapato katika Manispaa ya Kahama bilioni 9.6, mwaka 2022 walikusanya bilioni 9.6 na mwaka 2023 Kahama wamekusanya zaidi ya bilioni 10 kwa miaka mitatu Kahama imekusanya zaidi ya bilioni 35. Iweje sasa tusiitenge kuwa ni lango la kibiashara? Kuna eneo limetengwa Dodoma ukienda wafanyabiashara wamejaa pale wengi zaidi ya 1,500. Biashara zilizosajiliwa tu Kahama ni zaidi ya 8,558.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tu magari ya nchi jirani yanayopita Kahama kwa siku ni zaidi ya 446 mpaka 600, na yanayolala pale Kahama ni zaidi ya magari 200. Kwa nini tusifanye Mji wa Kahama kama lango la kibiashara kwa ukanda wa maziwa makuu ili makusanyo ya kodi na mtandao wa kodi kwenye Serikali yetu uwe mkubwa? Kwa sababu tunaangalia wananchi wengi wanakwenda kuhemea mpaka wafike Kariakoo, mpaka waende Dar es Salaam. Wananchi pia na

wafanyabiashara wanaposafiri kwa muda mrefu gharama za uendeshaji inaongezeka na biashara zina bei zao zinaongezeka lakini wanapoishia Ukanda huu wa Kahama, ina maana biashara yetu, wafanyabiashara na wakulima wanaweza wakaendelea na vitu vyao hapa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji Mheshimiwa Cherehani kwamba Mji wa Kahama pamoja na biashara kubwa zinazokuwepo pale Kahama sasa hivi wapo maafisa wa *TRA* ambao si waadilifu na wanadharau mpaka kauli za viongozi wa Taifa kwamba habari ya kudai kodi za miaka mitano nyuma hizo ni kauli za kisiasa. Kahama ndiyo yanayofanyika, wanataka kuuwa ule Mji wa Kahama, naomba uendelee Mheshimiwa Mchangiaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani taarifa unaipokea.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa wananchi wa Kahama wanalalamika, wafanyabiashara wanalia na akina mamantilie wanateseka. Na kwa kuwa Rais wetu ni msikivu na Waziri wa Fedha uko hapa, ninaomba tenga muda, kaa na wafanyabiashara wa Kahama wasikilize ni wachangiaji wazuri sana wa mapato ya Serikali. Kama ni madeni yaliyoko kwa wafanyabiashara waiteni mzungumze nao, waiteni muwasikilize, walipe kidogokidogo. Na, nikupongeze juzi ulisema wafanyabiashara wasifungiwe biashara zao, akina mamantilie wasifungiwe biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mamantilie anauza nyanya, anauza biashara yake ya hoteli anafungiwa anawekewa *seal* sasa baada ya siku mbili, tatu ndio wanaenda kumfungulia. Hebu niambie zile nyanya zinakuwa na hali gani? Kama ni kanyama ka kuku kale katakuwa na hali gani? itakuwa imeshaharibika mama amekopa kwenye halmashauri, akina mama wamekopa benki. Tunaomba Serikali ipo ilifanyie kazi, biashara Mji wa Kahama uendelee kukua kwa kuwa ni tegemeo kwenye ukanda wa maziwa makuu nchi za maziwa makuu pamoja na mikoa yetu ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja nishukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chereheni.

Waheshimiwa Wabunge orodha yetu kwa jioni ya leo imekamilika. Nitumie nafasi hii kuwapongeza wale wote waliopata nafasi ya kuchangia pia kwa upande wa Serikali pia kwa kupokea mapendekezo na hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.00 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi ya Siku ya Alhamisi, Tarehe 22 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*

Na. 685

**Ujenzi wa Barabara ya Karatu – Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami Kilomita 76 za barabara ya Karatu – Mbulu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. *ENG.* GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo kwenye maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami kwa utaratibu wa *EPC+F (Engineering, Procurement, Construction plus Finance)*. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti – Lalago hadi Maswa yenye urefu wa kilomita 389, ambapo barabara ya Karatu hadi Mbulu kilomita 72 ni sehemu ya barabara hii. Hadi sasa Mkandarasi

amepatikana na mkataba wa kuanza ujenzi umesainiwa Tarehe 16 Juni, 2023. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.